# MICHAKATO NA MBINU ZILIZOTUMIKA KATIKA UUNDAJI WA MAJINA YA MITAA KATIKA WILAYA YA MJINI UNGUJA

**MOZA OMAR RASHID**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA SEHEMU YA MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA ISIMU YA KISWAHILI YA CHUO KIKUU HURIA TANZANIA**

**2017**

## UTHIBITISHO

Aliyetia saini hapo chini anathibitisha kwamba, ameisoma tasnifu hii iitwayo michakato na mbinu zilizotumika katika uundaji wa majina ya mitaa katika katika wilaya ya Mjini Unguja na anapendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kutimiza sehemu ya sharti la kutunukiwa shahada ya M. A Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

______________________________________

**Dkt: P.P. Lipembe**

**(Msimamizi)**

Tarehe_________________________

## HAKI MILIKI

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, au kutoa tasnifu hii kwa njia yoyote ile Kielektroniki, Kurudufu nakala, Kurikodi bila ya idhini ya mwandishi au idhini ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa niaba ya mwandishi.

## TAMKO

Mimi, **Rashid, Moza Omar**, nathibitisha kuwa hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada hii au nyingine yoyote.

__________________________

Sahihi

__________________________

Tarehe

# TABARUKU

Natabaruku kazi hii kwa watoto wangu wapenzi, mume wangu mpenzi na mama yangu mpenzi Bibi Maryam Mfaume Abdalla, kwa kunilea kwa mapenzi na kunisomesha.

## SHUKRANI

Kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kukamilisha tasnifu hii nikiwa mzima wa afya. Kisha shukrani zangu nyingi zimuendelee msimamizi wangu Dr. P. Lipembe ambaye muda wote alikua na mimi kwa kuniongoza, kunielekeza pamoja na kunipa ushauri bora na wa hekima uliochangia kwa kiwango kikubwa sana kukamilisha kazi hii nzito. Bila ya maelekezo yake, masahihisho na ushauri wake nisingeweza kufikia hapa nilipofikia.

Ninampa shukrani za dhati kutoka moyoni mwangu mama yangu mzazi Bi. Maryam Mfaume Abdalla, mume wangu Mohd Saleh Mohd , na watoto wangu Kauthar Mohd, Hunayfah Mohd na Atqa Mohd na familia yangu kwa ujumla pamoja na ndugu, jamaa na marafiki wote kwa kunivumilia na kuwa na mimi bega kwa bega katika hatua zote za utafiti wangu. Kwa kweli walinifariji na kunipa moyo na furaha muda wote wa utafiti wangu. Uvumilivu wao kwangu na uchangamfu wao ulizidi kunipa hamu na shauku ya kuikamilisha kazi hii kwa utulivu zaidi.

Nawapa shukrani zangu za dhati pia Mw. Ali Mwalim wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Ndugu Suleiman Almas wa Mwera Mwembemchomeke na Mwalim Ramadhani wa Idara ya Makumbusho Mnazimmoja. Bi Najat Mohd Khamis wa Kwarara Zanzibar, Mw. Mussa Khamis wa Skuli ya Kiembe samaki sekondari Zanzibar, walimu wenzangu wote wa Skuli ya Kiembe samaki msingi” A”na wanafunzi wenzangu wote wa Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa msaada wao mkubwa walionipa katika kufanikisha utafiti huu.

Shukrani zangu ziwafikie pia Bwana Ramesh Dayal Ramji wa Sokomuhogo, ndugu Fardi Juma Mohd wa Mlandege Zanzibar, wafanyakazi wa Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa kwa mchango wao wenye tija katika mchakato wa kufuatilia majina ya mitaa mbali mbali.

Pia, ninakishukuru Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa kuniamini na kunipa fursa ya kuendelea na masomo yangu ya shahada ya uzamili kikamilifu. Kwani hii ni fursa adhimu kwangu ambayo imenikuza sana katika kupata elimu na mwamko wa mambo mbali mbali yahusuyo fani yangu.

Mwisho, kwa kuwa sitoweza kuwataja wote, nawapa shukrani wale wote ambao wamechangia kwa namna moja au nyengine na kunipa msaada wa hali na mali katika kufanikisha tasnifu hii. Ninathamini michango yao yote na Mola awape afya njema na maisha yenye kheri na baraka.

# IKISIRI

Tasnifu hii inawasilisha uchunguzi uliofanywa kuhusu michakato na mbinu zilizotumika katika uundaji wa maneno ya mitaa mbalimbali katika wilaya ya Mjini Unguja. Malengo mahususi yalikuwa ni pamoja na kubainisha vigezo, kuelezea michakato iliyotumika kupata majina hayo, na kubainisha umuhimu wa majina ya mitaa katika kukuza lugha ya Kiswahili. Utafiti ulitumia muundo wa maelezo na takwimu Utafiti ulifanyika katika wilaya ya Mjini Unguja. Walengwa wa utafiti walikuwa ni wakaazi wa wilaya ya Mjini Unguja. Usampulishaji ulifanywa kwa kutumia njia ya usampulishaji tabakishi. Jumla ya watafitiwa 90 walihusishwa katika utafiti huu. Ukusanyaji wa data ulifanywa kwa kutumia njia za mahojiano (usaili), uchunguzi makini, dodoso na mapitio ya nyaraka. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa; vigezo vilivyotumika katika kutoa majina ya mitaa katika wilaya ya Mjini Unguja ni vya kimaumbile, kijamii na kiuchumi.. Utafiti umeonesha kuwa njia ambayo imetumika zaidi katika kuita majina ya mitaa katika wilaya ya Mjini Unguja ni njia ya uambatishaji wa maneno. Majina hayo ya mitaa yamechangia sana katika kuleta misamiati mipya hasa ya maneno ambatano. Utafiti umeonesha pia kuwa maneno ambayo yametumika kuita majina ya mitaa katika wilaya ya Mjini Unguja yametokana na miundo mbalimbali ya maneno na muundo uliotumika zaidi ni mwambatano wa nomino na nomino. Utafiti umedhihirisha pia kuwa majina ya mitaa yameweza kudumisha maneno ya Kiswahili yenye hadhi kubwa kwenye lugha ya Kiswahili na kuhifadhi historia na urithi wa lugha yetu

# YALIYOMO

**UTHIBITISHO** ........ **ii**

**HAKI MILIKI** ........ **iii**

**TAMKO** ........ **iv**

**TABARUKU** ........ **v**

**SHUKRANI** ........ **vi**

**IKISIRI** ........ **viii**

**YALIYOMO** ........ **ix**

**JEDWALI** ........ **xiv**

**ORODHA YA VIELELEZO** ........ **xv**

**ORODHA YA PICHA** ........ **xvi**

**ORODHA YA RAMANI** ........ **xvii**

**SURA YA KWANZA** ........ **1**

**1.0 UTANGULIZI NA USULI WA UTAFITI** ........ **1**

1.1 Utangulizi ........ 1

1.2 Usuli wa Tatizo ........ 3

1.3 Kauli ya Tatizo la Utafiti ........ 3

1.4 Lengo Kuu la Utafiti ........ 4

1.5 Malengo Mahsusi ........ 4

1.6 Maswali ya Utafiti ........ 5

1.7 Umuhimu wa Utafiti ........ 5

1.8 Mipaka ya Utafiti ........ 6

1.9 Matatizo ya Utafiti ........ 6

1.10 Hitimisho ........ 7

**SURA YA PILI** ........................................................................................... **8**

**2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA** ....... **8**

2.1 Utangulizi ........................................................................................... 8

2.2 Jamii na Makaazi ........................................................................................... 8

2.3 Dhana ya Utambulisho ........................................................................................... 8

2.3.1 Utambulisho wa Kiisimu ........................................................................................... 9

2.3.2 Utambulisho wa Kijamii: ........................................................................................... 10

2.4 Dhana ya Majina na Aina zake ........................................................................................... 11

2.5 Mchakato wa Utoaji wa Majina ........................................................................................... 13

2.6 Vigezo Vilivyotumika kutoa Majina ya Mitaa ........................................................................................... 15

2.6.1 Vigezo vya Maumbile ........................................................................................... 15

2.6.2 Vigezo vya Kijamii ........................................................................................... 15

2.6.3 Vigezo vya Kiuchumi ........................................................................................... 15

2.7 Kazi Tangulizi Zinazohusu Dhana ya Majina ya Maeneo ........................................................................................... 16

2.8 Tafiti Tangulizi Zinazohusu Majina ya Mahala ........................................................................................... 20

2.9 Umuhimu wa Majina ya Mitaa ........................................................................................... 25

2.10 Pengo la Utafiti ........................................................................................... 27

2.11 Kiunzi cha Nadharia ........................................................................................... 27

2.12 Hitimisho ........................................................................................... 29

**SURA YA TATU** ........................................................................................... **30**

**3.0 MBINU ZA UTAFITI** ........................................................................................... **30**

3.1 Utangulizi ........................................................................................... 30

3.2 Muundo wa Utafiti ........................................................................................... 30

3.3 Eneo la Utafiti ........................................................................................... 31

3.4 Walengwa wa Utafiti ..... 31
3.5 Usampulishaji ..... 32
3.6 Mbinu za Ukusanyaji Data ..... 33
3.6.1 Uchunguzi Makini ..... 33
3.6.2 Mahojiano (usaili) ..... 33
3.6.3 Dodoso ..... 34
3.6.4 Mapitio ya Nyaraka ..... 34
3.7 Mkabala wa Kimaadili ya Utafiti ..... 35
3.8 Uchanganuzi wa Data ..... 36
3.9 Hitimisho ..... 37
**SURA YA NNE ..... 38**
**4.0 UWASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA DATA ..... 38**
4.1 Utangulizi ..... 38
4.2 Uwasilishaji wa data kuhusu Vyanzo, Michakato na Umuhimu wa Majina ya Mitaa ..... 38
4.2.1 Mtaa wa Shangani ..... 38
4.2.2 Mtaa Wa Forodhani ..... 40
4.2.3 Mtaa wa Darajani ..... 42
4.2.4 Mtaa Wa Sokomuhogo ..... 45
4.2.5 Mtaa wa Hamamni ..... 47
4.2.6 Mtaa wa Funguni ..... 49
4.2.7 Mtaa Wa Mnazi Mmoja ..... 51
4.2.8 Mtaa wa Mkunazini ..... 53
4.2.9 Mtaa Wa Gulioni ..... 54

4.2.10 Mtaa wa Kisiwandui ........ 56
4.2.11 Mtaa wa Mwembetanga ........ 57
4.2.12 Mtaa wa Kisimamajongoo ........ 59
4.2.13 Mtaa wa Mfereji wa Wima ........ 61
4.2.14 Mtaa wa Mfenesi Mazizi ........ 63
4.2.15 Mtaa wa Mikunguni ........ 66
4.2.16 Mtaa wa Kaburi Kikombe ........ 67
4.2.17 Mtaa Wa Mwembebeni ........ 70
4.2.18 Mtaa wa Mwembenjugu ........ 72
4.2.19 Mtaa wa Mwembemadema ........ 74
4.2.20 Mtaa wa Mwembemimba ........ 76
4.2.21 Mtaa wa Shauri Moyo ........ 77
4.2.22 Mtaa wa Mlandege ........ 79
4.2.23 Mtaa wa Kwa Hajitumbo ........ 80
4.2.24 Mtaa wa Kidongochekundu ........ 82
4.2.25 Mtaa wa Mwembeladu ........ 83
4.2.26 Mtaa wa Michenzani ........ 85
4.2.27 Mtaa wa Kibandamaiti ........ 87
4.2.28 Mtaa wa Mitiulaya ........ 89
4.2.29 Mtaa wa Makadara ........ 91
4.2.30 Mtaa wa Mwembeshauri ........ 92
4.3 Vigezo vya Chimbuko la Majina ........ 97
4.3.1 Kigezo cha Kiuchumi ........ 97
4.3.2 Kigezo cha Kijamii ........ 97

4.3.3 Kigezo cha Maumbile ........................................................................ 98

4.3.4 Michakato ya Kiisimu ya Uundaji wa Maneno ya Majina ya Mitaa ............ 99

4.3.5 Muunndo wa Maneno ya Mitaa ................................................................ 101

4.4 Hitimisho ................................................................................................ 104

**SURA YA TANO ......................................................................................... 105**

**5.0 MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........................... 105**

5.1 Utangulizi ................................................................................................ 105

5.2 Muhtasari wa Utafiti ................................................................................ 105

5.3 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti ............................................................. 106

5.4 Hitimisho ................................................................................................ 107

5.5 Mapendekezo ya Utekelezaji ..................................................................... 109

5.6 Tafiti za Baadae ........................................................................................ 110

**MAREJELEO ............................................................................................... 112**

**VIAMBATISHO ........................................................................................... 117**

# JEDWALI

Jedwali 4.1: Uchanganuzi wa Michakato ya Kiisimu ya Uundaji na Muundo wa Maneno .......................................................................... 95

# ORODHA YA VIELELEZO

Kielelezo Na 4.1: Vigezo Vilivyotumika Kuibua Majina ya Mitaa ya Wilaya ya Mjini Unguja ..... 98

Kielelezo Na 4.2: Njia Zilizotumika Kuunda Maneno ya Majina ya Mitaa ya Wilaya ya Mjini Unguja ..... 100

Kielelezo Na 4.3: Miundo ya maneno ya majina ya mitaa ya wilaya ya Mjini Unguja ..... 103

## ORODHA YA PICHA

Picha Na 1.1: Baadhi ya Maeneo ya Wilaya ya Mjini Unguja ................................ 2

Picha Na 4.1: Daraja Lililokua Likiunganisha Kati ya Mji Mkongwe na Ng'ambo........................................................................... 43

Picha Na 4.2: Hamamu Lenyewe ........................................................... 47

Picha Na 4.3: Picha ya Jongoo .............................................................. 61

Picha Na 4.4: Mtaa wa Mfereji wa Wima ............................................... 62

Picha Na 4.5: Mtaa wa Mfenesi Mazizi.................................................. 64

Picha Na 4.6: Mtaa wa Mwembenjugu.................................................... 72

Picha Na 4.7: Picha ya Dema.................................................................. 75

Picha Na 4.8: Ladu Za Ufuta .................................................................. 84

Picha Na 4.9: Mtaa wa Mitiulaya ........................................................... 90

## ORODHA YA RAMANI

Ramani Na 1.1: Visiwa Vya Unguja Na Pemba ........................................................ 1

Ramani Na 4.1: Baadhi ya Mitaa ya Mji Mkongwe na Ng'ambo Miaka ya 1890 ... 40


# SURA YA KWANZA

# 1.0 UTANGULIZI NA USULI WA UTAFITI

## 1.1 Utangulizi

Majina ya mitaa ni miongoni mwa amali muhimu kwa maisha ya kila siku na maendeleo ya binaadamu. Humfanya mtu aweze kutekeleza majukumu na wajibu wake wa kila siku katika nyanja mbali mbali za kiutamaduni, kijamii, kisiasa na kiuchumi. Pia huwa na maana muhimu na maalumu katika lugha zilizotumika katika kuita majina hayo.

Hivyo hivyo, ndio muktadha ya majina ya mitaa katika wilaya ya Mjini Unguja kuchukua nafasi na kujitokeza katika ndimi za wakaazi wa Wilaya ya Mjini na mikoa mbali mbali ya Zanzibar na Tanzania. Upeo na mipaka ya majina hayo yamevuka mipaka na kusikika kutajwa na Wazanzibar wanapokuwa nje ya Tanzania kama vile Omani, Dubai, Uingereza, Marekani na maeneo mengine.




**Ramani Na 1: Visiwa Vya Unguja Na Pemba**

Chanzo: http://www.hartford-hwp.com/archives (imepatikana 22.9.2016)

Hata wageni mbali mbali wanapokuja Zanzibar na kuondoka, huondoka na kumbukumbu nzuri ya majina hayo, huchangia katika kuendeleza na kukuza lugha ya Kiswahili na matumizi yake ndani na nje ya Zanzibar. Ifuatayo ni ramani inayoonesha visiwa vya Unguja na Pemba.

Kwa kuwa Kiswahili asili ya chimbuko lake kimetokana na lahaja iliyokuwa ikitumika maeneo ya Unguja Mjini (lahaja ya Kiunguja Mjini) na utafiti huu unatafiti asili ya majina ya mitaa ya wilaya ya Mjini Unguja, kuna umuhimu mkubwa wa majina ya mitaa hiyo kwani majina hayo ni ya Kiswahili halisi na yana mchango mkubwa katika kukuza lahaja ya Kiunguja Mjini kisha lugha ya Kiswahili ambayo mpaka leo wakaazi wa mitaa hiyo wanaitumia katika shughuli zao za kila siku.



**Picha Na 1.1: Baadhi ya Maeneo ya Wilaya ya Mjini Unguja**

Chanzo: https://encrypted-tbn1.gstatic.com/images?q=tbn:ANd9GcR245yrmM04B7uaq2tt6SkDovZYiWQUvJO3BKeOzGn8of9MKV6Gag (imepatikana 22.9.2016)

Watafiti mbalimbali wametafiti kuhusu majina ya pahala kama vile Juma (2011), Kombo na wenzake (2015), Mwanakheri ( 2014), Drummond (2014), King (2008), Olabiyi (1978), Nieminen (1998), Cornevin (1978), Zubeir (2015) na Lehrer (1992). Picha ifuatayo inaonesha baadhi ya maeneo ya wilaya ya Mjini Unguja.

## 1.2 Usuli wa Tatizo

Majina ya mitaa ni muhimu sana kwa jamii inayoishi pahala husika, ni muhimu kwa mtu binafsi, jamii na hata taifa. Mtu binafsi hujieleza wapi anaishi, jamii hujinasibisha na jina la mitaa inayoishi ili iheshimike na taifa hujipangia maendeleo kulingana na mahitaji au umuhimu wa mitaa hiyo kwa taifa

Kwa mujibu wa Massamba na wenzake (2009) wanaeleza fasili ya isimu jamii kuwa ni taaluma inayoshughulika na uchunguzi unaolenga kufafanua uhusiano uliopo kati ya isimu (lugha) na jamii. Kutokana na fasili hiyo ya isimu jamii, majina ya mitaa yana uhusiano mkubwa sana na isimu jamii kwa sababu isimu jamii inahusu lugha na jamii, hivyo jina la mtaa haliji tu isipokuwa linatokana na jamii, na jamii hiyo ndio inayotoa jina, vilevile jamii hiyo hiyo hutumia lugha katika kuita majina hayo. Mfano jina la Sokomuhogo linatokana na jamii inayoishi hapo na imetumika lugha katika kuliita jina hilo. Kutokana na sababu hiyo ndio tukasema kuwa isimu jamii ina uhusiano na majina ya mitaa.

## 1.3 Kauli ya Tatizo la Utafiti

Tafiti nyingi katika nchi mbalimbali zimechunguza asili ya majina ya mitaa mbali mbali katika maeneo ya Afrika na nje ya Afrika. Tafiti kama hizo ziko kwa kiwango

kidogo sana katika baadhi ya majina ya mitaa hapa Zanzibar. Katika wilaya ya Mjini ambayo inajumuisha mji mkongwe na maeneo ya ng'ambo (angalia picha nambari 1 ukurasa wa 3) wakaazi wake wengi ni vijana ambao umri wao ni kati ya miaka 15 – 40, na wazee wengi huhama na kuhamia maeneo ya vijijini au wengine wametangulia mbele ya haki. Hilo limepelekea kutofahamika asili ya majina ya mitaa ya wilaya ya Mjini Unguja, na kama jitihada za makusudi hazikuchukuliwa tunaweza kupoteza kabisa asili ya majina ya mitaa hiyo. Hilo ndilo tatizo ambalo limefanya kuwepo na umuhimu wa kufanya utafiti huu.

Ukizingatia pia mpaka muda huu hakuna hata utafiti mmoja uliowahi kuchunguza kuhusu michakato ya mbinu zilizotumika katika uundaji wa majina ya mitaa katika wilaya ya Mjini Unguja, mtafiti ameona kuwa kuna haja na umuhimu mkubwa wa kufanya utafiti huu ili kuziba pengo hilo kubwa ambalo linaweza likatoa athari kubwa kwa taifa na vizazi vijavyo na kuathiri lugha yetu ya Kiswahili. Kwa hivyo utafiti huu unakusudia kueleza majina ya mitaa ya wilaya ya Mjini yameanzaje ili wakaazi wa wilaya ya Mjini na wadau wengine mbali mbali wapate hazina hiyo inayoweza kupotea.

## 1.4 Lengo Kuu la Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza michakato na mbinu zilizotumika katika uundaji wa maneno ya majina ya mitaa mbalimbali katika wilaya ya Mjini Unguja.

## 1.5 Malengo Mahsusi

Utafiti huu una malengo mahsusi yafuatayo:

i) Kulezea michakato iliyotumika katika kutoa majina ya mitaa ya wilaya ya Mjini Unguja.

ii) Kubainisha vigezo vilivyotumika kutoa majina ya mitaa ya wilaya ya Mjini Unguja.

iii) Kubainisha umuhimu wa majina ya mitaa ya wilaya ya Mjini Unguja katika kukuza lugha ya Kiswahili.

## 1.6 Maswali ya Utafiti

i) Ni michakato ipi iliyotumika katika kutoa majina ya mitaa ya wilaya ya Mjini Unguja?

ii) Ni vigezo gani vilivyotumika katika kutoa majina ya mitaa ya wilaya ya Mjini Unguja?

iii) Majina ya mitaa ya wilaya ya Mjini Unguja yana umuhimu gani katika kukuza lugha ya Kiswahili?

## 1.7 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu unaohusu michakato na mbinu zilizotumika katika uundaji wa majina ya mitaa katika wilaya ya Mjini Unguja utatoa mchango ufuatao:-

Utawasaidia Waswahili kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili hasa katika upande wa isimu jamii. Vilevile utafiti huu utaitanabahisha serikali na wanajamii kwa ujumla, kuhakikisha kuwa asili ya mitaa na historia zake zinahifadhiwa pamoja na kuimarishwa kwani asili na historia za majina ya mitaa mingi bado hazijahifadhiwa, utawasaidia kutunza kumbukumbu ya majina ya mitaa katika wilaya ya Mjini na iwe

kama kichocheo cha tafiti zaidi kuhusu majina mbali mbali. Pia utawasaidia wasomi ambao watakaotafiti vipengele vinavyoshabihiana na utafiti huu watapata dira na marejeo yatakayowasaidia katika kukamilisha tafiti zao.

## 1.8 Mipaka ya Utafiti

Utafiti unachunguza michakato na mbinu zilizotumika katika uundaji wa majina ya mitaa katika wilaya ya Mjini Unguja. Utafiti huu pia kwa kiasi fulani unaelezea historia ya eneo na hali za kijamii na kiuchumi za watu wa eneo husika na mambo yote ambayo yanapelekea kufafanua asili ya majina ya mitaa hiyo pamoja na vigezo vilivyotumika kutoa majina ya mitaa hiyo, michakato inayotumika katika kutoa majina ya mitaa na kubainisha umuhimu wa majina ya mitaa katika kukuza lugha ya Kiswahili. Utafiti huu haukujishughulisha na majina ya watu, wanyama au vitu ambavyo havikutumika katika kuitwa mitaa, pia haukushughulikia majina ya kigeni ambayo yameitwa katika mitaa ambayo si majina ya lugha ya Kiswahili.

## 1.9 Matatizo ya Utafiti

Katika utafiti huu matatizo mbalimbali yalijitokeza na mtafiti wa utafiti huu alijitahidi kwa kila njia kukabiliana na matatizo hayo. Baadhi ya matatizo hayo ni:-

**Uhaba wa fedha**: Kazi ya utafiti inagharimu fedha nyingi, jambo ambalo mtafiti alikumbana nalo katika utafiti wake, hata hivyo, halikumfanya mtafiti kushindwa kuendelea na kazi yake, alikabiliana nalo kwa kupata msaada wa fedha hizo kutoka kwa ndugu na familia yake ambao walikuwa naye bega kwa bega na kumpa msaada wa hali na mali.

**Mashirikiano hafifu kwa baadhi ya wakaazi:** Baadhi ya wakaazi wingine walikuwa wazito kutoa data za utafiti huu, kwa sababu waliuhusisha utafiti huu na maswala ya siasa na pia kuona mtafiti analipwa kutokana na kazi hii, mtafiti wa utafiti huu aliwaelimisha na kuwafahamisha kwa kina malengo ya utafiti huu jambo ambalo lilimsaidia mtafiti kupata data na wakaazi walitoa mashirikiano mazuri baadae.

**Uchache wa muda:** Utafiti unahitaji muda wa kutosha ili kuukamilisha, na ukizingatia kuwa mtafiti ni mama mwenye familia na ana majukumu ya kuishughulikia familia yake, hivyo, ilimlazimu kutumia muda mkubwa zaidi kuhakikisha anafikia lengo lake la utafiti.

### 1.10 Hitimisho

Katika sura hii ya mwanzo mtafiti amezungumzia utangulizi wa mada, usuli wa tatizo, kauli ya tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti pamoja na matatizo ya utafiti. Sura inayofuata inahusu mapitio ya kazi tangulizi na kiunzi cha nadharia.

# SURA YA PILI

# 2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Sehemu hii inaelezea dhana mbali mbali kuhusu mada ya majina ya maeneo ya maskani na tafiti tangulizi. Mada zinazojadiliwa ni pamoja na dhana ya utoaji wa majina ya makaazi ya watu, vigezo vinavyotumika katika kutoa majina ya makaazi ya kuishi watu (maskani) na namna majina hayo yanavyotolewa. Vile vile inaelezea michakato inayohusu utoaji wa majina ya makaazi ya watu na umuhimu wa majina ya makaazi ya watu unavyohusiana na ukuzaji wa lugha kwa jumla.

## 2.2 Jamii na Makaazi

Jamii ni jumla ya watu wanaoishi mahali pamoja ambao huunda makundi tofauti ya watu kwa misingi ya kiuchumi, itikadi, utaalamu, eneo wanaloishi, kazi wanayofanya n.k. Kwa mujibu wa Mdee (2012), sifa mojawapo ya jamii ya watu ni kuwa wanaishi pamoja katika maeneo mbalimbali yanayotambulika kwa majina. Watu wanapoishi pamoja huwa wanawasiliana kwa kutumia lugha ambayo ndio inayoonesha utambulisho wa watu hao. Makaazi ni eneo, maskani au mazingira ambayo ni makao ya viumbe hai. Makaazi ya binaadamu ni mazingira ambayo binaadamu huishi na kuingiliana (TUKI, 2014).

## 2.3 Dhana ya Utambulisho

Mdee (keshatajwa) anaeleza maana ya utambulisho kuwa ni sifa au vibainishi vinavyotumiwa kutambulisha kundi la watu, jamii, taifa au mtu ili kuonesha tofauti

yake na makundi, mataifa au watu wengine. Pia Mdee (2012) amesema lugha inatumika katika utambulisho mbali mbali kama inavyoelezwa hapa chini;

### 2.3.1 Utambulisho wa Kiisimu

Ni utambulisho unaohusu lugha ya mzungumzaji kama vile kutumia lahaja, mkazo, kiimbo, matamshi ya sauti, maneno na hata miundo ya lugha. Mambo hayo humwezesha mzungumzaji wa lugha kubaini utambulisho wa mshiriki wa mazungumzo yake kuwa anatoka mahali fulani, mkoa au jimbo fulani au anatoka nchi fulani (Msanjila, 2011). Utambulisho huu hujidhihirisha katika aina mbalimbali za tanzu za isimu, yaani kifonolojia, kileksika na kisintaksia kama inavyofafanuliwa katika vipengele vifuatavyo:-

#### 2.3.1.1 Utambulisho wa Kifonolojia

TUKI (2014), inaeleza maana ya fonolojia kuwa ni tawi la isimu linaloshughulikia uchunguzi, uchambuzi na uainishaji mfumo wa sauti pambanuzi katika lugha mahsusi. Utambulisho huu unaweza kupatikana katika majina ya watu, vitu, na hata mitaa. Kwa mfano neno penya, linaweza kumtambulisha mtu anakotoka kutokana na anavyolitamka.Unguja mjini hulitamka penya, Makunduchi hulitamka venya, neno pika, Unguja mjini hulitamka pika, Makunduchi hulitamka vika, Hivyo sauti {pi} na {vi} zinamtambulisha mtu huyo anatoka wapi.

#### 2.3.1.2 Utambulisho wa Kileksika

Kwa mujibu wa TUKI (2014) neno leksika lina maana ya sehemu ya sarufi iliyo na taarifa zote za maneno. Hivyo neno linaweza kumtambulisha mtu sehemu anayotoka

kutokana na neno kutumia neno tofauti lenye maana moja. Kwa mfano: neno *wali* (Unguja mjini), *ubwabwa* (Tumbatu), neno *mende* (Unguja mjini) *pepe* (Tumbatu).

#### 2.3.1.3 Utambulisho wa Kisintaksia

Utambulisho wa kisintaksia unaelezea muundo na uchanganuzi wa taratibu na kanuni za uhusiano baina ya maneno katika tungo (TUKI, 2014). Kisintaksia tunaangalia namna sentensi/tungo zinavyoweza kumtambulisha mtu sehemu anayotoka.Kwa mfano.

*Mtoto yule ni mgomvi* (Unguja mjini)
*Mwanakele uyoko mziwi* (Makunduchi*).*
*Mwana yulya mgovi* (Kitumbatu*).*

### 2.3.2 Utambulisho wa Kijamii:

Utambulisho wa kijamii ni ule upekee wa jamii unaobainishwa kwa misingi ya kitamaduni ambayo iko tofauti na misingi ya tamaduni za jamii nyingine (Msanjila, 2011). Aina hii ya utambulisho kwa mujibu wa Msanjila (ameshatajwa) huhusisha majina mbalimbali; kama vile majina ya familia, majina ya matukio na majina ya vitu na mahali, kama inavyoelezwa hapo chini.

#### 2.3.2.1 Majina ya Familia

Ni majina ya jamii fulani ambayo yanatokana na utamaduni wa jamii husika na ambayo hueleweka na jamii hiyo. Mfano Ramadhani, Rajab, Shaabani na Muharam ni majina ambayo hutumia baadhi ya familia za watu wa Zanzibar wenye imani ya dini ya kiislamu kama ni viashiria vya miezi mitukufu katika tamaduni zao. Baadhi ya majina ya mitaa hutokana na majina ya familia aghalabu zile zilizokuwa muhimu katika jamii husika.

#### 2.3.2.2 Majina ya Matukio

Majina ya matukio ni majina ambayo chanzo chake ni masimulizi yanayosimuliwa kutoka kizazi hadi kizazi. Mfano mwaka kogwa ni jina la tukio linaloambatanisha mambo mbali mbali yanayofanywa na jamii ya Wamakunduchi kama vile kuomba kwenye mizimu, kupigana bakora, kuchinja wanyama, kuchoma moto kibanda n.k. Baadhi ya mitaa hupewa majina yao kutokana na matukio mbalimbali yaliyotokea mara kwa mara katika maeneo husika.

#### 2.3.2.3 Majina ya Mahala na Vitu

Majina ya mahali ni sehemu ya urithi wa jamii ambao huendelea na kubadilishana kati ya vizazi mbalimbali ndani ya jamii moja na huwa majina hayo yanaheshimiwa kwa urithi wake uliokuwemo wa kihistoria, kilugha na kijamii (NSW Heritage Office, 2004). Moja ya sehemu ya isimu ni utambulisho wa majina ya mahala na vitu.

## 2.4 Dhana ya Majina na Aina zake

Wataalamu mbali mbali wameelezea dhana ya majina na aina zake. Miongoni mwao ni Masebo na Nyangwine (2004), ambao wamesema kuwa majina ni maneno yanayotaja vitu, hali au matendo ili kuviainisha na kuvitofautisha na vitu vingine. Pia wametaja aina za majina kuwa ni majina ya kawaida, majina ya pekee, majina ya jamii, majina ya dhahania na majina ya wingi.

Kwa upande mwingine Khamis (2011), ameeleza kwamba jina ni aina ya neno linalotaja au linalobainisha viumbe hai, vitu visivyo hai, mwahali, hisi, hali, maarifa,

jambo au tukio katika tungo au sentensi. Vile vile ametaja aina za majina kama vile majina ya pekee, majina maarufu, majina umbo, majina ya dhahania, majina ya hali, majina ya maarifa, majina ya jambo au tukio, majina ya jamii, majina ya umoja, majina ya wingi, majina yanayohesabika, majina yasiyohesabika na majina ambatano.

Massamba na wenzake (2003), nao wameeleza kwamba jina ni neno linalotaja kitu, kiumbe, hali, dhana au tendo lolote liwalo. Nao wamezitaja aina za majina kwa kuzigawa katika makundi makuu matatu kama vile majina jumuishi, majina mahsusi na majina kikundi.

Nae Wahiga (1999), ametoa mchango mkubwa katika kutaja aina za majina kupitia nomino, na kuzigawa katika aina tofauti za majina kama vile majina ya pekee, kama Asha, Tanga, Amina nk, majina ya kawaida, kama vile kuku, kalamu, ugonjwa, njaa nk, majina ya dhahania, kama vile ukarimu, afya, malaika, ukulima nk, majina ya jamii kama vile bunge, chama, kamati nk, hata majina ya wingi kama vile maji, mafuta, maziwa nk, lakini hakutaja majina ya pahala.

Kama tulivyoona Wahiga ametafiti kuhusu aina za majina kama majina ya pekee kama vile Mungu, majina ya kawaida kama vile meza, majina ya dhahania kama vile njaa, na majina ya jamii kama vile bunge. Yeye amekwenda sana kwenye nyanja hizo wakati mtafiti wa utafiti huu amefaidika sana na maelezo ya Wahiga katika majina ya jamii na ya pekee kwani mada hiyo ya Wahiga ina uhusiano na mada hii ya mtafiti.

Vilevile, Khamis (2003) ametaja majina na aina zake zikiwemo “Majina ya kawaida au maarufu, majina umbo, majina hisi, majina jamii, majina ya umoja pamoja na mifano mbali mbali.” Ufafanuzi wa Khamis umejikita zaidi kuelezea majina umbo kama vile duara , majina hisi kama vile njaa, majina ya kawaida kama vile kalamu, majina jamii kama vile kamati na majina ya umoja kama vile chupapppp . Yeye hakutofautiana sana na Wahiga katika baadhi ya majina kama vile ya kawaida na ya jamii, utafiti wake pia una mahusiano na mtafiti wa mada hii katika kipengele cha majina ya jamii.

## 2.5 Mchakato wa Utoaji wa Majina

Wataalamu mbalimbali wameeleza dhana ya mchakato wa utoaji wa majina, miongoni mwao ni hawa wafuatao:

Guma (2011) akimuunga mkono Funk (1997) kama alivyonukuliwa na Joho(2011) anafafanua kuwa mchakato mzima wa utoaji wa majina ni tukio la kijamii na kiutamaduni lenye kuonesha historia.

Tukizingatia maelezo ya Guma (ameshatajwa) amejaribu kueleza kwamba majina ni tukio la kijamii na kiutamaduni linalotokea katika sehemu fulani ambalo limehusishwa na jamii husika. Mtafiti wa utafiti huu ataweza kupata mifano ya matukio ya kijamii na kiutamaduni iliyopatikana katika maeneo na kuwezeshwa kuitwa jina la pahala na hiyo itampa mwanga katika utafiti wa eneo lake zaidi. Funk (1997) akinukuliwa na Joho (2011), anaeleza kuwa “utoaji wa jina ni tendo kama tendo jengine lolote na limo katika muktadha. Pia masuala ya jamii moja na

huyapambanua au huyatofautisha na jamii nyengine hivyo utoaji wa majina ya mitaa huweza kutafautisha baina ya mtaa mmoja na mwengine" (uk 43).

Maelezo ya Funk (ameshatajwa) yatamsaidia mtafiti kuelewa kuwa maana ya jina la mtaa mmoja na mwingine ni tofauti, kwa sababu kila jina la mtaa huitwa kutokana na sababu maalumu, kwa hivyo kila mtaa utakuwa na maana tofauti na mwingine. Kwa mfano Shaurimoyo maana  yake ni tofauti na Mikunguni.

Jenks (1912), ametaja njia mbalimbali zinazotimika katika kuita majina ya mitaa. Baadhi ya njia hizo ni;

i. Ufupisho mfano, Mwanakwerekwe likawa Kwerekwe, Mwembekisonge likawa Kisonge.
ii. Kuchanganya maneno mfano *Mwembe* na *Madema* likawa *Mwembemadema*.
iii. Kukutanisha kwa kuondoa herufi fulani ili kurahisisha kulitamka, mfano; *Tchad* likawa *Chad*.
iv. Kubadilika na kukua kwa lugha na kupoteza maana halisi ya jina la mtaa: mfano, *Mzambarauni* likawa *Barastekipande, Kibokoni* likawa *Kidutani*.
v. Kutumika lugha mpya kwenye eneo husika na ikachukua nafasi ya lugha ya mwanzo, hapo majina ya mitaa yanaweza kukosa maana yake sahihi. Mfano: *Mwemberikunda* likawa *Alabama*.
vi. Kuelezea jina la pahala ili kutofautisha pahala husika, maneno kama vile chini, juu, kubwa, ndogo hutumika ili kutafautisha jina la pahala husika: mfano, *Kikwajuni juu, Kikwajuni chini, Mchangani mjini, Mchangani shamba* nk.

vii. Kuboresha jina la pahala, mfano: *Nyikunduchi* kuwa *Makunduchi.*

## 2.6 Vigezo Vilivyotumika kutoa Majina ya Mitaa

Utoaji wa majina ya mitaa sehemu mbalimbali ulimwenguni hutumia vigezo maalumu, wataalamu mbalimbali wametaja vigezo tofauti vinavyotumika kutoa majina ya maeneo. Miongoni mwa vigezo hivyo ni;

### 2.6.1 Vigezo vya Maumbile

Baadhi ya mitaa hupata majina yake kwa kuwepo maumbile mbalimbali kama vile daraja, barabara, milima, mito, miti na mengineyo (Langford, 2013). Neno maumbile maana moja wapo ni vitu mbalimbali asilia au vilivyotengenezwa na binaadamu ambavyo vipo kwenye sehemu, mkoa, nchi au bara fulani, vitu hivyo kuwepo kwake kumesababishwa na mambo mbalimbali na vitu hivyo huwa na athari mbalimbali kwa mazingira asilia na mazingira ya watu (Abshir 2016).

### 2.6.2 Vigezo vya Kijamii

Kuna baadhi ya mitaa mengine hupata majina yake kutokana na harakati za kijamii mbalimbali zinazofanyika katika maeneo hayo kama vile michezo, matibabu, elimu, harusi, maziko, burudani na shughuli nyingine za kijamii (Helleland na wenzake 2012), (Helleland, 2002).

### 2.6.3 Vigezo vya Kiuchumi

Mitaa mingine hupata majina yake kutokana na harakati za kiuchumi kama vile biashara, uvuvi nk. (Helleland na wenzake, 2012), (Helleland, 2002).

Mlacha (1995) anaeleza kuwa kuna vigezo vya utoaji wa majina ya mitaa kuwa ni vya kisiasa au vya kijamii.

## 2.7 Kazi Tangulizi Zinazohusu Dhana ya Majina ya Maeneo

Wataalamu mbali mbali wametoa mchango wao katika kuelezea dhana ya majina ya mitaa, miongoni mwa wataalamu hao ni Eskeland (2001) anafasili kwamba majina ya pahala ni sehemu muhimu sana ya lugha ya kila siku na ni kitambulisho cha mtu mmoja mmoja na jamii kijumla. Naye Hulden (1994) anafafanua kuwa majina ya pahala ni kiashirio cha mshikamano wa kijamii, kila majina ya pahala yanapotumika zaidi ndio huzidisha mshikamano kwenye jamii husika. Vilevile Saporar (2003) anaeleza kwamba majina ya pahala ni muhimu sana na ni kitambulisho cha taifa. Helleland (2012) anasema kuwa hisia na akili za jamii hupenda jina libakie lisibadilishwe na endapo likibadilishwa au kutamkwa vibaya basi jamii hukasirika na kulaumu hali hiyo na huonesha ishara za kutoridhishwa Vilevile, anasema kwamba jina la pahala ikiwa linaleta hisia chanya basi mtumiaji atakuwa na furaha kwa mfano jina la *Forodhani*, na ikiwa jina la pahala linaleta hisia hasi basi mtumiaji atakuwa na huzuni na ataliepuka kwa mfano jina la *Shaurimoyo*.

NSW Heritage Office (2004), wanaeleza kwamba majina ya pahala ni sehemu ya urithi wa jamii ambao huendelea na kubadilishana kati ya vizazi mbalimbali ndani ya jamii moja na huwa majina hayo yanaheshimiwa kwa urithi wake wa kihistoria, kilugha na kijamii.Vilevile, wanafafanua kwamba jina la pahala ni jina lolote linalopewa pahala fulani ili kuweza kumiliki pahala hapo utambulisho maalumu ambao una sifa maalumu zinazotofautisha pahala hapo na mahala mwingine. Wetas

(2000) anatufahamisha kuwa jina la mji mkuu wa *Norway "Kristiania*" lilipobadilishwa la kutumika jina la "Oslo" palitokea mzozo kwenye jamii. Zilliacus (1978) anaeleza kuwa majina ya pahala ni sehemu muhimu ya mazingira yetu ya Kijiografia na ya kiutamaduni, yanatambulisha vitu vya aina mbalimbali na huleta hisia za umiliki, kujinasibisha na utambulisho kwa jamii.

Helleland (2012) anatilia mkazo kueleza kwamba baadhi ya majina ya mitaa hujulikana na watu kidogo kijiji tu na baadhi hujulikana na watu wengi hadi mjini au nje ya nchi. Jenks (1912), anaeleza kwamba nchi ambazo yametokea mabadiliko makubwa ya lugha na utamaduni kama vile *England* na *France* majina hubadilika haraka na mapya hutumika. Nchi ambazo hazina mabadiliko makubwa ya lugha na utamaduni majina ya pahala hubakia vilevile mfano *Wales.* Arthur (1998) anaeleza kuwa majina ya vijiji na miji mara nyingi hurejelea watu maalum, jamii na shughuli za kiutawala, mandhari, ndege na wanyama, mazao na mboga mboga. Pia ameeleza majina mengi ya Marekani yamehamishwa kutoka Britain. Mengine yana asili ya Ufaransa kama vile *Detroit, Michigan* na mengine yamechukuliwa kutoka lugha za wenyeji. Majina maalum (watu au wanyama) na maeneo ya jumla au misemo imetumika.

Kwa mujibu wa Arthur (ameshatajwa), majina mengi mapya ya Kifaransa yameeleza milima na mengine yanatokana na Kiingereza kama *Richmond, Grosmont*. Pia anasema akizungumzia majina ya makaazi majina huwa yanaelezea kazi ya pahala kama soko, ngome, shamba au umbile asilia. Ikiwa moja ya hivi vipo, hurekebishwa kuwa jina la mtu au sifa. Jina la pahala linaweza kutokana na umbile asilia

lililokuwepo katika mtaa huo. Mfano *Blackstream* lenye maana ya chemchem nyeusi ni jina la mtaa uliopo Uingereza. Vile vile jina la pahala linaweza likatokana na jina la mtu na umbile asilia. Mfano *Beorn's clearing* ni jina la mtaa uliopo Uingereza linatokana na jina la mtu aitwaye Beorn ambaye alipata kuishi katika eneo hilo. Pia jina la pahala linaweza likatokana na jina la mtu, na shughuli ifanyikayo kwa mfano *Grimr's farm* shamba la Grimr ni mtaa uliopo Uingereza. Ameeleza tena kuwa jina la pahala linaweza likatokana na jina la mtu, kazi na umbile asilia. Mfano *Totta's boundary valley* ni mtaa uliopo Uingereza. Majina ya mitaa yenye mfano kama huo yanapatikana katika nchi nyengine na miji mengine. Mfano *Amsterdam* (River Amstel dam) lenye maana ya demu ya mto Amstel, *Tashkent* (stone city) yaani jiji la mawe, *Copenhagen* (Merchants' harbor) lenye maana ya bandari ya wafanyabiashara, *Paris* (Home of the Paris) yaani nyumba ya Paris, *Shanghai* (Seaport) yaani bandari yenye bahari. Arthur (ameshatajwa) naye kama alivyoeleza kuwa majina ya miji humaanisha watu, mandhari, viumbe hai, maumbile, majina mengine hutokana na lugha mbali mbali na mengine huelezea kazi ya pahala. Utafiti huu utasaidia kuijua mitaa mbali mbali ambayo majina yake ni ya watu, majina yanayotokana na mandhari ya pahala, majina ya viumbe hai kama ndege, wadudu n.k, majina ambayo chanzo chake ni maumbile asilia kama vilima, mabonde nk, na majina ambayo yanatokana na kazi ya pahala yaani ile kazi inayofanywa eneo hilo ikawa ndio jina la pahala hapo kama vile soko, shamba nk, na hata majina ambayo yanatokana na lugha nyingine ambayo asili yake si ya Kiswahili.

Lehrer (1992) anafafanua zaidi hoja na kueleza kuwa majina ya mitaa mara nyingi hutokana na majina ya watu mashuhuri, maumbile asilia, miti na nambari. Vilevile

anaeleza kwamba majina ya mitaa yanakwenda sambamba na maana halisi ya majina yenyewe. Makame (2001) ameeleza kuwa jina la Zanzibar linatumiwa kutaja visiwa viwili ndugu ambavyo ni Unguja na Pemba. Unguja ambacho ni kikubwa na Pemba ambacho ni kidogo vikiwa vimezungukwa na zaidi ya visiwa vidogo 50. Pia ameeleza kuwa Zanzibar hupata misimu (majira) minne kwa mwaka, hata hivyo Zanzibar imekusanya mambo mbali mbali kutoka katika tamaduni za bahari ya Hindi na kupata utamaduni wa Waswahili. Kama tunavyojua kuwa wilaya ya Mjini Unguja ni sehemu ya Zanzibar, mtafiti wa utafiti huu atachangia kutafiti baadhi ya hiyo mitaa ya Zanzibar na hasa katika eneo la wilaya ya Mjini Unguja.

Pandu (2014) katika utafiti wake wa majina ya shule za Unguja mjini katika kutunza historia ya Zanzibar. Alieleza historia ya Zanzibar kuwa "Asili ya neno Zanzibar ni Ajemi au waarabu. Waajemi wamelitoa jina hili kutoka katika neno "Zenji – bar" lenye maana ya "Negro coast" yaani pwani ya watu weusi. Waarabu wamelitoa jina hili kutokana na neno **"*Zayns – al – bar*"** lenye maana ya "Nchi ya usawa au neema ya nchi hiyo".Mtafiti wa utafiti huu atafaidika kujua asili ya majina ya mitaa mbalimbali katika wilaya ya Mjini Unguja ambayo ipo katika kisiwa hicho cha Zanzibar. Njozi (2010), ameeleza wakati wa vita vya Abushiri na Wajerumani huko Kilwa, wazalendo walipigana kufa na kupona na Wajerumani, kutokana na udhaifu wa wazalendo hao Wajerumani waliwanyonga wazalendo katika mwembe, akiwemo kiongozi wa wazalendo Al-ustadhi Omar Makunganya. Hivyo, sehemu iliyotumika kutekeleza unyongaji huo pakaitwa jina la Mwembe kunyonga. Kutokana na utafiti huo mtafiti wa utafiti huu atapata mwanga wa kuelewa mahusiano ya jina la mtaa na jamii husika kama alivyoona uhusiano uliopo kati ya jina hili na jamii ya Wahehe

wa Kilwa. Kadmon (2000) ni miongoni mwa wataalamu anaejishughulisha na taaluma ya majina ya pahala, alijadili kuhusu majina ya mwahala mbalimbali huko Uingereza, alichunguza pia na uundwaji wa majina ya pahala katika lugha zote bila ya kuwa na lugha mahsusi. Uchambuzi huu umemsaidia mtafiti wa utafiti huu kufahamu mengi kuhusu majina ya pahala.

Maandiko yote haya yana mchango mkubwa katika kumwezesha mtafiti wa utafiti huu kufahamu aina za majina na vipengele vyake, kazi zake, faida zake na pia kuelewa kwa kina mahusiano na isimu jamii na majina ya pahala, kwani baadhi ya majina hayo hayo yaliyotajwa na baadhi ya wataalamu ndio yanayotumika kuitwa mahala na mitaa mbali mbali likiwemo eneo analofanya utafiti mtafiti. Kwa hivyo yamechangia kuupa muendelezo na mwanga utafiti huu.

Kutokana na hali hiyo imepelekea mtafiti kuona kwamba kuna haja na umuhimu mkubwa kufanya utafiti wake katika kujua michakato na mbinu zilizotumika katika uundaji wa majina ya mitaa katika wilaya ya Mjini Unguja.

## 2.8 Tafiti Tangulizi Zinazohusu Majina ya Mahala

Kuna tafiti mbalimbali ambazo zimefanywa kuhusu majina ya mitaa katika maeneo mbalimbali, miongoni mwa tafiti hizo ni ule uliofanywa na Juma (2011), ambaye alielezea asili ya majina ya Bwejuu, Mtende, Makunduchi na Kizimkazi kwa kusema kuwa " Katika utafiti huo mtafiti alibainisha kuwa kuibuka kwa jina la Makunduchi inasemekana kulitokana na kuwepo kundi moja la watu lililokuwa huko Kae Pwani, Unguja Ukuu, baadhi yao waliondoka na kuelekea kusini Mashariki ya hiki Kisiwa

na kupitia sehemu mbali mbali hatimae wakafikia hii sehemu yenye udongo mwekundu. Hapo kundi hili lilisita kwanza na kuanza shughuli za kilimo. Baada ya muda fulani kulikuwa na wengine waliorudi kule Kae Pwani na walipokuwa wakiulizwa na wenzao hujibu, "*Tuwa uko nyikundu chi*" yaani wanaishi ardhi ambayo ardhi yake ni nyekundu. Kwa kuwa hawakuweza kulipata jina hasa la mahali penyewe, hivyo tamko nyikunduchi liliwakalia wepesi zaidi. Basi katika kulikariri neno hili mara kwa mara wenyeji walifanya nyongeza ya herufi kidogo kidogo na ndimi nyengine zikaanza kubainisha tamko Makunduchi na kubakia hivyo hivyo.

Mtafiti huyu alielezea pia asili ya watu wa Mtende, akifafanua chanzo cha jina la Mtende Juma (ameshatajwa) alieleza kuwa "Asili ya jina la Mtende linatokana na Mzee mmoja aliyeishi Kizimkazi aliitwa Mzee Kizi alikuwa hodari wa kazi. Kwa hivyo alikwenda kijijini kwa matembezi pamoja na "wenyeji wake kutoka Kizimkazi, wenyeji wake wakamtania kwa kumwambia "kizi mkazi" yaani Kizi ni mchapa kazi ...... nae kizi akawajibu "Isiwe Kizi tu ndie mtenda kazi bali nanyi Mtende" akimaanisha kuwa na wao wafanye kazi kwa hivyo kijiji hicho kikaitwa Mtende. Katika utafiti huo Juma (ameshatajwa) alielezea pia kuhusu asili ya jina la Bwejuu limetokana na hapo kale walikuja watu watatu kutoka Unguja Ukuu. Walifika sehemu moja ambayo imeinuka kidogo na ambayo ilikuwa na mawe mengi, baadae kidogo wakateremka chini ili wajue wamefika wapi? Kwa bahati mbaya mwenzao mmoja akafa wakamzika wakatafuta jiwe wakaliweka juu yake kama alama yao .Waliporudi Unguja Ukuu wakaulizwa mbona hamkutimia nao wakajibu mwenzetu kafa lakini tumemzika kisha tukaweka jibwe juu" kwa hiyo eneo hili likaitwa Bwejuu.

Vilevile Kombo na wenzake (2015) wametafiti kuhusu asili na historia ya majina ya mitaa ya Fukuchani iliyopo mkoa wa Kaskazini Unguja. Watafiti hawa wamepata kujua asili na historia ya majina ya mitaa ya Fukuchani, majina hayo yalianza lini na vitu gani vilivyopelekea mitaa hiyo kuitwa majina hayo. Mtafiti wa utafiti huu atafaidika naye kujua michakato na mbinu zilizotumika katika uundaji wa majina ya mitaa katika wilaya ya Mjini Unguja, yameanza lini, na mambo gani yamepelekea kupewa mitaa hiyo majina hayo. Masoud (2014), katika utafiti wake kuhusiana na mchango wa majina ya vijiji vya Donge katika kuhifadhi historia ya Unguja ameeleza historia ya vijiji vya Donge kama vile Kipange, Mbiji, Michenzani, Chechele, Pangamaua, Mwembe mapapai nk, katika utafiti wake huu amesema "Asili ya kijiji hicho wakaazi wake hujishughulisha na shughuli za kilimo na kila walichokipanda kilikuwa kinatoa mazao mengi kutokana na sababu hiyo wakasema "Hili sio Dongo bali ni Donge tena la dhahabu" huu ukawa mwanzo wa eneo hilo kuitwa Donge.

Naye Zubeir (2015), katika utafiti wake unaohusu etimolojia ya majina ya mahali ya kaskazini Pemba kuwa utambulisho wa utamaduni wa Wapemba amegundua kuwa majina ya mahali yana mfungamano na jamii na utamaduni wa jamii husika. Pia baadhi ya majina yanaakisi moja kwa moja shughuli wanazofanya wanajamii. Vile vile, alibaini kuwa baadhi ya majina huwa ni ya hali ya kimazingira ya maeneo hayo kama jiografia inavyoonekana. Hata hivyo, kuna baadhi ya majina ya mahali hutokana na watu maarufu au matendo ya kihistoria yaliyofanywa na wakaazi wa zamani wa maeneo hayo. Mwanakheri (2014), katika utafiti wake unaohusu uchanganuzi wa kiisimu jamii wa mifumo ya utoaji wa majina ya mitaa katika mkoa

wa Kusini Unguja amegundua kuwa yana maana mahususi na yenye uhusiano na jamii ya mkoa huo katika mifumo ya utoaji wa majina.

Utafiti mwingine kuhusu asili ya majina ya mahali ni ule uliofanywa na Drummond (2014), katika utafiti wake alibainisha kuwa majina ya pahala huzaliwa wakati lugha zinapokutana kimandhari, mara nyingi majina ya pahala hurejelea mandhari, maumbile asilia au yalotengenezwa na binadamu, majina huwepo hata kama maumbile yapotee. Katika utafiti wake alibainisha kuwa miongoni mwa majina ya milima katika makaazi yalitokana na majina ya watu. Mfano *Hornshill* yaani mlima wenye pembe, pia huhusiana na majengo au ukweli wa kihistoria. Mfano *Castehill* lenye maana ya kasri ya mfalme. Sehemu nyengine huhusiana na mimea au wanyama Mfano *Berryhill* na sehemu nyengine ni muonekano wa mandhari ya milima Mfano *Whitehill* yaani mlima mweupe. Mtafiti wa utafiti huu nae amepata kujua majina ambayo yameitwa kutokana na maumbile yaliyotengenezwa na binaadamu kama vile madaraja, barabara nk. Naye King (2008), katika utafiti wake unaohusu majina ya pahala huko Uskochi, amegundua kuwa majina ya pahala yameitwa kutokana na kigezo cha maumbile ambacho kinakuwepo, majina ya mahala humo huendelea kuwepo kwa muda mrefu kwa vizazi vingine. Mfano, Kilimani, Migombani nk. Pia King (ameshatajwa) anaeleza kuwa kuna uhusiano mkubwa kati ya mito na majina yanayotumika kwa mito hiyo kwani majina hayo yanaakisi pahala husika. Mfano *Mto wa mbu*, *Mto pepo* nk.

Kwa upande wake Nieminen (1998), katika utafiti wake aligundua kuwa wakaazi asilia wa Quebec wa asili wanayaenzi majina ya mitaa yao kama ni sehemu muhimu

ya matukio mbalimbali ya kimazingira, kihistoria na kiutamaduni. Alihitimisha uchunguzi wake kwa kusema kuwa jamii na siasa zinahusika sana katika kuitwa majina ya pahala ya Quebec. Pia Nieminen (ameshatajwa) anaeleza pia mara nyingi mvutano hutokea kati ya majina ya pahala yaliyotumika na watu wa asili na majina mapya yaliyowekwa na serikali, kinachojitokeza ni kutumika yote mawili kwa wahusika tofauti, jamii hutumia yao na serikali hutumia yao kwa pahala pale pale. Mfano, *Kibandamaiti* kuitwa *Uwanja wa demokrasia.* Utafiti mwingine ni ule uliofanywa na El fas (1978), matokeo ya utafiti wake yalionesha kuwa majina mengi ya pahala ya nchi za Afrika yametokana na lugha zinazotumika maeneo husika .

Vilevile ameeleza majina ya pahala ya baadhi ya maeneo ya Afrika yamebadilika yanavyoandikwa na kutamkwa. Mfano, Acila sasa linaitwa *Arzila*, *Fas* (*Morocco*) sasa linaitwa *Fez*, *Nyikunduchi* sasa *Makunduchi*. Yai (1978), ameeleza katika utafiti wake unaohusu majina ya pahala amegundua kuwa majina ya pahala ya Afrika yanatumia majina ya lugha za Afrika sio za kigeni. Kila taifa liitwe kwa jina wanalolikubali na waliloliweka wenyewe sio vyenginevyo. Naye Cornevin (1978) katika utafiti wake wa majina ya mitaa amegundua kuwa wazungu wanayatamka na kuyaandika majina ya pahala ya Afrika tofauti na wanavyoyaandika na kuyatamka wao wenyewe.

Tafiti za watafiti waliotajwa hapo juu zimeashiria upeo mkubwa ambao wameuonesha katika tafiti zao za majina ya mitaa, na pia zimetoa umuhimu ambao umeamsha ari ya kuendelea kufanya tafiti zaidi katika sehemu ambazo bado majina ya mitaa hayajachunguzwa ipasavyo**.**

## 2.9 Umuhimu wa Majina ya Mitaa

Wataalamu Langford (2013) na Lehrer (1992), wameelezea kuwa majina ya mitaa yana umuhimu mbalimbali, miongoni mwa umuhimu huo ni kama ifuatavyo; kwanza majina ya mitaa huashiria kuwa maumbile asilia au harakati za kijamii au harakati za kisiasa zilizopelekea kuitwa majina husika ambazo zilikuwa ni vitu muhimu sana kwa wakaazi wa eneo hilo na vimeathiri sana maisha yao na wanavithamini vitu hivyo. Pia wamefafanua kwamba majina hayo ya mitaa yanahifadhi vitamkwa, misamiati, na lugha inayotumiwa maeneo hayo isipotee na kuzidi kudumaa bali iwe inatumiwa kila siku katika shughuli mbalimbali kupitia matumizi ya majina ya mitaa husika. Vilevile Odelle (2012), alibainisha umuhimu wa majina ya mitaa kwa kusema kwamba majina ya mitaa yanajenga utambulisho mzuri wa mtaa, wilaya, mji na hata wa nchi kwa kutoa taswira halisi ambayo anayesikia majina ya mitaa hiyo humpa picha na utambulisho unaojitosheleza unaobeba dhana kamili wa jina hilo na vilevile huwakutanisha wataalamu mbalimbali wa isimu, fasihi, saikolojia, sosholojia, historia na jiografia kwa kukaa pamoja katika kufanya utafiti wa majina ya mitaa hiyo na kuyachambua kwa kuangalia sehemu mbalimbali za utafiti kwenye majina husika.

Umuhimu mwingine wa majina ya pahala ni ule aliouelezea Helleland (2002) kuwa majina ya pahala hutoa maelezo muhimu ya historia ya eneo husika, athari za utamaduni, kijamii na kisiasa zilizojitokeza kwenye maeneo ya majina hayo. Majina ya pahala yana nafasi kubwa katika mfumo wa mawasiliano ya pahala na ni kifaa muhimu cha kiisimu ambacho watu hukitumia mara nyingi kila siku. Kuna majina ya mitaa ambayo mengine ni maarufu katika kiwango cha kijiji, wilaya, mkoa, taifa na

hata mengine kimataifa. Wataalamu wingine Lehrer (1992) na Zubeir (2015) wakielezea zaidi kuhusu maana inayopatikana katika majina ya mitaa walifafanua kuwa dhana ya kitu chenyewe kilichohusiana na majina husika ya mitaa. Walibainisha zaidi kuwa majina ya mitaa hutambulisha utamaduni wa wanajamii kwa kujua asili na maana zilizomo ndani ya majina. Majapela (2009), alibainisha namna majina ya mahali yanavyonyambulishwa kuunda majina ya watu wanaoishi katika eneo linalohusika, na kubainisha viambishi ngeli vinavyojitokeza katika majina ya mahali.

Naye Abeid (2005), amesema kuwa kila tukio huacha athari sehemu hiyo na kuifanya kuwa na historia. Hivyo kila mtaa una utamaduni kwa jamii ya pale.Akielezea asili ya jina la Jang’ombe alifafanua kuwa asili ya jina hilo ni kutokana na tabia za wakaazi wa asilia wa eneo hilo ambao zilikuwa sawa na wanyama kama ng’ombe. Katika kilahaja cha Makunduchi kipashio ‘ja’ ni sawa na neno kama. Vilevile aliusifu mtaa wa Mwera ambako ndiko makaazi ya watawala wa Kiarabu katika karne za zamani alisema ukipita hapo askari hukwambia regeza mwendo ili usifanye fujo ya viatu. Kwa upande mwingine, Zuberi (2015) alibainisha kuwa jina la pahala mara kwa mara hubeba kumbukumbu ya historia, utamaduni, jamii, jiografia na lugha iliyotumika sehemu husika. Hoja hii inaunga mkono mtazamo wa Kadmon (2004) aliyebainisha kwamba siasa ina mchango mkubwa katika kubadili majina ya pahala, wageni wengi walipokuja Afrika na kuitawala waliweka majina ya pahala yanayotokana na utamaduni wao lakini nchi hizo zilipopata uhuru zilibadili majina hayo na kurejesha majina ya utamaduni wao.

Mfano, jina la *Sultan's palace* lilibadilishwa na kuwa *Peoples palace* (yaani jumba la wananchi) kufuatana na mabadiliko ya kisiasa yaliyotokea.

Kadmon (2004) anahusisha suala la majina ya pahala na dhana ya uchumi. Anabainisha kuwa jina la pahala linaweza kupelekea kuongezeka mapato ya kiuchumi likiwa litatumika vizuri katika biashara na bidhaa mbali mbali, kwa mfano, karafuu za Zanzibar. Kwa upande mwingine hata hivyo, majina ya pahala yanaweza yakawa chanzo cha migogoro ya kisiasa endapo yatatumika kwa namna ambayo yanaleta hisia tofauti kati ya jamii moja au jamii mbali mbali. Kwa mfano, ziwa Malawi kwa watu wa Malawi, na ziwa hilo hilo huitwa ziwa Nyasa kwa watu wa Tanzania. Maelezo haya yamempa mtafiti wa utafiti huu hamu ya kutafuta maana ya majina katika ukweli wake.

## 2.10 Pengo la Utafiti

Kila jamii ya watu ina upekee wake unaotokana na mazingira na utamaduni wa jamii husika. Hali hii hufanya utoaji wa majina ya maeneo kutofautiana pia. Kwa kuzingatia upekee huo, utafiti huu unakusudia kuchunguza ni misingi, michakato na mbinu gani ziliyotumika katika uundaji wa majina ya mitaa katika wilaya ya Mjini Unguja.

## 2.11 Kiunzi cha Nadharia

Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya uumbuji. Kwa mujibu wa Wardhaugh (1992) nadharia hii imeasisiwa na mwanaisimu wa Kimarekani Sapir na kuendelezwa na mwanafunzi wake Whorf. Nadharia hii hujulikana kama nadharia jumuishi ya Sapir Whorf.

Nadharia hii inaeleza kuwa lugha ndio msingi wa kuelewa ulimwengu wa jamii husika, lugha za jamii zinasaidia kufahamu utamaduni, historia, mazingira, hali za kiuchumi na kisiasa katika jamii husika. Nadharia hii inasisitiza kuwa lugha hufungamana na jamii bila ya jamii hakuna lugha.

Kwa vile majina ya mitaa ni kipengele cha lugha bila ya shaka majina hayo yana uhusiano na jamii husika. Pia nadharia hii inasisitiza kuwa ni vigumu kuchukua jina la sehemu kutoka jamii fulani na kuliita jina hilo sehemu nyingine kwa madai kuwa haliwezi kuwa na athari katika eneo lililoitwa. Lugha hubadilika kulingana na mazingira ya jamii, mabadiliko hayo huathiri majina ya mitaa baadhi yao yamedondosha au yamebadilisha viambishi, maneno na hata herufi.

Nadharia hii inatilia mkazo kuwa lugha hufuata jamii ilivyo na huelezea kile wanachokiona wanajamii wenyewe, na maana ya maneno hufahamika na watumiaji. Hivyo majina ya mitaa huelezea kilichomo ndani ya jamii na mazingira yanayoizunguka jamii ile.

Kwa kutumia mhimili huu, kutokana na mapendekezo ya Sapir na Whorf, mtafiti wa utafiti huu ametambulisha maana ya jamii kama kitu kilichopo na kinachohusu jamii. Kulingana na malengo ya utafiti huu vigezo, michakato na umuhimu wa majina ya mitaa ni vipengele vinavyotokana na lugha na mazingira yake, hivyo, matumizi yake katika malengo hayo yanaonesha namna lugha inavyofungamanana jamii

## 2.12 Hitimisho

Katika sura hii imeelezwa maana ya jamii, dhana ya utambulisho, kazi mbalimbali tangulizi zinazohusiana na mada hii, vigezo, umuhimu wa majina ya mitaa, pengo la utafiti na kiunzi cha nadharia. Sura inayofata itaelezea mbinu za utafiti.

# SURA YA TATU

# 3.0 MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inashughulikia mbinu za utafiti zilizotumika katika kukusanya data. Pia inafafanua eneo la utafiti kuwa ni kisiwani Unguja katika wilaya ya Mjini. Mada muhimu zinazoelezwa katika sura hii ni pamoja na muundo wa utafiti, eneo la utafiti, mbinu za ukusanyaji data, wahusika na sampuli za utafiti, pamoja na uchanganuzi wa data.

## 3.2 Muundo wa Utafiti

Utafiti huu umekuwa na muundo wa maelezo na takwimu. Kwa mujibu wa Mazhar (2013) njia ya maelezo inajihusisha na namna ya ulimwengu unavyochunguzwa, au unavyoonekanwa na kufahamu mahusiano ya mtu mmoja au vikundi katika matatizo mbali mbali. Pia anaeleza kuwa njia hii inaeleza hisia, mawazo na mahusiano yanayoeleza namna ya pahala, watu na matukio yalivyofanyika. Njia ya takwimu inahusisha taarifa zinazohusu idadi au namba za vitu vinavyohusika katika utafiti.

Kwa hivyo mtafiti ametumia miundo hii kwani imemwezesha kuelezea na kuchambua mawazo na hisia za watu mbali mbali kuhusu michakato na mbinu zilizotumika katika uundaji wa majina ya mitaa katika wilaya ya mjini ya Mjini Unguja, vilevile imeonesha takwimu kuhusu vigezo vya chimbuko la majina ya mitaa, njia za uundaji wa maneno ya majina ya mitaa, pamoja na miundo ya maneno ya majina ya mitaa ya wilaya ya Mjini Unguja.

### 3.3 Eneo la Utafiti

Eneo la utafiti ni sehemu ambayo utafiti umefanyika, yaani ni sehemu ambayo mtafiti amezipata data za utafiti wake. Utafiti huu umechunguza michakato na mbinu zilizotumika katika uundaji wa majina ya mitaa katika wilaya ya Mjini Unguja (angalia ramani nambari moja kwenye viambatanisho).

Hivyo utafiti huu umefanyika katika wilaya ya Mjini Unguja, ukihusisha mitaa mbali mbali iliyomo katika wilaya hii. Kwa mujibu wa Tanzania population census (2012), inaelezea kwamba wilaya ya Mjini ina jumla ya shehia 45 zenye wakaazi wapatao 223,033. Wakaazi wa wilaya ya Mjini Unguja wanafanya shughuli mbali mbali za kimaisha kama vile biashara, ufugaji, uvuvi, maofisini n.k. Mtafiti ameamua kufanya utafiti kwenye eneo hilo na sio lingine kwa sababu zifuatazo. Kwanza hili ndilo eneo ambalo Kiswahili sanifu kimezaliwa, yaani lahaja ya Kiunguja mjini ndio iliyosanifiwa na kuwa Kiswahili sanifu. Hakuna utafiti wowote uliofanywa kuhusu michakato na mbinu zilizotumika katika uundaji wa majina ya mitaa katika wilaya ya Mjini Unguja ambayo yana mchango katika kukuza Kiswahili na wenyeji wa wilaya hiyo katika shughuli zao mbali mbali. Na pia wilaya hii ina mji mkongwe ambao ni mji wa urithi wa kimataifa na ndio kitovu cha biashara na mambo mbalimbali.

### 3.4 Walengwa wa Utafiti

Ni wakaazi wa wilaya ya Mjini Unguja ambao idadi yao ni (223,033) kwa mujibu wa Tanzania census population ya mwaka 2012. Mtafiti wa utafiti huu amewashirikisha wazee wa kike na wa kiume, vijana wa kike na wa kiume, wasomi na watafiti wanaoishi eneo hili ambao wanaelewa asili na historia ya majina ya wilaya hii.

### 3.5 Usampulishaji

Kothari (2004) anaelezea dhana ya usampulishaji kuwa ni mchakato wa kuteua au kuchagua washiriki ambao utawatumia kupata data katika utafiti wako. Unapofanya usampulishaji huwa unatumia sampuli.

Sampuli ni sehemu ndogo iliyochaguliwa kutoka kwenye jumuiya ambayo imeteuliwa kwenye kundi kubwa ili itumiwe katika utafiti (Kothari, 2004). Watafitiwa hao wanaweza kuwa watu au vitu ambapo mtafiti huteuwa ili kufanya utafiti. Usampulishaji nasibu tabakishi ndio ametumia mtafiti kupata jumla ya watafitiwa 90. Jumla ya mitaa 30 imetumika katika utafiti huu, wazee wa kike na kiume walikuwa 39, vijana wa kike na kiume walikuwa 39 wasomi wa kike na kiume walikuwa 7 na watafiti wa kike na kiume walikua 5. Pia katika kuchagua watafitiwa suala l'umri limezingatiwa.

**Jedwali Na 3.1 : Linaloonesha Mgawanyiko wa Idadi ya Watafitiwa**

| | **JINSIA** | | |
|---|---|---|---|
| **WATAFITIWA** | **WANAUME** | **WANAWAKE** | **JUMLA** |
| WAZEE | 29 | 10 | 39 |
| VIJANA | 29 | 10 | 39 |
| WASOMI | 5 | 2 | 7 |
| WATAFITI | 4 | 1 | 5 |
| JUMLA KUU | 67 | 23 | 90 |

Mtafiti amechagua wale wazee wenye umri wa miaka 55 na kuendelea, kwa sababu wazee ndio wanaojua asili ya majina ya mitaa, sababu ya kuitwa majina hayo na matukio yanayoambatana na majina hayo. Vijana wenye umri wa miaka 25 – 40, kwa sababu ndio wanaoyatumia majina hayo mpaka sasa katika shughuli mbali mbali, vijana ndio wanaoleta majina mbadala na hilo linasaidia kujua hali ya baadae

ya asili ya majina ya mitaa. Jedwali Na 3.1 linaloonesha mgawanyiko wa idadi ya watafitiwa.

## 3.6 Mbinu za Ukusanyaji Data

Katika utafiti huu mtafiti ametumia mbinu mbali mbali kama vile uchunguzi makini, mahojiano, dodoso na mapitio ya nyaraka.

### 3.6.1 Uchunguzi Makini

Kwa mujibu wa Kothari (2004), mbinu ya uchunguzi makini ni mbinu aliyoitumia mtafiti katika utafiti wake kwa kuangalia moja kwa moja bila ya kuuliza chochote. Njia hii ni maalumu kwa kuangalia tabia za kisayansi lakini sio uchunguzi wa kisayansi. Vile vile njia hii inafaa kwa watu wasioweza kuelezea kwa mdomo hisia zao kwa sababu moja au nyengine. Kutokana na kutumia njia hii mtafiti amepata uhakika na uthibitisho wa maelezo ambayo washiriki wameyatoa kwa kuthibitisha kuwa yale aliyoelezwa na washiriki yapo au la. Kwa mfano baadhi ya mitaa imeitwa kutokana na majina ya maumbile asilia kama vile vilima, miti kama vile Mifenesi, Mibuyu, Miembe nk. Hivyo mtafiti ametembelea na kuiangalia miti hiyo ili kuthibitisha uwepo wake. Changamoto aliyopata mtafiti wa utafiti huu kupitia njia hii ni muda mrefu aliutumia katika kuchunguza ili kupata data za uhakika.

### 3.6.2 Mahojiano (usaili)

Mbinu hii kwa mujibu wa Enon (1998), ni mbinu ya kukusanya taarifa inayohusisha uulizaji wa maswali kwa njia ya mdomo au majadiliano. Njia hii imefanywa ana kwa ana baina ya mtafiti na watafitiwa. Utafiti huu ulifanywa kwa wazee ambao

hawakuweza kujaza dodoso za utafiti huu. Katika utafiti huu mtafiti ametumia maswali yaliyomwongoza katika kuwahoji watafitiwa. Njia hii imemsaidia mtafiti kupata mawazo na mtazamo wa mtafitiwa kuhusu jambo linalotafitiwa, na limemsaidia kupata taarifa za ziada ambazo si rahisi kuzipata kwa kutumia njia nyingine.

### 3.6.3 Dodoso

Kwa mujibu wa Kothari (2004), mbinu ya dodoso ni kutuma kwa mtu anayehusika maswali yaliyochapishwa kwa ajili ya kujibiwa na kurejeshwa dodoso.Njia hii ameitumia mtafiti kwa wataalamu na wakaazi ambao hawakuwa na muda kujibu maswali ya ana kwa ana.

Mtafiti amefaidika na mbinu hii kwa sababu muhusika ameyajibu kwa uhakika maswali yaliyokuwemo kwenye dodoso kwani muda umetolewa wa kutosha na mtafiti ametumia gharama ndogo. Changamoto alizopata mwandishi kupitia njia hii ni kuwa baadhi ya washiriki hawakuzirejesha dodoso na wengine hawakuzijaza dodoso hizo kikamilifu kama ilivyotarajiwa, hata hivyo mtafiti haikumzuia kupata data za utafiti huu kwani aliwatumia wataalamu wingine na wakaazi wingine kufanikisha malengo yake.

### 3.6.4 Mapitio ya Nyaraka

Kupitia nyaraka na machapisho mbali mbali mtafiti anapata taarifa anazotafuta kulingana na mada na malengo yake ya utafiti (Pons, 1992). Mtafiti ametumia mbinu hii kwa sababu taarifa nyingine muhimu ziko kwenye nyaraka na machapisho mbali

mbali ambazo zimemsaidia kufanya ulinganifu wa data alizozikusanya kwa njia ya mahojiano na dodoso. Pia ilimsaidia mtafiti kupata data kwa haraka na gharama zilikuwa hafifu. Nyaraka zilizotumika katika utafiti huu ni zile ambazo zinaelezea habari za majina ya mitaa, historia yake na vigezo vyake ambazo zimepatikana idara ya nyaraka na mambo ya kale na halmashauri ya wilaya mjini. Changamoto alizopata mtafiti kupitia njia hii ni muda mrefu wa kufatilia kibali cha utafiti na uchache wa nyaraka zinazohusu majina ya mitaa, lakini alikabiliana nayo kwa kila hali na kufanikisha malengo yake.

## 3.7 Mkabala wa Kimaadili ya Utafiti

Mukuthuria (2010), ameeleza maana ya maadili ya utafiti kuwa ni uwajibikaji na uwelekevu kitabia kuhusiana na haki za wale wote tunaotangamana nao katika utafiti, uwelekevu katika nia na malengo ya utafiti na jinsi ya kutumia matokeo kwa uadilifu ili yaweze kuwa na faida kwa ajili ya binaadamu. Katika utafiti huu, misingi ifuatayo ya maadili ilifuatwa:

**Kulinda haki za watafitiwa**: Mtafiti amelinda haki za wengine. Kwa mfano mtafitiwa alipotokezewa na jambo la dharura mtafiti alompa nafasi ya kufanya jambo hilo, kama ni mlemavu amezingatia hali yake ya ulemavu, na kama mtafitiwa ni mgonjwa mtafiti amejali afya yake mpaka alipopata nafuu nk.

**Kutunza siri:** Taarifa alizopewa mtafiti amezitumia vizuri yaani kwa lengo la utafiti tu na si vyenginevyo. Na kama taarifa hizo ni za siri mtafiti amezilinda na amezihifadhi.

**Uhuru wa kushiriki**: Watafitiwa walioshiriki katika utafiti huu hawakulazimishwa ila wameshirikishwa kwa hiari na ridhaa zao ili watoe mashirikiano mazuri kwa mtafiti.

Maadili hayo ya utafiti yameelezwa na watafiti mbali mbali katika vitabu vyao. Miongoni mwa hao ni Hammersley na Traianou (2012) ambao wametaja maadili hayo kuwa ni pamoja na kuepuka madhara, kuwaheshimu watu, kuhifadhi siri, kuwafanyia usawa washiriki katika matendo na watafitiwa wapewe taarifa kamili na wawe huru kushiriki.

Naye Van den Hoonard (2011), ameeleza maadili ya utafiti kuwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa utafiti usisababishe madhara kwa watafitiwa mmoja mmoja na watu wote. Mtafiti amheshimu mtafitiwa mmoja mmoja na watu wote kwa ujumla. Vilevile alinde haki na utu wa washiriki.

### 3.8 Uchanganuzi wa Data

Data za utafiti huu zimechanganuliwa kwa kutumia mbinu mseto (mixed method); ambayo imechanganya njia ya maelezo na njia ya kitakwimu. Kwa mujibu wa Kothari (2004), uchanganuzi wa data wa aina hii unahusisha idadi ya mambo yanayohusiana ambayo yanafanywa kwa lengo la kufafanua data zilizokusanywa na kuzipanga kwa namna ambayo zitatoa maelezo pamoja na takwimu zinazohusu maswali ya utafiti.

Mbinu mseto imeonekana inafaa katika utafiti huu kwa kuwa imewezesha kufahamu hisia na maono binafsi ya watafitiwa; na vilevile imewezesha kubaini idadi

(takwimu) ya vigezo vya majina, idadi ya mbinu za uundaji wa maneno ya majina; na pia idadi ya miundo mbalimbali ya maneno ya majina ya mitaa ya wilaya ya Unguja mjini.

## 3.9 Hitimisho

Sura hii imefafanua muundo wa utafiti, eneo la utafiti, walengwa wa utafiti na usampulishaji, mbinu mbalimbali za ukusanyaji data, mkabala wa maadili ya utafiti na uchanganuzi wa data.Sura inayofata inahusu uwasilishaji na uchanganuzi wa data.

# SURA YA NNE

# 4.0 UWASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA DATA

## 4.1 Utangulizi

Sehemu hii inawasilisha na kuchanganua taarifa za utafiti zilizopatikana kutokana na njia mbalimbali za kukusanya data zilizotumika ambazo ni uchunguzi makini, dodoso, mahojiano na mapitio ya nyaraka. Data zimewasilishwa na kujadiliwa kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Uwasilishaji umefanywa kwa kuzingatia malengo mahsusi ya utafiti, ambayo ni kubainisha vigezo vilivyotumika kutoa majina ya mitaa ya wilaya ya Mjini unguja, kuelezea michakato iliyotumika katika kutoa majina ya mitaa ya wilaya ya Mjini Unguja na kubainisha umuhimu wa majina ya mitaa ya wilaya ya Mjini Unguja katika kukuza lugha ya Kiswahili. Hivyo kwenye kila jina la mtaa ambalo limewasilishwa, yametolewa pia maelezo yanayoelezea kigezo au mchakato upi uliotumika katika kupata jina husika na pia umuhimu wa jina hilo hususan katika kukuza lugha ya Kiswahili.

## 4.2 Uwasilishaji wa data kuhusu Vyanzo, Michakato na Umuhimu wa Majina ya Mitaa

### 4.2.1 Mtaa wa Shangani

Mtaa wa Shangani upo katika wilaya ya Mjini Unguja katika mkoa wa Mjini Magharibi. Mtaa huu umepakana na mitaa ya Forodhani, Baghani, Sokomuhogo, na Mnazi mmoja. Shughuli muhimu zinazofanywa na wakaazi wa mtaa wa Shangani ni uvuvi, biashara na utalii.

#### 4.2.1.1 Asili na Mchakato wa Kuanzishwa Jina la Shangani

Kwa mujibu wa maelezo yaliyopatikana kutoka kwa wahusika wengi kwa njia ya mahojiano, huu ni mmoja wa mitaa mikongwe kabisa ya mji wa Unguja, kwa mujibu wa maelezo ya walengwa wa utafiti mtaa huu ulianzishwa katika karne ya 10 mwaka 950. Neno Shangani linatokana na neno "shanga" ambalo ni miongoni mwa mapambo ya Waswahili wa Afrika hususan hutumia wanawake, na hii "ni" inamaanisha pahala. Hivyo, jina Shangani lina maana ya "pahala penye shanga" au "zinapopatikana shanga". Mmoja wa wahusika wa uchunguzi huu alikuwa na haya ya kusema:

> Asili ya jina hili ni maingiliano ya watu kutoka sehemu mbali mbali, shughuli nyingi zilifanywa hapo miongoni mwao ni biashara,ambapo biashara kuu iliyokuwa inafanywa katika eneo hili ni uuzaji na ununuzi wa shanga. Kutokana na eneo hili kuwa linafanywa biashara hii kwa wingi ndiyo ilipelekea kuitwa Shangani, na kwa mujibu wa data za mahojiano na nyaraka mbalimbali ndipo mji ulipoanzia kuenea na baadae sehemu nyingine kwa sasa katika eneo hilo hakuna tena biashara ila limebakia jina tu."

Data za ushahidi zimekosekana kutokana na kutokuwepo tena shughuli za biashara hiyo katika eneo hili (Angalia ramani nambari 2).

#### 4.2.1.2 Kigezo cha Uanzilishwaji wa Jina la Shangani


Kigezo cha chimbuko la jina la Shangani ni kigezo cha shughuli za kiuchumi. Kwa sababu hizi shanga walizitumia kama ni biashara ili kuwasaidia katika maisha yao. Matokeo haya yanalingana na maelezo ya Helleland (2002), ambaye amesema kuwa kuna baadhi ya mitaa mingine hupata majina yake kutokana na harakati za kiuchumi zinazofanyika au zilizowahi kufanyika katika maeneo husika ni kama vile biashara, kilimo, uvuvi nk.

### 4.2.1.3 Umuhimu wa Jina la Shangani Katika Lugha ya Kiswahili

Jina la Shangani kama ilivyoelezwa hapo juu linatokana na unyambuaji wa neno ambao umeunganisha neno ‘***shanga***’ na mofimu “***ni*** ” ya pahali. Kwa hiyo, umuhimu mmoja wapo wa jina hili ni kuwa linatokana na matumizi ya njia moja wapo ya uundaji wa misamiati ya lugha ya Kiswahili. Vile vile, kuendelea kwa matumizi ya neno Shangani kunafanya neno hili lisisahaulike na liendelee kutumika, kwa sababu limo katika lugha ya Kiswahili na linatumika hadi sasa.  Kwa mujibu wa watafitiwa, wakaazi wa mtaa huu wanalitambua jina la Shangani, wanalipenda na wanataka libakie hivi hivi lisibadilishwe kwa sababu ni la asili, wamelizoea na maarufu.

### 4.2.2 Mtaa Wa Forodhani

Mtaa wa Forodhani unapatikana katika wilaya ya Mjini Unguja katika mkoa wa Mjini Magharibi. Mtaa huu unapakana na mitaa ya Shangani, Gizenga, Hurumzi na Malindi.




**Ramani Na 4.1:  Baadhi ya Mitaa ya Mji Mkongwe na Ng’ambo Miaka ya 1890**

Chanzo: http://indian-ocean.africa.si.edu/ (Imepatikana 22.9.2016)

Wakaazi wa mtaa wa Forodhani hujishughulisha na biashara, utalii na uvuvi. Katika mtaa huu kuna jumba la kumbukumbu la *Beit el ajaib*, ngome kongwe na bustani nzuri ambayo ni kivutio kwa wageni na wenyeji (Angalia ramani na 4.1).

### 4.2.2.1 Asili na Mchakato wa Kuanzishwa Jina la Forodhani

Kutokana na mahojiano na mapitio ya nyaraka mbalimbali ilibainika kwamba jina la Forodhani linatokana na neno "forodha" ambalo kwa tafsiri ya TUKI (2014) maana yake ni bandari au mahali pa kutozea ushuru wa vitu vinavyoingia au kutoka nchini wakaazi wa eneo hili wanaeleza kuwa jina hili lilianza kutumiwa katika karne ya 19, ambapo watu waliokuwa wakitumia sehemu hii kwa shughuli zao za kutoa bidhaa mbalimbali katika bandari hii ndio walioanzisha jina hili. Kwa mujibu wa maelezo ya mmoja wa wahusika wa uchunguzi huu chanzo cha eneo hili kuitwa Forodhani ni kuwa;

> Sehemu hiyo ilikuwa ni makaazi ya pwani ambapo watu kutoka sehemu mbali mbali walikuja sehemu hiyo na majahazi ili kuuza na kununua bidhaa na wanapofika eneo lile walitoa ushuru katika nyumba maalumu iliyotumika kukusanyia ushuru huo kwa kila aliyetumia bandari hiyo kwa shughuli mbalimbali."

### 4.2.2.2 Kigezo cha Uanzilishwaji wa Jina la Forodhani

Shughuli za uchumi zilizokuwa zinaendeshwa kwenye eneo lile inaonekana kuwa ndicho kigezo kilichotumika kuanzishwa kwa jina hili. Katika sehemu hii, watu walikuwa wanauza na kununua bidhaa pamoja na kutoa ushuru. Kuna baadhi ya wataalamu mbalimbali wameelezea kuwa shughuli za kiuchumi kuwa ni kigezo katika kutoa majina ya pahala, miongoni mwao ni Helleland na wenzake (2010) wao wameeleza kwamba baadhi ya mitaa hupata majina yake kutokana na harakati za kiuchumi zinazofanywa katika maeneo hayo kama vile biashara, uvuvi nk. Matokeo

haya yanashabihiana na ugunduzi wa Helleland (ameshatajwa) kuwa majina ya mitaa yanahifadhi kumbukumbu na matukio yaliyopita.

#### 4.2.2.3 Umuhimu wa Jina la Forodhani Katika Lugha ya Kiswahili

Kama yalivyo kwa majina mengi yanayotumika jina la Forodhani linatokana na msamiati wa Kiswahili. Hivyo umuhimu wa jina hili ni kuwa linadumisha na kukuza misamiati ya lugha ya Kiswahili kwani asili ya neno hili ni la lugha ya Kiarabu ambapo neno "***forodha***" likiwa na maana ya mahali pa kutoza ushuru wa vitu vinavyoingia au kutoka nchini (TUKI, 2014), (kama ilivyoelezwa hapo juu) na mofimu "***ni***" ya pahala. Umuhimu mwingine wa jina Forodhani ni kuwa jina hili linatokana na njia moja wapo ya uundaji wa misamiati inayoitwa kutohoa yaani ya kuazima kutoka katika lugha ya Kiarabu, pia hudumisha matumizi ya Kiswahili, kwa sababu jina hili sio sana kutumika badala yake linatumika bandari, hivyo matumizi ya jina hili yanasaidia neno hili liendelee kudumu na kutumika katika lugha ya Kiswahili.

Jina la Forodhani linaelezea na kuhifadhi historia ya matukio yaliyotokea mahala hapo. Pia wakaazi wake wanapenda jina hili libakie hivi hivi kwa sababu limezoeleka linafurahisha, maarufu na ni jina linaloonesha historia ya eneo husika.

### 4.2.3 Mtaa wa Darajani

Mtaa wa Darajani upo katika wilaya ya Mjini katika mkoa wa Mjini Magharibi. Mtaa huu umepakana na mitaa ya Kiponda, Vikokotoni, Malindi, Mkunazini na Mtendeni. (Rejea ramani nambari 2).Wakaazi wa mtaa huu wanajishughulisha na biashara mbalimbali, vile vile mtaa huu una ofisi mbalimbali za serikali na binafsi.

### 4.2.3.1 Asili Na Mchakato wa Kuanzishwa Jina la Darajani

Data zilizopatikana kutokana na njia ya mahojiano na mapitio ya nyaraka, zinadhihirisha kuwa jina la Darajani lilianza kabla ya mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964. Jina hili limeanzishwa na wakaazi na wenyeji wa eneo hilo. Sababu ya kuanzishwa jina la Darajani kwa mujibu wa maelezo ya mmoja wa watafitiwa ni kulikuwepo na daraja katika eneo hilo ambalo lilijengwa mwaka 1835 na Sultan Seyyid Said na baadae likaboreshwa na sultan wengine, daraja hilo lilikuwa linaunganisha sehemu mbili za mji wa Unguja: ambazo ni Mjimkongwe na Ng'ambo kwa wakatihuo, daraja hilo lilikuwa  kwenye njia ambayo inatokea kwa Suma hadi kwa Muzammil zinapouzwa haluwa. Drummond (ameshatajwa) kutilia mkazo maelezo haya anaeleza kuwa majina ya pahala hurejelea mandhari, maumbile asilia au yaliyotengenezwa na binaadamu.

Katika mahojiano, mkaazi mmoja wa mtaa wa Darajani alieleza ifuatavyo:

> Katika barabara ya kutoka Mnazi mmoja mpaka Malindi eneo hili lilikuwa na maji ndio likajengwa daraja hilo, na baadae eneo hilo lilifukiwa ndiyo sasa ipo hiyo barabara,  ili iwe rahisi kutoka na kwenda nga'mbo na mji. Daraja hili, kwa sasa halipo lakini jina bado lipo na linatumika mpaka muda huu."  (Rejea picha nambari 4.1).



**Picha Na 4.1: Daraja Lililokua Likiunganisha Kati ya Mji Mkongwe na Ng'ambo**

Chanzo:http://indianocean.africa.si.edu/wpcontent/uploads/2014/11/map32.jpg

#### 4.2.3.2 Kigezo cha Uanzilishwaji wa Jina la Darajani

Kigezo kilichotumika kuanzishwa jina la Darajani ni kigezo cha kimaumbile, ambapo watu walivutika kuwepo daraja hili ambalo liliunganisha kati ya jamii inayokaa mji mkongwe na jamii inayokaa ng'ambo katika kufanikisha shughuli zao mbalimbali. King (2008), katika utafiti wake unaohusu majina ya pahala, amegundua kuwa majina ya pahala yameitwa kutokana na kigezo cha maumbile ambacho kinakuwepo, majina ya mahala humo huendelea kuwepo kwa muda mrefu kwa vizazi vingine.

#### 4.2.3.3 Umuhimu wa Jina la Darajani Katika Lugha ya Kiswahili

Jina hili linatokana na neno "***daraja***" ambalo maana yake ni kivuko kilichojengwa kwa zege na vyuma, miti au mbao kwa ajili ya kuvukia mto au mfereji (TUKI, 2014). Jina hili linatokana na unyambuaji wa neno ambao umeunganisha neno "***daraja***" na mofimu "***ni***" ya pahala. Miongoni mwa umuhimu wa jina hili unatokana na njia moja wapo ya uundaji wa misamiati ya lugha ya Kiswahili.Vile vile kuendelea kwa matumizi ya neno Darajani kunafanya liendelee kutumika na lisisahaulike.

Mitaa midogo midogo iliyopo katika mtaa wa Darajani ni Marikiti, Kwa Suma, Jumba la treni, Ngazi nje, Jua kali n.k. Jina la Darajani linatambulika na watu wengi hadi sasa, na wakaazi wake wanapenda libakie hivi hivi lisibadilishwe na wanalifurahia. Jina la Darajani linatambulika na watu wengi hadi sasa, na wakaazi wake wanapenda libakie hivi hivi lisibadilishwe na wanalifurahia kwani linatoa taswira nzuri.

### 4.2.4 Mtaa Wa Sokomuhogo

Mtaa wa Sokomuhogo unapatikana katika wilaya ya Mjini Unguja, katika mkoa wa Mjini Magharibi. Mtaa huu unapakana na mitaa ya Shangani, Kajificheni, Hamamni na Gizenga.Wengi wa wakaazi wa eneo hili ni wajasiri amali wadogo wanaojishughulisha na biashara ndogondogo kama vile, udobi (kufua na kupiga pasi nguo) na useremala (Rejea ramani nambari 2 kwenye viambatanisho). Katika mtaa huu kuna mtaa mdogo uitwao Jaws corner ambao unakwenda sambamba kwa umaarufu na mtaa huu wa Sokomuhogo; hii ni sehemu ambayo watu wengi hasa wanaume wanakaa kwa ajili ya mazungumzo yao mbalimbali ya kijamii na kisiasa pamoja na kunywa kahawa.

#### 4.2.4.1 Asili na Mchakato wa Kuanzishwa Jina la Sokomuhogo

Data zilizopatikana kutokana na usaili na mapitio ya nyaraka zinaonesha kuwa mtaa wa Sokomuhogo ulianzishwa kabla ya mapinduzi ya mwaka 1964. Kwa mujibu wa taarifa za watafitiwa asili ya jina hili ni kuwa katika eneo hili palikuwa na soko ambalo watu kutoka maeneo mbalimbali walikuja kwenye mtaa huu kwa nia ya kufanya biashara ya mihogo; ambapo wengi walijihusisha katika kuuza au kununua mihogo mibichi na hata ya kuchoma. Mmoja wa watafitiwa alifafanua chimbuko la jina la Sokomuhogo kwa maelezo yafuatayo:

> Watu kutoka sehemu mbalimbali walikuwa wanakuja kuuza na kununua mihogo katika eneo hili kwa ajili ya chakula chao. Kwa hiyo watu waliokuwa wakitumia soko hili yaani wakaazi na wafanyabiashara, ndio wakapaita Sokomuhogo.

Taarifa za utafiti zinaonesha kuwa ingawa soko hili lilikuwa linauzwa bidhaa mbalimbali lakini bidhaa kubwa na maarufu ilikuwa ni mihogo. Matokeo haya

yanalingana na maelezo ya Arthur (ameshatajwa) kuwa kazi ya pahala kama soko, ngome, shamba au umbile asilia inaweza kuwa chimbuko la jina la pahala. Ingawa mtaa huu ungali na jina hilo lakini uchunguzi wa ushuhuda umeonesha kuwa kwa sasa soko hili halipo tena limehamia katika soko kuu la Darajani lakini jina bado lipo na linatumika.

#### 4.2.4.2 Kigezo cha Uanzilishwaji wa Jina la Sokomuhogo

Shughuli za biashara ya mihogo inaelezwa kuwa ni kigezo cha kiuchumi, kwa sababu ni shughuli ambayo watu waliifanya ili kujipatia pesa za kukidhi mahitaji yao mbalimbali ya kila siku na ya kimaisha kwa ujumla. Hivyo chimbuko la jina la mtaa huu ni shughuli ya uchumi.

#### 4.2.4.3 Umuhimu wa Jina la Sokomuhogo Katika Lugha ya Kiswahili

Jina hili la Sokomuhogo ni la msamiati wa Kiswahili linatokana na mwambatano wa maneno. Neno Sokomuhogo limeundwa na maneno mawili tofauti yenye maana tofauti. Neno la mwanzo ni "***soko"*** ambalo kwa tafsiri ya TUKI (2014) lina maana ya mahala penye mkusanyiko wa wanunuzi na wauzaji wengi wa bidhaa za rejereja. Neno la pili ni ***"muhogo"*** ambalolinaelezwa na TUKI (2014) maana yake ni mzizi wa mmea wenye shina lenye viduntu na moyo mwororo ambao unazaa mihogo pia majani yake yanatumika kama mboga ya kisamvu na mzizi huo unapokuwa tayari huliwa. Maneno haya mawili yameunganishwa na kutoa neno jipya Sokomuhogo ambalo maana yake ni mahala panapouzwa na kununuliwa mihogo. Hivyo umuhimu mmoja wapo wa jina hili ni kuwa linatokana na matumizi ya njia ya uundaji wa misamiati iitwayo uambatishaji maneno. Pia linakuza na kudumisha matumizi ya

lugha ya Kiswahili kupitia jina husika, ambapo kuendelea kutumiwa jina hili litafanya maneno haya yaendelee kutumika na yasisahaulike.Jina la mtaa huu linatambulikana na wengi na wanapenda liendelee hivi hivi kwa sababu limezoeleka, maarufu na linafurahisha kwa kuleta taswira nzuri.

### 4.2.5 Mtaa wa Hamamni

Mtaa huu wa Hamamni uliopo katika wilaya ya Mjini Unguja katika mkoa wa Mjini Magharibi. Mtaa huu unapakana na mitaa ya Kajificheni, Sokomuhogo, na Hurumzi.

#### 4.2.5.1 Asili na Mchakato wa Kuanzishwa Jina la Hamamni

Neno Hamamni lina maana ya mahodhi ya kuogelea ambayo hujengwa ili yatumike kwa kuogea TUKI (2014). Kwa mujibu wa data za mahojiano mtaa huu ulianzishwa kabla ya mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964. Jina hili linatokana na mahodhi au hamam ambayo yalijengwa maalumu kwa kuogea watu wenye hadhi ya juu. Kwa mujibu wa moja wa Wakaazi wa mtaa huu ndio waliolianzisha jina hili. Kwa mujibu wa mmoja wa wakaazi wa eneo hili alikuwa na haya ya kusema:

> Sultan Baraghash alijenga jumba katika eneo hili na ndani ya jumba hilo alijenga mahodhi ambayo aliyatumia kwa ajili ya kukoga, ikawa kama ni starehe yake kila anapotaka kukoga anakwenda kwenye mahodhi hayo ndio sababu iliyopelekea eneo hili likaitwa jina hilo" (Angalia picha nambari 4.2).



**Picha Na 4.2: Hamamu Lenyewe**

Chanzo;http://zanziplanet.com/wpcontent/u (Imepatikana 22.9.2016)

#### 4.2.5.2 Kigezo cha Uanzilishwaji wa Jina la Hamamni

Maana ya jina Hamamni ni mahala penye hamam Kigezo kilichotumika katika kuliita jina hili ni cha kimaumbile, maumbile yaliyotoa jina hili ni hamamu lililojengwa na mfalme Baraghash kuwa ni starehe na burudani yeye na familia yake kwenda kukoga katika mahodhi hayo, jambo hili lilikuwa jambo geni kwa wakaazi wa eneo hili kwa sababu hakukuwa na mtu yeyote ambaye alikuwa anafanya hivyo. Hali hiyo ilipelekea kutambulika mahodhi hayo na jina la Hamamni kuanza kutumika. Drummond (ameshatajwa) kutilia mkazo maelezo haya anaeleza kuwa majina ya pahala hurejelea mandhari, maumbile asilia au yaliyotengenezwa na binaadamu.

#### 4.2.5.3 Umuhimu wa Jina la Hamamni Katika Lugha ya Kiswahili

Jina hili la Hamamni linatokana na unyambulishaji neno ***"hamam"*** kama ilivyoelezwa hapo juu kwa kuongeza mofimu –***"ni***" ya pahala. Umuhimu wa jina Hamamni ni kuwa linatokana na tukio, matumizi yake yanadumisha ukweli wa tukio la kihistoria ambalo lilitokea katika jamii ya Waswahili. Vilevile neno hamam lina asili ya kiarabu, hivyo kutumika kwake katika jamii ya Kiswahili ni kutokana na njia moja wapo ya uundaji wa maneno ambayo ni kutohoa, njia hii ni ya kuazima maneno kutoka lugha moja kwenda nyingine. Kwa njia hii neno hamam limeazimwa na kuingia katika lugha ya Kiswahili. Matumizi yake yamesaidia kukuza misamiati ya lugha ya Kiswahili kwani limeongeza maneno katika Kiswahili.

Umuhimu mwingine wa jina hili ni kutokana na matumizi yake kutalifanya lisipotee na lisisahaulike kwa sababu vijana wa sasa hawalijui kwa vile hawalitumii. Wakaazi

na watu mbalimbali wanapenda jina hili libakie hivi hivi lisibadilishwe kwa sababu ni jina maarufu, limezoeleka, linawafurahisha na linaelezea historia nzuri ya eneo hili kwa vizazi vya sasa na vya baadae.Matokeo haya yanakubaliana na maelezo ya Meiring (ameshatajwa) kwamba jina la pahala huweza kubeba kumbukumbu ya historia, utamaduni, jiografia ya jamii na lugha inayotumika katika sehemu husika.

### 4.2.6 Mtaa wa Funguni

Mtaa wa Funguni upo wilaya ya Mjini Unguja katika mkoa wa Mjini Magharibi, mtaa huu umepakana na Hoteli ya Bwawani Plaza na Malindi. Baadhi ya shughuli muhimu za kijamii zinazofanywa katika mtaa huu ni za uvuvi na biashara. Mtaa wa Funguni umejengwa na mitaa midogo midogo kama vile Jongeani, kwa Mchina tambi, Bwawani nk mitaa ambayo imezuka kutokana na maumbile pamoja na shughuli za kijamii zinazofanyika. Jina la Funguni linatambulika na watu wengi sana kwa vile ni moja ya mitaa mikongwe katika mji wa Zanzibar (Rejea ramani Na 4.1).

#### 4.2.6.1 Asili na Mchakato wa Kuanzishwa Jina la Funguni

Kwa mujibu wa data za mahojiano mtaa huu ulianzishwa kabla ya mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964. Neno Funguni ni neno la msamiati wa Kiswahili na linatokana na neno fungu ambalo linafasiriwa na TUKI (2014) maana yake ni shungu la mchanga uliokusanyika baharini. Jina hili lilianzishwa na wavuvi na watu walioishi karibu na eneo hili. Mmoja wa wahusika wa utafiti huu alikuwa na haya ya kueleza:

> Kuanzishwa jina hili kunatokana na kuwepo kwa fungu la mchanga katika eneo hilo lililozungukwa na bahari katika pande zake zote, kabla ya hapo hapakuwa na jina jengine kwa sababu watu walikuwa hawaishi katika eneo hili. Kwa sasa sehemu hii imefukiwa na kupoteza umbile

> lake la asilia la fungu, kutokana na kuwepo fungu hilo ndio eneo hilo likaitwa Funguni".

#### 4.2.6.2 Kigezo cha Uanzilishwaji wa Jina la Funguni

Kigezo ambacho kilichotumika cha kuanzishwa jina la mtaa huu ni kigezo cha maumbile, kwa sababu fungu hilo halikuanzishwa na watu ila wamelikuta tuu katika eneo hili. Langford (2013), katika kufafanua vigezo vya utoaji majina ameelezea pia kigezo hiki cha kimaumbile kwa kusema kuwa baadhi ya mitaa hupata majina yake kwa kuwepo maumbile asilia mbalimbali kama vile milima, mito, miti na mengineyo.

#### 4.2.6.3 Umuhimu wa Jina la Funguni Katika Lugha ya Kiswahili

Jina la Funguni linatokana na msamiati wa Kiswahili. Kama tulivyoeleza hapo juu jina hili linatokana na neno ***"fungu"*** lililoambatanishwa na mofimu –'***_ni_***' ya pahala. Umuhimu wa mwanzo wa jina hili linatokana na matumizi ya njia ya uundaji wa misamiati ya lugha ya Kiswahili ya unyambuaji kutokana na neno "fungu" kuunganishwa na mofimu –'_ni_'. Pia linaeleza dhana ya jina lilotumika kwa kutoa maana halisi, kwani mtu anapolisikia anaweza kuelewa asili yake imekusudiwa kitu fulani. Lehrer (ameshatajwa) anaeleza kuwa maana inayopatikana katika majina ya mitaa huwakilisha dhana ya kitu chenyewe kinachohusiana na majina husika ya mitaa. Vilevile, linadumisha matumizi ya msamiati wa lugha ya Kiswahili kupitia jina hili kwa kulifanya liendelee kutumika na lisisahaulike.Vilevile jina Funguni ni jina la pekee katika misamiati ya majina katika mji wa Zanzibar. Watu wengi wanaoishi eneo hili wanapenda jina hili libakie hivi hivi kwa sababu linawafurahisha, wamelizoea na ni jina la asili.

### 4.2.7 Mtaa Wa Mnazi Mmoja

Mtaa wa Mnazimmoja upo katika wilaya ya Mjini Unguja katika mkoa wa Mjini Magharibi. Mtaa huu unapakana na mitaa ya Kikwajuni, Vuga, Shangani na Mkunazini. Katika eneo hili ndiko kuna hospitali kuu ya Mnazimmoja, Ikulu, mahakama kuu, kituo cha televisheni cha Karume house, ofisi mbali mbali na uwanja mkubwa ambao hutumika kwa shughuli mbalimbali za kijamii, kiuchumi na kisiasa (Rejea ramani nambari 4.1 ).

Katika mtaa wa Mnazimmoja kuna mitaa midogo midogo inayotaja vitongoji mbalimbali vya mtaa huo, baadhi ya vitongoji hivyo ni; Mnazimmoja makumbusho, Uwanja wa Mnazimmoja, Mnazimmoja hospitali, Victoria garden, Ikulu, Msikiti wa majamvi, Majestic nk.

#### 4.2.7.1 Asili na Mchakato wa Kuanzishwa Jina la Mnazimmoja

Data za mahojiano na mapitio ya nyaraka ambazo zinaonesha kuwa jina la mtaa huu lilianzishwa katika karne ya 19 mwaka 1872 wakati wa utawala wa mfalme Sayyid Baraghash.Neno Mnazimmoja linaelezea kuwepo kwa mnazi mmoja pekee katika eneo ambalo awali lilikuwa na minazi mingi. Hali hii ilitokana na tufani kubwa ambayo iliambatana na upepo mkubwa uliotokea katika mji wa Zanzibar. Upepo huo uling'oa miti mingi na kuharibu majengo mengi. Miti michache sana ilibakia baada ya tukio hilo, ikiwemo mnazi mmoja uliokuwa umesimama pekee na kuonekana waziwazi. Mmoja wa watafitiwa kwa njia ya usaili alieleza ifuatavyo:

> Jina hili lilianza kutokana na maafa ya kimbunga kilichotokea katika eneo hili mwaka 1872.Kimbunga hicho kilisababisha nusu ya miti mikubwa kama vile miembe, mibuyu, minazi n.k kungoka. Upepo huo

> wa kimbunga uliotokea kusini mashariki na kuelekea kaskazini magharibi mpaka sehemu za Tanga, uliacha eneo hilo likibakia na mnazi mmoja ndio ulionusurika ikawa ndio sababu ya mtaa huo kuitwa Mnazi mmoja.

Mapitio ya nyaraka vilevile yanadhihirisha kuwa katika mtaa huo kuna mtaa wa Mji mpya, huu ulianza miaka ya baadae baada ya kuanzishwa ujenzi wa makaazi mapya ya watu katika moja ya eneo hilo.

#### 4.2.7.2 Kigezo cha Uanzilishwaji wa Jina la Mnazimmoja

Kigezo kilichotumika kuanzishwa jina hili ni kigezo cha kimaumbile kwa sababu minazi ilikuwa ipo katika eneo hilo ila baada ya kutokea kimbunga ndio ukabakia huo mnazi mmoja tu. Matokeo haya yanakubaliana na maelezo ya King (ameshatajwa), kuwa majina ya pahala yanaweza kutokana na kigezo cha maumbile asilia na yasiyo asilia ambayo yapo katika eneo husika.

#### 4.2.7.3 Umuhimu wa Jina la Mnazimmoja Katika Lugha ya Kiswahili

Jina la Mnazimmoja linatokana na maneno mawili tofauti na yenye maana tofauti. Neno la kwanza ni ***"mnazi***" ambalo maana yake ni mti mrefu usiokuwa na panda unaotoa matawi yenye majani marefu yanayotumika kwa kujengea na matunda yanayoitwa nazi ambayo hutumiwa kupikia vyakula mbalimbali au kutengenezea mafuta (TUKI, 2014), neno la pili ni ***"mmoja***" ambapo moja ni tarakimu ya idadi ya kwanza ya mamoja, yaani "1" (TUKI, 2014) Hivyo, umuhimu wa jina hili unatokana na njia ya uundaji wa misamiati ya Kiswahili iliyotumika ya uambatishaji wa maneno. Vile vile linakuza misamiati ya Kiswahili kutokana na maneno haya mawili tofauti yenye maana tofauti tunapata neno moja ambatano Mnazimmoja lenye maana

ya mtaa ulio na mnazi mmoja. Wakaazi wake wanapenda jina hili libakie hivi hivi kwani ni la asili, maarufu na limezoeleka.

### 4.2.8 Mtaa wa Mkunazini

Mtaa huu wa Mkunazini upo katika wilaya ya Mjini Unguja katika mkoa wa Mjini Magharibi. Mtaa huu umepakana na mitaa ya Kibokoni, Marikiti ya Darajani, Hamamni, Ukutani, Kajificheni na Mnazimmoja. Mtaa wa Mkunazini ni moja ya mitaa mikongwe ya mji wa Zanzibar. Katika mtaa huu kuna mitaa mingine midogo midogo ambayo ni; Ukutani, Kwa Batashi, Sunni Madrasa, Kwa Sati, Msikiti Gofu, Msikiti Gibril, Empire, Kinu cha soda, Kwa Chavda, Kwa Kimoto, Bekari, Mlango wa chuma, Msikiti Luta.

#### 4.2.8.1 Asili na Mchakato wa Kuanzishwa Jina la Mkunazini

Jina la Mkunazini linatokana na neno “mkunazi” ambalo linafasiliwa na TUKI (2014) kuwa ni mti wenye miba na majani madogo madogo unaozaa kunazi ambazo zinaliwa. Data za mahojiano na mapitio ya nyaraka zinasema kuwa jina la mtaa huu lilianzishwa kutaja uoto wa mikunazi ambao ulipatikana katika eneo hilo. Mkaazi mmoja wa eneo hili alieleza kuwa:

> Jina la Mkunazini linatokana na mti mkubwa wa mkunazi kwenye makaburi ambao ulikuwa karibu na msikiti Jibril, vilevile kwenye misikiti mingi ya eneo hili kulikuwa mikunazi na makaburi. Ingawa kwa sasa kuna mikunazi mingine midogo midogo ambayo imeota katika eneo hili kutokana na sababu hiyo ndio eneo hili pakaitwa Mkunazini.

#### 4.2.8.2 Kigezo cha Uanzilishwaji wa Jina la Mkunazini

Jina la Mkunazini linatokana na utambuzi wa maumbile ya eneo hilo, linatokana na kuwepo kwa mti mkubwa wa mkunazi. Hivyo kigezo cha kuanzishwa kwa jina hilo

ni kigezo cha kimaumbile kutokana na kuwepo kwa mti huu wa mkunazi katika eneo hili, mkunazi huu umeota wenyewe na wala haukupandwa. Matokeo haya yanakubaliana na ufafanuzi wa King (ameshatajwa), kuwa maumbile asilia na yasiyo asilia ya eneo fulani huweza kuwa kigezo cha kupatia jina la pahala hapo.

#### 4.2.8.3 Umuhimu wa Jina la Mkunazini Katika Lugha ya Kiswahili

Jina la Mkunazini kama ilivyoelezwa hapo juu linatokana na unyambuaji wa neno "***mkunazi***" na mofimu –"***ni"*** ya pahala. Kwa hivyo, umuhimu wa jina hili unatokana namatumizi ya njia hii ya uundaji wa misamiati ya lugha ya Kiswahili. Pia linadumisha matumizi ya lugha ya Kiswahili pale linapotumika kwa kufanya lisisahaulike liendelee kutumika. Wakaazi wa eneo hili wanapenda libakie hivi hivi lisibadilishwe kwa sababu wamelizoea, maarufu na jina la asili.

### 4.2.9 Mtaa Wa Gulioni

Mtaa huu upo katika wilaya ya Mjini Unguja katika mkoa wa Mjini Magharibi. Mtaa huu unapakana na mitaa ya Mfenesi mazizi, Miti ulaya, Mbuyu taifa, Makadara na Kinazini. Shughuli kubwa ya wakaazi wa mtaa huu ni biashara.

#### 4.2.9.1 Asili na Mchakato wa Kuanzishwa Jina la Gulioni

Data za mahojiano na mapitio ya nyaraka zinadhihirisha kuwa jina la mtaa huu lilianzishwa mnamo karne ya 19 na wenyeji waliokuwa wanakaa au waliokuwa wanaitumia sehemu hiyo. Neno Gulio ni msamiati wa lugha ya Kiswahili maana yake ni soko lifanywalo mara moja kwa juma au mwezi (TUKI, 2014). Ingawa soko hili limeelezwa kuwa ni la muda maalumu au msimu fulani lakini kwa hapa

Zanzibar Gulio ni soko la wakati wowote. Akijibu maswali ya usaili, mkaazi wa mtaa huu na mmoja wa watafitiwa wa utafiti huu alieleza kuwa:

> Jina hili lilianzishwa kutokana na kuwepo kwa gulio (soko) ambalolikitumika kwa shughuli za kibiashara za kuuza na kununua bidhaa mbalimbali.

Data za uchunguzi makini hazikuweza kupatikana kwa sababu kwa sasa soko hilo halipo limebaki jina tu.

#### 4.2.9.2 Kigezo cha Uanzilishwaji wa Jina la Gulioni

Kigezo kilichotumika kuanzishwa jina hili ni kigezo cha kiuchumi ambapo kuwepo kwa gulio (soko) hilo, ambapo lilitumiwa na wakaazi wa eneo hilo katika shughuli zao mbalimbali za biashara. Mitaa mingine hupata majina yake kutokana na harakati za kiuchumi kama vile biashara, uvuvi nk. (Helleland na wenzake, 2012).

#### 4.2.9.3 Umuhimu wa Jina la Gulioni Katika Lugha ya Kiswahili

Jina la Gulioni linatokana na unyambuaji wa neno "***gulio***" na mofimu –ni ya pahala. Kwa hivyo, umuhimu mmoja wapo wa jina hili ni kuwa linatokana na njia mojawapo ya uundaji wa misamiati ya lugha ya Kiswahili .Vile vile kuendelea kwa matumizi ya neno gulioni kunafanya msamiati huu usipotee na usisahaulike kwa sababu watoto na vijana wa sasa hawalijui neno gulio kwa vile halitumiki. Pia linaelezea dhana ya jina lililotumika kwa kutoa maana halisi ya jina lenyewe yaani ni mahali penye soko. Lehrer (ameshatajwa) anasema kuwa maana inayopatikana katika majina ya mitaa huwakilisha dhana ya kitu chenyewe kinachohusiana na majina husika ya mitaa. Jina hili watu wanalipenda libakie hivi hivi, kwa sababu la asili, limezoeleka na linafurahisha kwa ktuoa taswira nzuri ingawaje kwa muda huu hilo gulio halipo tena.

### 4.2.10 Mtaa wa Kisiwandui

Mtaa wa Kisiwandui unapatikana katika wilaya ya Mjini Unguja katika mkoa wa Mjini Magharibi. Mtaa huu unapakana na mitaa ya Kikwajuni, Michenzani, Vikokotoni na Kisimamajongoo na Darajani (Angalia ramani nambari 4.1).

#### 4.2.10.1 Asili na Mchakato wa Kuanzishwa Jina la Kisiwandui

Kwa mujibu wa data za mahojiano na zile kutoka dodoso, jina hili la Kisiwandui lilianzishwa katika karne ya 19. Sababu ya kuanzishwa jina hili ni kuwa eneo hili lilikuwa ni kisiwa kilichotumika kuwahifadhi watu wenye maradhi ya ndui, ambapo maradhi haya yalikuwa ni mabaya na yanaambukiza, kwa hiyo wale waliopata maradhi haya waliwekwa katika kisiwa hiki ili kupewa huduma mbalimbali za matibabu. Mkaazi mmoja wa eneo hili alikuwa na haya ya kusema:

> Kabla ya eneo hili kuanza kutumiwa kuwahifadhi wagonjwa wa ndui na kuitwa Kisiwandui wengine walipaita Pwani ndogo wengine walipaita Pwani mbovu. Hivyo, kutokana na kuhifadhiwa wagonjwa wa ndui katika kisiwa hicho eneo hili likaitwa Kisiwandui.

#### 4.2.10.2 Kigezo cha Uanzilishwaji wa Jina la Kisiwandui

Kigezo kilichotumika kuanzishwa jina hili ni kigezo cha shughuli za kijamii. Shughuli iliyokuwa ikifanywa kwenye eneo hili ni ile ya kuhifadhi wagonjwa wa ndui. Kwa hiyo jina lililopewa eneo hili lilihusisha dhana ya shughuli ya uhifadhi wagonjwa wa ndui. Dhana hii inakubaliana na maelezo ya Drummond (ameshatajwa) aliyesema kuwa majina ya pahala huweza kurejelea mandhari, maumbile asilia au shughuli zinazofanywa na binaadamu. Kisiwa kinachorejelewa katika jina hili kwa sasa hakipo tena kilifukiwa zamani na mamlaka za utawala, lakini jina linaendelea kutumika mpaka muda huu.

#### 4.2.10.3 Umuhimu wa Jina la Kisiwandui Katika Lugha ya Kiswahili

Jina la Kisiwandui linatokana na mwambatano wa maneno mawili tofauti ya Kiswahili yenye maana tofauti. Neno la kwanza ni "***kisiwa***" ambalo maana yake ni fungu la nchi kavu lililozungukwa na maji pande zote (TUKI, 2014) ,na neno la pili ni "***ndui***" ambalo maana yake ni ugonjwa wa kuambukiza unaofanana na surua (TUKI, 2014), kupitia maneno haya mawili tunapata neno moja ambatano ambalo ni Kisiwandui maana yake ni kisiwa ambacho walikuwa wanawekwa watu ambao wenye ugonjwa wa ndui.Umuhimu wa jina hili katika maendeleo ya lugha ya Kiswahili ni kuwa linatokana na njia ya uambatishaji wa maneno, ambayo ni mojawapo wa njia muhimu za uundaji wa misamiati ya lugha ya Kiswahili. Vilevile jina hili linasaidia katika kukuza misamiati ya lugha ya Kiswahili. Jina hili watu wanapenda libakie hivi hivi na wanalifurahia kwa sababu ni maarufu, la asili na wamelizoea. Katika mtaa wa Kisiwandui kuna majina madogo madogo kama vile Msikiti makuti, msikiti mabati, Makao makuu, na sababu ya kuzuka mitaa hii ni kuwepo vitu halisi na kupata urahisi wa kumfahamisha mtu.

### 4.2.11 Mtaa wa Mwembetanga

Mtaa wa Mwembetanga huu upo katika wilaya ya Mjini Unguja katika mkoa wa Mjini Magharibi. Mtaa huu umepakana na mitaa ya Michenzani, Vikokotoni, Mchangani, Mtendeni, na Darajani (Rejea ramani nambari 2).

#### 4.2.11.1 Asili na Mchakato wa Kuanzishwa Jina la Mwembetanga

Kwa mujibu wa data za mahojiano jina la Mwembetanga lilianzishwa kabla ya mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964. Walioanzisha jina hili ni wenyeji wa eneo

hilo pamoja na wavuvi waliotumia eneo hilo kwa ajili ya ushonaji wa matanga. Inafahamika kuwa kuanzishwa jina hili ni kuwepo kwa mti wa mwembe ambao wavuvi kutoka sehemu mbalimbali walikuwa wanakutana chini yake kwa shughuli za kushona matanga waliyokuwa wanayatumia katika shughuli zao za uvuvi. Katika majibu ya usaili mmoja wa wakaazi wa mtaa huo alitoa ufafanuzi ufuatao:

> Mwembe huo ulikuwa mkubwa na wenye kivuli muruwa. Hivyo, kutokana na kuwepo kwa mwembe huo uliokuwa unatumiwa kwa shughuli za ushonaji wa matanga ndio pakaitwa eneo hilo Mwembetanga."

Data za kushuhudia hazikuweza kupatikanakuthibitisha maelezo haya kwa sababu kwa sasa mwembe huo haupo tena limebakia jina tu.

#### 4.2.11.2 Kigezo cha Uanzilishwaji wa Jina la Mwembetanga

Kigezo kilichotumika kuanzishwa jina hili la Mwembetanga ni kigezo cha kiuchumi, nacho ni hiyo shughuli ya ushonaji matanga kwa ajili ya shughuli za uvuvi, ambazo ndizo zilizowasaidia kupata kipato cha kuwaendeleza katika maisha yao ya kila siku. Matokeo haya yanakubaliana vilevile na yale ya uchunguzi wa Drummond (ameshatajwa) ambaye alibaini kwamba majina ya pahala huweza kurejelea mandhari, maumbile asilia au shughuli zinazofanywa na binaadamu. Mwembe unaorejelewa katika jina hili kwa sasa haupo tena.

#### 4.2.11.3 Umuhimu wa Jina la Mwembetanga Katika Lugha ya Kiswahili

Jina la Mwembetanga linatokana na msamiati wa lugha ya Kiswahili, na linachangia kwa kiwango kikubwa katika kukuza misamiati ya lugha ya Kiswahili, jina hili linatokana na maneno mawili tofauti yenye maana tofauti, neno la mwanzo ni

***"mwembe"*** ambalo maana yake ni mti mkubwa wenye majani marefu na membamba kiasi, magome magumu na unaozaa embe lenye ganda laini, kokwa kubwa nyama laini na tamu linapoiva (TUKI, 2004). Neno la pili ni "***tanga"*** ambalo maana yake ni kitambaa kikubwa kinachozuia kwenye mlingoti wa chombo kama vile jahazi, kuteka upepo na kukiwezesha chombo kwenda (TUKI, 2004). Hivyo kutokana na maneno hayo mawili ukapatikana msamiati mpya Mwembetanga ambapo ni mahala palipokuwa na mwembe uliotumiwa kwa shughuli za ushonaji wa matanga ya ngalawa na wavuvi. Pia jina hili linatokana na njia moja wapo ya uundaji wa maneno ya uambatishaji maneno William (ameshatajwa) anaielezea njia hii kuwa ni moja wapo ya njia za kuita majina ya pahala ambayo inatokana na kuchanganya maneno ambayo ndiyo iliyopelekea kuitwa jina la mtaa huu. Watu wanaoishi eneo hili wanalipenda jina la mtaa huu na wanapenda libakie hivi hivi lisibadilishwe kwa sababu ni jina maarufu, wamelizoea, linawafurahisha kwa kutoa taswira nzuri na ni jina la asili. Kwa sasa mwembe huo haupo na shughuli za kushona matanga pia hazipo tena, imebaki historia tuu.

### 4.2.12 Mtaa wa Kisimamajongoo

Mtaa huu upo katika wilaya ya Mjini Unguja katika mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, na unapakana na mitaa ya Kisiwandui, Gongoni, Michenzani, na Kikwajuni (Rejea ramani nambari 2).

#### 4.2.12.1 Asili na Mchakato wa Kuanzishwa Jina la Kisimamajongoo

Data za mahojiano za watafitiwa zinaeleza kwamba jina la Kisimamajongoo lilianza kutumika kabla ya mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964. Wakaazi wa eneo hili

ndio walioanzisha jina hili la Kisimamajongoo. Mmoja wa watafitiwa wa utafiti huu alikuwa na haya ya kusema:

> ….” sababu ya kuanzishwa jina hili ni kuwepo kwa kisima cha maji ambacho kilikuwa na majongoo yaliyokuwa yanaingia ndani ya kisima hicho, kwa hivyo, kutokana na kuwepo kwa kisima hicho chenye majongoo ndio eneo hilo likaitwa Kisimamajongoo.”

Ushahidi kutokana na uchunguzi makini haukuweza kuthibitisha kuwepo kwa kisima hicho kwa leo. Kwa maelezo ya wakaazi wa eneo hilo kisima hicho hakipo tena hivyo, data za kushuhudia hazikuweza kupatikana (Angalia picha nambari 4).

#### 4.2.12.2 Kigezo cha Uanzilishwaji wa Jina la Kisimamajongoo

Uchanganuzi wa data zilizopatikana zinaonesha kuwa kigezo kilichotumika kuanzishwa jina la Kisimamajongoo ni kigezo cha maumbile, ambapo kisima hicho walikuwa wanaingia majongoo ambayo ni mojawapo wa vitu vya asili vilivyokuwa vinapatikana katika eneo hilo. Matokeo haya yanakubaliana na ufafanuzi wa Lehrer (1992) anaeleza kwamba majina ya mitaa yanakwenda sambamba na maana halisi ya majina yenyewe.

#### 4.2.12.3 Umuhimu wa Jina la Kisimamajongoo Katika Lugha ya Kiswahili

Jina la Kisimamajongoo linatokana na msamiati wa Kiswahili. Jina hili lina umuhimu mkubwa katika lugha ya Kiswahili, kwanza, linachangia kwa kiasi kikubwa katika kukuza misamiati ya lugha ya Kiswahili, jina hili linatokana na mwambatano wa maneno mawili tofauti yenye maana tofauti. Neno la mwanzo ni “***kisima”*** ambayo maana yake ni mahali palipochimbwa na kutoa maji kwa ajili ya matumizi (TUKI, 2014). Neno la pili ni “***majongoo”***, ambalo lina maana ya wadudu

weusi au wa kikahawia wenye miguu mingi sana (TUKI, 2014), hivyo, kutokana na maneno haya mawili tumepata neno moja Kisimamajongoo ambalo lina maana ya mahali ambapo palikuwa na kisima ambacho kina majongoo. Pia umuhimu mwingine jina hili linatokana na njia ya uundaji misamiati ya Kiswahili ya uambatishaji maneno. Vile vile ni jina la pekee kwa sababu hapa Zanzibar hapana sehemu nyingine penye jina hili. Jina hili wakaazi wake wanataka libakie hivi hivi lisibadilishwe kwani wamelizoea, la asili na maarufu.



**Picha Na 4.3: Picha ya Jongoo**

https://encryptetbn1.gstatic.com/images?q (Imepatikana 24.9.2016).

### 4.2.13 Mtaa wa Mfereji wa Wima

Mtaa huu unapatikana katika wilaya ya Mjini Unguja katika mkoa wa Mjini Magharibi. Mtaa wa Mfereji wa Wima unapakana na mitaa ya Mikunguni, Mwembemimba, Kwaalamsha na Mwembeladu. Shughuli muhimu zinazofanyika katika mtaa huu ni biashara.

#### 4.2.13.1 Asili na Mchakato wa Kuanzishwa Jina la Mfereji wa Wima

Kwa mujibu wa data za mahojiano jina la Mfereji wa Wima lilianzishwa kabla ya mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964. Jina la Mfereji wa Wima linatokana na kuwepo kwa mfereji uliokuwa wima ambao ulitumiwa kujaza maji kwenye magari makubwa. Katika mahojiano mkaazi mmoja wa eneo hilo alieleza ifuatavyo:-

> …..” sababu za kuanzishwa jina la mtaa huu ni kuwepo kwa mfereji uliosimama wima kwa lengo la kuyawezesha magari makubwa kuingiza maji kwa urahisi, mfereji huu ni wa serikali, hivyo magari makubwa ya maji yalitumia mfereji huu kuingizia maji na kuyasambaza sehemu mbalimbali za mji. Kutokana na kuwepo kwa mfereji huo uliosimama wima katika eneo hilo ndipo pakaitwa Mfereji wa Wima”.

Uchunguzi makini uliofanywa wakati wa utafiti huu umethibitisha kuwa mfereji ulioanzisha jina hilo ungalipo hadi leo lakini hautumiki tena kwa shughuli za kuingizia maji magari makubwa wala kwa shughuli zozote zile.



**Picha Na 4.4: Mtaa wa Mfereji wa Wima**

Chanzo: Mtafiti, 2016

#### 4.2.13.2 Kigezo cha Uanzilishwaji wa Jina la Mfereji wa wima

Kigezo kilichotumika kuanzishwa jina hili ni cha kijamii, kwa sababu huduma ya maji inahitajika na kila mtu katika jamii na ni muhimu, hivyo baada ya serikali kuona

kuwa kuna upungufu wa maji katika maeneo mbalimbali ndio ikatengeneza mfereji huu ili kuwasaidia wananchi wake kwa kuwasambazia maji kwa kutumia magari makubwa. Kigezo cha kijamii kuwa ni msingi wa kutolea jina la pahala, kimejadiliwa pia na Arthur (ameshatajwa) ambaye alieleza kuwa kazi ya pahala na shughuli za kijamii kama kazi za shamba au umbile asilia huweza kuwa chimbuko la jina la pahala.

#### 4.2.13.3 Umuhimu wa Jina la Mfereji wa Wima Katika Lugha ya Kiswahili

Jina la Mfereji wa Wima linatokana na mwambatano wa maneno matatu tofauti yenye maana tofauti. Neno la mwanzo ni "***mfereji"*** ambalo maana yake ni kipande cha mwanzi, plastiki au chuma chenye uwazi ndani kinachotumika kupeleka maji kama vile majumbani (TUKI, 2004). Jina la pili ni "***wima"*** ambalo maana yake ni kwa kusimama au kunyooka kwenda juu ( TUKI,2004), na "***wa***" ni kiunganishi ambacho kinaunganisha majina haya mawili. Hivyo, umuhimu mwingine ni kuwa jina hili linatokana na njia moja wapo ya uundaji wa maneno ya uambatishaji maneno. Pia jina hili linadumisha matumizi ya lugha ya Kiswahili, kwa sababu linapoendelea kutumika linafanya maneno haya yasisahaulike kama yanavyosahaulika baadhi ya misamiati ya lugha ya Kiswahili.

### 4.2.14 Mtaa wa Mfenesi Mazizi

Mtaa wa Mfenesi mazizi upo katika wilaya ya Mjini Unguja, katika mkoa wa Mjini Magharibi, mtaa huu umepakana na mitaa ya Kwa Haji Tumbo, Gulioni, Mbuyu pacha, Mwembeladu na Mitiulaya. Shughuli kubwa ya wakaazi wa mtaa huu ni kufanya biashara mbalimbali.

#### 4.2.14.1 Asili na Mchakato wa Kuanzishwa Jina la Mfenesimazizi

Kwa mujibu wa data za mahojiano zilizopatikana kwa njia ya mahojiano jina la mtaa huu lilianzishwa tangu enzi za ukoloni yaani kabla ya mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964.Wakaazi wa eneo hili ndio walioanzisha jina hili, jina lenyewe linatokana na upotoshaji wa matamshi wa neno la Kiswahili ***"mizizi"*** na kutamkwa mazizi. Kwa sababu ambazo wakaazi wa mtaa huu hawakuwa na maelezo yanayokubaliana, neno mizizi lilibadilishwa kimatamshi na kuwa mazizi. Mkaazi mmoja wa eneo hilo alieleza kuwa:

> "katika eneo hili kulikuwa na mfenesi ambao ulikuwa upo kwa muda mrefu yaani miaka kadhaa, mfenesi huo ulikuwa na mizizi ambayo ilikuwa imetokeza juu ya ardhi, wenyeji wa eneo hili walikuwa na kawaida ya kukaa juu ya mizizi hiyo na kufanya mazungumzo yao mbalimbali."



**Picha Na 4.5: Mtaa wa Mfenesi Mazizi**

Chanzo: Mtafiti 2016

Kutokana na huo mfenesi kuwa hivyo wakaazi wenyewe kwa mujibu wa maelezo yao wakaamua kuuita mfenesi mazizi ingawa mfenesi huo ulikuwa na miaka mingi, hivyo ulianguka na kutokana na kutaka kulienzi na kulitunza jina hilo la Mfenesimazizi wamepanda mfenesi mwingine katika sehemu ambayo ulikuwepo

mfenesi wa mwanzo ili jina hilo lisisahaulike liendelee kutumika. Matokeo haya yanathibitisha maelezo ya Nieminen (ameshatajwa), ambaye katika utafiti wake alibaini kuwa wakaazi wa asili wa Quebec wanayaenzi majina ya mitaa yao kama ni sehemu muhimu ya matukio mbalimbali ya kimazingira, kihistoria na kiutamaduni. Hivi ndivyo walivyofanya wakaazi wa mtaa wa Mfenesimazizi.

#### 4.2.14.2 Kigezo cha Uanzilishwaji wa Jina la Mfenesimazizi

Kigezo cha chimbuko la jina la Mfenesimazizi ni maumbile ya eneo husika. Hali ya kuwepo kwa mfenesi wenye mizizi mikubwa kuliwafanya wakaazi wa eneo hili kuanzisha au kutoa jina hili la Mfenesimazizi. Mfenesi wenye mizizi ni maumbile asilia, ambacho wakaazi walikitumia kama kigezo cha msingi wa kutoa jina la mtaa huo.

#### 4.2.14.3 Umuhimu wa Jina la Mfenesi mazizi Katika Lugha ya Kiswahili

Jina la Mfenesimazizi linatokana na msamiati wa Kiswahili, Jina hili lina umuhimukatika lugha ya Kiswahili.Umuhimu wa kwanza wa jina hili ni kuwa, linakuza misamiati ya lugha ya Kiswahili. Neno Mfenesimazizi linatokana na maneno mawili tofauti ambayo yana maana tofauti. Neno la kwanza ni "***mfenesi"*** ambalo maana yake ni mti mkubwa wenye majani yaliyochongoka nchani, matawi yanayoelekea juu na huzaa matunda makubwa yenye ganda la rangi ya kijani na vidutudutu (TUKI, 2014), neno la pili ni "***mazizi"*** ambalo maana yake ni sehemu ya mmea iliyo ardhini ambayo huvuta maji, madini na vitu vyote vinavyohitajika na mmea kutoka ardhini kwa ajili ya maisha yake. (TUKI, 2014). Umuhimu mwingine wa jina hili ni kuwa linatokana na moja ya njia za uundaji wa misamiati ya Kiswahili

ya uambatishaji maneno. Vile vile jina hili la Mfenesimazizi linadumisha matumizi ya lugha ya Kiswahili kwani maneno hayo mawili yataendelea kutumiwa na hayatosahaulika kama baadhi ya maneno ya lugha ya Kiswahili yanavyopotea na kusahauliwa. Jina la mtaa huu linatambulikana na wengi, na watu wanapenda libakie hivi hivi kwani ni jina la asili, maarufu, limezoeleka na wengi na vile vile linawafurahisha kwa kutoa taswira nzuri wanapolisikia.

#### 4.2.15 Mtaa wa Mikunguni

Mtaa wa Mikunguni upo katika wilaya ya Mjini Unguja katika mkoa wa Mjini Magharibi, mtaa huu umepakana na mitaa ya Mfereji wa wima, Mkele, Amani, na Kibanda maiti. Wakaazi wa eneo hili shughuli yao kubwa ni biashara. Pia katika mtaa huo kuna soko maarufu linaitwa "soko la mapinduzi" linalotumiwa na wakaazi hao kuuza na kununua bidhaa mbalimbali.

##### 4.2.15.1 Asili na Mchakato wa Kuanzishwa Jina la Mikunguni

Data zilizotokana na mahojiano zinaonesha kwamba jina la Mikunguni lilianzishwa kabla ya mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964. Jina la mtaa huu lilianzishwa na wenyeji yaani wakaazi wa mtaa huo kubainisha hali ya wingi wa miti ya mikungu ambayo ilikuwa kwa wingi kwenye eneo hilo. Katika mahojiano ya mmoja wa watafitiwa wa utafiti, mhusika huyo alieleza ifuatavyo:-

> "Jina la Mikunguni limetokana na kuwepo miti mingi ni kuwepo kwa miti aina ya mikungu pembezoni mwa barabara katika eneo hilo ambayo ilikuwa ni mingi sana hapo zamani. Ni kutokana na wingi wa miti hiyo katika eneo hilo ndipo likaitwa Mikunguni".

Uchunguzi makini uliofanyika kwenye mtaa huu umeonesha kuwa kwa sasa mikungu hiyo haipo tena lakini jina bado lipo.

#### 4.2.15.2 Kigezo cha Uanzilishwaji wa Jina la Mikunguni

Kigezo kilichotumika kuanzishwa kwa jina hili ni kigezo cha kimaumbile, ambapo neno mikunguni linaakisi miti iliyoota yenyewe katika mazingira ya eneo hilo.

#### 4.2.15.3 Umuhimu wa Jina la Mikunguni Katika Lugha ya Kiswahili

Jina la Mikunguni ni msamiati wa Kiswahili, jina hili linatokana na neno "***mkungu***" ambayo maana yake ni mti unaozaa kungu ambazo ndani ya kokwa zake mna kiini (TUKI, 2004), na mofimu –***"ni"*** ya pahala. Hivyo, umuhimu wa mwanzo wa jina hili ni kuwa linatokana na matumizi ya njia moja wapo ya uundaji wa misamiati ya lugha Kiswahili yaani unyambuaji. Umuhimu wa pili wa kutumia jina mikunguni ni kuwa linakuza lugha ya Kiswahili na kudumisha matumizi yake lugha ya Kiswahili, kwa sababu hulifanya neno hili liendelee kutumika na lisisahaulike. Wakaazi wa mtaa huu wanalipenda jina hili la Mikunguni na wanapenda libakie hivi hivi kwa sababu linawafurahisha, wamelizoea na ni maarufu. Mitaa midogo midogo iliyomo katika eneo hili ni Mikunguni Utapoa, Mikunguni kwa Bachoo, Mikunguni sheli, Mikunguni kwa Juma Pweza, Mikunguni sokoni, mitaa hii midogo midogo imezuka kutokana na kuwepo vitu halisi kama soko, sheli na kuwepo kwa watu maarufu kama Bachoo na Juma Pweza katika eneo hilo.

### 4.2.16 Mtaa wa Kaburi Kikombe

Mtaa wa Kaburikikombe upo wilaya ya Mjini Unguja katika mkoa wa Mjini Magharibi Unguja. Mitaa iliyopakana na mtaa huu ni pamoja na mtaa wa Migombani, Jang'ombe na Mpendae.

#### 4.2.16.1 Asili na Mchakato wa Kuanzishwa Jina la Kaburikikombe

Data za mahojiano zinaonesha kuwa jina la mtaa huu lilianza kutumiwa kabla ya mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964. Jina hili lilianzishwa na wenyeji wa eneo hili kwa kuwepo kaburi lenye kikombe, kaburi hilo alizikwa mwanamke mmoja aliyefariki muda mfupi baada ya arusi yake na kuzikwa katika eneo hilo. Kutokana na huzuni waliyokuwa nayo ndugu zake waliamua kuweka juu ya kaburi lake baadhi ya mali alizopewa marehemu huyo siku ya arusi yake. Mojawapo wa mali hizo ilikuwa ni vikombe; hivyo kuwafanya wapita njia kulitambua kaburi hilo kama kaburi kikombe, baadae eneo au mtaa wote uliokuwapo kaburi hilo ukaitwa kwa jina hilo. Mmoja wa wakaazi wa mtaa wa Kaburi kikombe akichangia katika mahojiano alieleza yafuatayo:

> “Kuanzishwa kwa jina hili ni kutokana na kuwepo kwa kaburi lenye kikombe ambalo alizikwa mwanamke aliyeolewa…….muda mfupi tu baada ya kuolewa na kupelekwa kwa mumewe alifariki dunia….. ndipo akazikwa katika kaburi hilo na kuwekewa kikombe cha kaure juu ya kaburi lake ambacho ni miongoni mwa vitu alivyopewa biharusi huyo kwa ajili ya matumizi ya nyumbani kwake”.

Taarifa zaidi za mapokeo zinaeleza kuwa hili kaburi ni la miaka mingi sana kwa sasa hapana hata alama yake kwa sababu watu wamejenga katika eneo hilo na kuondoa kila kitu. Inaelezwa pia na wakaazi wa mtaa huo kuwa watu mbali mbali walikuwa wanakwenda katika eneo hilo na kuomba maombi yao mbalimbali wengine wanavunja mayai katika eneo hilo la kaburi, wingine wanaweka vichupa ambavyo ndani yake mna vitu vya ajabu, wingine wanatupa hela katika kaburi hilo, mambo ambayo yanawapelekea wakaazi wa eneo hili kusita kuwaonesha watu ambao wanataka kuliona kaburi hilo kwa sababu wingine wanafanya mambo ya kishirikina. Matokeo haya yanathibitisha ugunduzi wa Helleland (ameshatajwa)

kuwa matukio muhimu ya kihistoria au kijamii yanaweza kuwa ni vyanzo vya kutolea majina ya pahala, vilevile yanahifadhi kumbukumbu muhimu za historia na matukio yaliyopita.

#### 4.2.16.2 Kigezo cha Uanzilishwaji wa Jina la Kaburikikombe

Kigezo kilichotumika kuanzishwa kwa jina hili ni kigezo cha maumbile, ambapo palikuwa na kaburi lililowekwa kikombe juu yake, jambo ambalo liliwastaajabisha wengi na kupelekea kupaita hapo jina hilo.

#### 4.2.16.3 Umuhimu wa Jina la Kaburi kikombe Katika Lugha ya Kiswahili

Jina la Kaburi kikombe ni msamiati wa Kiswahili. Jina hili linatokana na maneno mawili tofauti yenye maana tofauti na kupata neno jipya. Neno la mwanzo ni "***kaburi"*** ambalo maana yake ni shimo la kuzikia maiti linalochimbwa kwa kipimo maalumu (TUKI, 2014). Na neno la pili ni "***kikombe***" ambalo maana yake ni chombo cha kauri, chuma, madini n.k kitumiwacho kwa kunywea vitu vya majimaji (TUKI, 2014). Hivyo umuhimu wa mwanzo wa jina hili ni kuwa linajengwa na maneno hayo msamiati wa Kiswahili. Kwa njia hii msamiati wa Kiswahili umekuwa kutokana na kutohoa neno moja jipya kaburikikombe ambalo maana yake ni mahala ambapo palikuwa na kaburi ambalo juu yake limewekwa vikombe. Umuhimu wa pili linadumisha matumizi ya lugha ya Kiswahili kwa kufanya maneno haya yaendelee kutumika yasisahaulike. Umuhimu wa tatu wa jina la Kaburikikombe ni jina la pekee katika misamiati ya majina ya mitaa hapa Zanzibar. Jina hili la Kaburi kikombe wakaazi wake wanalipenda sana, na wanalipenda libakie hivi hivi, kwani linawafurahisha, limezoeleka maarufu na la asili.

### 4.2.17 Mtaa Wa Mwembebeni

Mtaa wa Mwembebeni huu upo katika wilaya ya Mjini Unguja katika mkoa wa Mjini Magharibi Unguja. Mtaa huu umepakana na mitaa ya Mikunguni, Mwembe njugu na Muungano. Wakaazi wa mtaa huu hujishughulisha zaidi na kufanya biashara mbalimbali ndogondogo.

#### 4.2.17.1 Asili na Mchakato wa Kuanzishwa Jina la Mwembebeni

Kwa mujibu wa data zilizopatikana kwa njia ya mahojiano na dodoso jina hili la Mwembebeni lilianzishwa kabla ya mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964. Jina hili lilianzishwa na wenyeji wanaoishi eneo hilo kuelezea shughuli ya kijamii iliyokuwa ikifanyika chini ya mwembe mmoja uliokuwepo kwenye eneo hilo. Kwa mujibu wa maelezo ya watafitiwa, shughuli hiyo ya ngoma ya beni likuwa ikifanyika wakati wa sherehe au matukio mbalimbali ya kijamii katika eneo hilo. Mmoja wa watafitiwa akishiriki katika usaili alikuwa na haya ya kueleza:

> "Sababu ya kuitwa jina hili ni kuwepo kwa mwembe ambao watu kutoka sehemu mbali mbali za mjini walikuja kupiga beni wanapokuwa na shughuli hasa za harusi. Ngoma hiyo ya beni ilikuwa inapigwa wakati wa usiku mpaka karibu na alfajiri, kutokana na hali hiyo ndio watu wanaoishi eneo hilo wakapaita Mwembebeni"

Langford (2013), anaeleza kwamba baadhi ya majina ya mitaa huashiria maumbile au harakati za kijamii, za kisiasa zilizopata kutokea katika eneo fulani na kupelekea kuitwa majina ya maeneo hayo. Matukio au vitu hivi vilikuwa muhimu sana kwa eneo husika na vikaathiri sana maisha yao.

#### 4.2.17.2 Kigezo cha Uanzilishwaji wa Jina la Mwembebeni

Kigezo kilichotumika kuanzishwa jina la Mwembebeni ni kigezo cha shughuli za

kijamii, ambapo jina husika linatokana na shughuli maalumu ya kijamii iliyokuwa inatendeka katika eneo hilo. Sherehe zinazoambatana na kupiga ngoma ni sehemu muhimu ya mfumo wa maisha na desturi za waswahili tangu zamani.

#### 4.2.17.3 Umuhimu wa Jina la Mwembebeni katika Lugha ya Kiswahili

Jina la Mwembebeni ni msamiati wa Kiswahili. Jina hili la Mwembebeni linatokana na mwambatano wa maneno mawili tofauti yenye maana tofauti. Neno la mwanzo ni "***mwembe***" ambapo maana yake ni mti mkubwa wenye majani marefu na membamba kiasi, magome magumu na unazaa embe lenye ganda laini, kokwa moja, nyama laini na tamu linapoiva (TUKI, 2004). Na neno la pili ni "***beni***" ambalo maana yake ni ngoma inayopigwa Unguja wakati wa harusi au sherehe na wachezaji wakicheza kwa kuzunguka mduara (TUKI, 2004). Hivyo, umuhimu wa jina hili unatokana na maneno haya mawili tofauti tunapata neno moja Mwembebeni ambalo maana yake ni pahali ambapo watu walikuwa wanapatumia kwa kupiga ngoma ya beni wakati wa usiku.

Hivyo umuhimu wa jina hili unatokana na njia muhimu ya uundaji wa misamiati ya lugha ya Kiswahili iliyotumika katika kuanzisha jina hili; njia ya uambatishaji maneno. Vile vile matumizi ya jina hili yanaendeleza na yanadumisha matumizi ya lugha ya Kiswahili, kwa sababu linafanya neno hili lisisahaulike na liendelee kutumika na wakaazi wa eneo hili. Wakaazi wa mtaa huo wanapenda jina la Mwembebeni libakie hivi hivi kwani linawafurahisha, wamelizoea, maarufu na jina la asili.

### 4.2.18 Mtaa wa Mwembenjugu

Mtaa wa Mwembenjugu unapatikana katika wilaya ya Mjini Unguja katika mkoa wa Mjini Magharibi Unguja. Mtaa huu umepakana na mitaa ya Mwembebeni, Mwembematarumbeta, Kwa Alamsha, Kidongo chekundu na Muungano. Wakaazi wa mtaa huu hujishughulisha na biashara ndogondogo. Mitaa midogo midogo iliyomo katika mtaa wa Mwembenjugu ni pamoja na Jaani, Mharitani, Changongo nk.

#### 4.2.18.1 Asili na Mchakato wa Kuanzishwa Jina la Mwembenjugu

Matokeo ya data za mahojiano na dodoso zinaonesha kuwa jina hili la Mwembenjugu lilianzishwa kabla ya mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964. Nalo lilianzishwa na wenyeji walioishi eneo hili kuelezea shughuli ya kibiashara iliyokuwa ikifanyika kwenye eneo hilo. Jina Mwembenjugu linaakisi maisha ya jamii na shughuli walizofanya kwenye eneo hilo.Mmoja wa watafitiwa wa utafiti huu alieleza ifuatavyo katika majadiliano:-

> "Sababu ya kuanzishwa jina hili ni palikuwa na mwembe ambao watu walikuwa wanakaa wanasubiriana kwa lengo la kwenda mashamba, alikuwepo mtu anauza njugu katika eneo hili, hivyo watu waliokuwa wanafika eneo hilo la mwembe huo wananunua njugu hizo, watu wakapaita eneo hili Mwembenjugu."



**Picha Na 4.6: Mtaa wa Mwembenjugu**

Chanzo: Mtafiti, 2016

Ushahidi wa uchunguzi makini ulionesha kuwa mwembe huo wa asili ulioanzisha jina hilo haupo tena, lakini wakaazi wa eneo hili wamepanda mwembe mwingine katika eneo hilo ili kuweka kumbukumbu na kutunza jina la asili katika eneo hili.

#### 4.2.18.2 Kigezo cha Uanzilishwaji wa Jina la Mwembenjugu

Kigezo kilichotumika kuanzishwa kwa jina la Mwembenjugu ni kigezo cha kiuchumi, kutokana na uuzwaji wa njugu ambazo zilimsaidia muuzaji kupata kipato kwa ajili ya kukidhi mahitaji yake mbali mbali ya kimaisha. Matokeo haya yanashabihiana na uchunguzi wa Langford (2013) uliioonesha kwamba baadhi ya majina ya mitaa huashiria harakati za kijamii zilizopata kutokea katika eneo f ulani na kupelekea kuitwa majina ya maeneo hayo.

#### 4.2.18.3 Umuhimu wa Jina la Mwembenjugu Katika Lugha ya Kiswahili

Jina hili la Mwembenjugu ni msamiati wa Kiswahili. Jina la Mwembenjugu linatokana na muunganiko wa maneno mawili tofauti yenye maana tofauti. Neno la mwanzo ni "***mwembe"*** ambalo maana yake ni mti mkubwa wenye majani marefu na membamba kiasi, magome magumu na unazaa embe lenye ganda laini, kokwa moja, nyama laini na tamu linapoiva (TUKI, 2014).Neno la pili ni "***njugu"*** ambalo maana yake ni punje ngumu za mviringo yaani karanga (TUKI, 2014). Hivyo, umuhimu wa mwanzo wa jina hili ni unatokana na maneno haya mawili tunapata neno jengine moja Mwembenjugu ambayo maana yake ni pahala ambapo palikuwa panauzwa njugu. Vile vile jina hili linatokana na moja ya njia za uundaji wa misamiati ya lugha ya Kiswahili ya uambatishaji maneno. Pia linadumisha matumizi ya neno hili katika lugha ya Kiswahili na kusababisha jina hili lisisahaulike na liendelee kutumika.

### 4.2.19 Mtaa wa Mwembemadema

Mtaa wa Mwembemadema upo katika wilaya ya Mjini Unguja katika mkoa wa Mjini Magharibi Unguja. Mtaa huu umepakana na mitaa ya Kilimani, Michenzani, Miembeni, Kikwajuni na Mpirani.

#### 4.2.19.1 Asili na Mchakato wa Kuanzishwa Jina la Mwembemadema

Data zilizotokana na mahojiano zinaonesha kuwa jina hili la Mwembemadema lilianzishwa kabla ya mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964. Jina la Mwembemadema lilianzishwa na wavuvi ambao walikuwa wakilitumia eneo hili kwa shughuli za kutengeneza zana zao za uvuvi. Kutokana na kuwa zana muhimu iliyotumika na wavuvi wa enzi hizo kuwa ni madema, basi wenyeji wakatokea kuiita sehemu waliyoitumia kwa kazi hiyo kuwa mwembemadema, na baadae utambulisho wa eneo ulihusisha maeneo jirani kuwa yote yakaitwa kwa jina hilo.Mmoja wa wakaazi wa eneo hilo alifafanua uanzishwaji kwa kusema:

> “kulikuwa na mwembe ambao wavuvi kutoka sehemu mbali mbali walikuwa wanakaa kwa lengo la kusuka madema yao kwenye mwembe huo. Kwa sasa mwembe huo haupo tena ila pana jengo ambalo lilikuwa linaitwa makao makuu ya wavuvi ambapo walikuwa wanalitumia wavuvi hao baada ya kuyasuka madema yao kuyaweka, jengo hili kwa sasa linaitwa Tanzania Youth Icon (TAYI).”

#### 4.2.19.2 Kigezo cha Uanzilishwaji wa Jina la Mwembemadema

Kigezo kilichotumika kuanzishwa kwa jina hili ni kigezo cha shughuli za kiuchumi, ambapo usukaji wa madema kwenye mwembe huo ni shughuli ambayo waliifanya wavuvi ili kuwasaidia kupata  mahitaji yao mbali mbali ya kimaisha.

#### 4.2.19.3 Umuhimu wa Jina la Mwembemadema Katika Lugha ya Kiswahili

Jina la Mwembemadema linatokana na mwambatano wa maneno mawili tofauti

yenye maana tofauti. Neno la mwanzo ni “***mwembe”*** ambalo maana yake ni mti mkubwa wenye majani marefu na membamba kiasi, magome magumu na unazaa embe yenye ganda laini, kokwa moja, nyama laini na tamu linapoiva (TUKI, 2014). Neno la pili ni ‘***madema”*** ambalo maana yake ni mitego ya samaki iliyofumwa kwa vijiti (TUKI, 2014), (angalia picha nambari 8 kwenye viambatanisho). Hivyo, umuhimu wa jina hili kwanza unatokana na maneno haya mawili tunapata neno moja Mwembemadema ambalo maana yake ni mahala ambapo palikuwa na mwembe watu walikuwa wanasuka madema kwa ajili ya uvuvi. Pia, linatokana na moja ya njia ya uundaji wa misamiati ya Kiswahili ya uambatishaji maneno.Vile vile kuendelea kwa matumizi ya neno hili kunafanya lidumu na lisisahaulike.



**Picha Na 4.7: Picha ya Dema**

Chanzo: https://encrypted-tbn2.gstatic.com/images?q=tbn: (Imepatikana 24.9.2016).

### 4.2.20 Mtaa wa Mwembemimba

Mtaa wa Mwembemimba upo katika wilaya ya Mjini Unguja katika mkoa wa Mjini Magharibi. Mtaa huu unapakana na mitaa ya Mwembeladu, Makadara, Mfereji wa wima, na Miti ulaya,

#### 4.2.20.1 Asili na Mchakato wa Kuanzishwa Jina la Mwembemimba

Kutokana na data za mahojiano na dodoso ambazo zimepatikana zinaonesha kuwa jina la mtaa wa Mwembemimba lilianzishwa kabla ya mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964. Jina la mtaa huu lilianzishwa na wenyeji yaani wakaazi wa wa mtaa huo.Mmoja wa watoa taarifa hizo anasema kuwa:

> ”sababu za kuanzishwa jina la mtaa huo ni kuwepo kwa mwembe ambao kulikuwa na bibi anaitwa Mwanajuma Kassim alikuwa anakaa chini ya mwembe huo kuuza na kutoa dawa kwa wale ambao hawajapata watoto, na wengi ambao waliotumia dawa za bibi huyu walifanikiwa kupata ujauzito na watoto, watu kutoka sehemu mbalimbali walikuwa wanakwenda katika mwembe huo ili kupata dawa za bibi huyu. Kutokana na sababu hiyo ndio pakaitwa Mwembemimba”.

Mtoa taarifa mwingine alitoa maelezo yanayofanana na hayo ingawa yanatofautiana kidogo akielezea sababu ya mtaa huu kuitwa Mwembemimba alieleza ifuatavyo:

> ”Katika eneo hili kuna hospitali ya wazazi, na nje ya hospitali hiyo kulikuwa na mwembe, hivyo, wajawazito kutoka sehemu mbalimbali waliokuwa wanakwenda hospitalini hapo kwa ajili ya huduma walikuwa wanakaa kwenye mwembe huo kusubiri huduma na kupumzika, hivyo eneo hilo ndio likaitwa Mwembemimba”.

Ushahidi wa uchunguzi makini unaonesha kuwa mwembe huu haupo tena, ila kwa mujibu wa maelezo ya wakaazi wa eneo hilo mwembe huo ulikuwa pembeni mwa hospitali ya wazazi ya Mwembeladu.

#### 4.2.20.2 Kigezo cha Uanzilishwaji wa Jina la Mwembemimba

Kigezo kilichotumika kuanzishwa jina la Mwembemimba ni kigezo cha kijamii ambapo akinamama walikuwa wanakwenda eneo hilo kwa ajili ya kupata tiba kwa wale ambao hawajapata watoto au wale wajawazito kwa ajili ya matibabu.

#### 4.2.20.3 Umuhimu wa Jina la Mwembemimba Katika Lugha ya Kiswahili

Jina hili linatokana na muunganiko wa maneno mawili tofauti yenye maana tofauti. Neno la mwanzo ni "***mwembe"*** ambalo maana yake ni mti mkubwa wenye majani marefu na membamba kiasi, magome magumu na unazaa embe lenye ganda laini, kokwa moja, nyama laini na tamu linapoiva (TUKI, 2014). Neno la pili ni "***mimba"*** ambayo maana yake ni utungo wa mwanzo wa binaadamu au mnyama katika tumbo la mama (TUKI, 2014). Hivyo, umuhimu wa mwanzo unatokana na maneno haya mawili tunapata jina jingine Mwembemimba ambalo maana yake ni pahala palipokuwa na mwembe uliokuwa unatumika kutoa dawa ili kupata ujauzito kwa wale wenye tatizo la kupata ujauzito au ni eneo ambalo wajawazito walikuwa wanakaa kusubiri huduma na kupumzika. Pia jina hili linatokana na moja ya njia ya uundaji wa misamiati ya lugha ya Kiswahili ya uambatishaji maneno.Vile vile, kuendelea kwa matumizi ya jina hili kunafanya neno hili lisisahaulike. Jina hili wakaazi wake wanalipenda na wanataka libakie hivi hivi lisibadilishwe kwa sababu ni jina la asili, wamelizoea na maarufu.

### 4.2.21 Mtaa wa Shauri Moyo

Mtaa wa Shaurimoyo upo katika wilaya ya Mjini Unguja katika mkoa wa Mjini Magharibi. Mtaa huu umepakana na mitaa ya Saateni, Ziwatuwe, Makadara na Mkele.

### 4.2.21.1 Asili na Mchakato wa Kuanzishwa Jina la Shaurimoyo

Kutokana na data za mahojiano na dodoso jina hili la Shaurimoyo lilianzishwa kabla ya mapinduzi ya Zanzibar.ya mwaka 1964. Jina la Shaurimoyo lilianzishwa na wakaazi wa eneo hili. Mkaazi mmoja wa eneo hilo anasema kwamba;

> ”katika eneo hili hapo zamani watu walikuwa hawaishi na kulikuwa na msitu tu, hivyo ikifika jioni kiza kinakuwa kinaanza kuingia katika eneo hilo jambo ambalo watu liliwatia hofu na wasi wasi kwenda katika eneo hilo, mtu akitaka kwenda anaambiwa aushauri moyo kwanza kabla ya kwenda huko, ikawa ndio sababu ya kuitwa jina hilo la Shaurimoyo.”

Ushahidi wa uchunguzi makini unaonesha kwamba msitu huo haupo tena watu wamejenga na wanakaa katika eneo hilo na limebakia jina tu.

### 4.2.21.2 Kigezo cha Uanzilishwaji wa Jina la Shaurimoyo

Kigezo kilichotumika kuitwa jina hili ni kigezo cha maumbile, kutokana na eneo hilo kuwa na msitu uliowatia watu hofu na wasi wasi kufika katika eneo hili. Matokeo haya yanakubaliana na maelezo ya Helleland na wenzake (wameshatajwa) wanafafanua kuwa ikiwa jina la pahala linaleta hisia chanya basi mtumiaji atakuwa na furaha na ikiwa jina la pahala linaleta hisia hasi basi mtumiaji atakuwa na huzuni na ataliepuka.

### 4.2.21.3 Umuhimu wa Jina la Shauri moyo Katika Lugha ya Kiswahili

Jina hili la Shaurimoyo linatokana na muunganiko wa maneno mawili tofauti yenye maana tofauti. Neno la mwanzo ni “***shaur***i” ambalo maana yake ni rai au nasaha (TUKI,2004), na neno la pili ni “***moyo”*** ambalo maana yake ni kiungo cha mwili kilicho sehemu ya kati ya kifua na mapafu ambacho husukuma damu ili ienee

mwilini kwa kupitia kwenye mishipa (TUKI, 2004) .Umuhimu wa mwanzo wa jina hili unatokana na maneno hayo mawili tunapata jina jingine Shaurimoyo ambapo ni mahala palipokuwa na msitu mkubwa ambao watu walikuwa hawaishi eneo hilo wala kwenda kutokana na kuwa na wasi wasi na hofu na eneo hilo. Pia linatokana na njia moja wapo ya uundaji wa misamiati ya lugha ya Kiswahili ya uambatishaji maneno.Vilevile kuendelea kwa matumizi ya jina hili kunafanya lisisahaulike. Wakaazi wa eneo hili wanalipenda jina hili na wanataka libakie hivi hivi lisibadilishwe kwa sababu wamelizoea.

### 4.2.22 Mtaa wa Mlandege

Mtaa wa Mlandege upo katika wilaya ya Mjini Unguja katika mkoa wa Mjini Magharibi. Mtaa huu unapakana na mitaa ya Barastekipande, Kwa Haji tumbo, Mchangani na Mfereji maringo. Katika eneo hili kuna maduka mengi hivyo, shughuli kubwa ya wakaazi wa mtaa huu ni biashara (Rejea ramani nambari 2 kwenye viambatanisho).

#### 4.2.22.1 Asili na Mchakato wa Kuanzishwa Jina la Mlandege

Kutokana na data za mahojiano na dodoso jina la mtaa huu lilianzishwa kabla ya mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964. Jina la Mlandege lilianzishwa na wakaazi wenyewe wa eneo hili kutokana na kuwepo kwa mti wa mlandege katika eneo hilo. Mmoja wa watafitiwa wa utafiti huu anatoa ufafanuzi ufuatao:

> “katika eneo hilo palikuwa na miti mingi, miongoni mwa miti hiyo mmoja wapo ni huo mlandege, ambapo mti huu ulikuwa una maua ya rangi ya manjano na ndani ya maua hayo mna tunda ambazo ndege walikuwa wanapenda kula. Kutokana na kuwepo kwa mti huu katika eneo hilo ndio pakaitwa Mlandege”

Ushahidi wa uchunguzi makini unaonesha kwamba mti huu haupo tena limebakia jina tu.

#### 4.2.22.2 Kigezo cha Uanzilishwaji wa Jina la Mlandege

Kigezo kilichotumika kuanzishwa jina hili ni kigezo cha maumbile asilia ambapo mti huu haukupandwa ila wameukuta tu wakaazi wa eneo hili.

#### 4.2.22.3 Umuhimu wa Jina la Mlandege Katika Lugha ya Kiswahili

Mlandege ni mmea wenye matawi laini na majani laini ya umbo la duaradufu na maua ya manjano unaota kwenye matawi ya mti mwingine (TUKI, 2014). Jina hili linatokana na maneno mawili tofauti yenye maana tofauti. Neno la mwanzo ni ***"mla***" ambalo maana yake ni mtu au mnyama mwenye tabia ya kula kitu fulani (TUKI, 2014). Na neno la pili ni ***"ndege"*** maana yake ni kiumbe mwenye mabawa na manyoya ambaye aghalabu huruka angani. Umuhimu wa mwanzo wa jina hili katika lugha ya Kiswahili unatokana na maneno haya mawili tunapata neno jingine ambalo ni Mlandege maana yake ni kama ilivyoelezwa hapo juu . Umuhimu mwingine jina hili linatokana na moja wapo ya njia za uundaji wa misamiati ya Kiswahili ya uambatishaji maneno. Vile vile kuendelea kwa matumizi ya jina hili kunafanya liendelee na lisisahaulike. Jina hili linatambulikana na wengi na wenyeji wa mtaa huu wanalipenda sana na wanataka libakie hivi hivi lisibadilishwe kwa sababu wamelizoea na jina la asili.

### 4.2.23 Mtaa wa Kwa Hajitumbo

Mtaa wa Kwa Haji tumbo upo katika wilaya ya Mjini Unguja katika mkoa wa Mjini Magharibi Unguja. Mtaa huu umepakana na mitaa ya Mlandege, Kwa Bizredi,

Mfenesimazizi, Mferejimaringo na Mwembeladu. Wakaazi wa mtaa huu wanajishughulisha na shughuli za biashara mbalimbali.

#### 4.2.23.1 Asili na Mchakato wa Kuanzishwa Jina la Kwa Hajitumbo

Kwa mujibu wa data za mahojiano za watafitiwa inaonesha kuwa jina la Kwa Haji tumbo lilianzishwa kabla ya mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964. Jina hili lilianzishwa na wakaazi wa eneo hilo kutokana na kuwa hapo zamani aliishi mtu mmoja ambaye alikuwa mfanyabiashara wa dawa za kienyeji katika eneo hilo aliyeitwa Haji. Mkaazi mmoja wa eneo hilo alikuwa na haya ya kueleza:

> …..” katika eneo hili alikuwepo mtu mwenye asili ya kihindi alikuwa anaishi hapo, mtu huyo aliitwa Haji ambae alikuwa na tumbo kubwa, kazi yake ilikuwa ni kuuza dawa za kienyeji katika duka lake, hivyo watu walikuwa wanakwenda kwa mtu huyu kununua bidhaa hizo, jambo ambalo lilimpatia umaarufu mkubwa na watu wengi wakawa wanamfahamu kutokana na kazi yake hiyo na ndiyo sababu eneo hili pakaitwa Kwa Haji tumbo”.

Ushahidi wa uchunguzi makini haukuonesha kuwepo kwa huyo mfanyabiashara anayeitwa Haji wala hilo duka lake kutokana na kutokuwepo kwa mtu huyo limebakia jina tu.

#### 4.2.23.2 Kigezo cha Uanzilishwaji wa Jina la Kwa Hajitumbo

Kigezo kilichotumika kuanzishwa kwa jina la Kwa Haj tumbo ni kigezo cha kiuchumi, kinachotokana na mtu huyu ka duka katika eneo hilo lililompatia umaarufu mkubwa na kupelekea eneo hili kupewa jina hilo. Matokeo haya yanalingana na maelezo ya Arthur (ameshatajwa) ambaye anaeleza kuwa jina la pahala linaweza kutokana na jina la mtu maarufu au umbile asilia.

#### 4.2.23.3 Umuhimu wa Jina la Kwa Hajitumbo Katika Lugha ya Kiswahili

Jina la Kwa Haji Tumbo linatokana na maneno matatu tofauti yenye maana tofauti. Neno la mwanzo "***kwa***" ambalo linamaanisha neno linalofata ni jina la mtu, neno la pili ni "***Haji"*** ambalo ni jina la mtu mwenye jinsia ya kiume, na neno la tatu ni "***tumbo"*** ambalo maana yake ni sehemu ya kiwiliwili iliyo kati ya kifua na kinena (TUKI, 2004). Umuhimu wa mwanzo ni kutokana na maneno haya matatu tunapata neno jingine Kwa Hajitumbo ambapo maana yake ni eneo ambalo alokuwa anaishi mtu aliyeitwa Haji ambae alikuwa ana tumbo kubwa.  Pia umuhimu mwingine jina hili linatokana na moja ya njia ya uundaji wa misamiati ya Kiswahili ya uambatishaji maneno. Wakaazi wa eneo hili wanapenda jina hili la Kwa Hajitumbo libakie hivi hivi lisibadilishwe kwa sababu ni jina la asili, maarufu na wamelizoea.

### 4.2.24 Mtaa wa Kidongochekundu

Mtaa wa Kidongochekundu ni mtaa uliopo katika wilaya ya Mjini Unguja katika mkoa wa Mjini Magharibi. Mtaa huu wa Kidongochekundu unapakana na mitaa ya Jang'ombe, Meya, Sogea, Kwaboko, na Mwembematarumbeta. Mitaa midogomidogo iliyomo kwenye mtaa huu ni Branch, Kidongochekundu skuli, Msikiti shurba na Mental hospital

#### 4.2.24.1 Asili na Mchakato wa Kuanzishwa Jina la Kidongochekundu

Data zilizotokana na mahojiano na dodoso zinaonesha kuwa jina la Kidongochekundu lilianzishwa kabla ya mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964. Jina hili lilianzishwa na wakaazi wa eneo hili kutokana na eneo hilo kuwa na udongo

wenye rangi nyekundu. Kwa mujibu wa maelezo ya mmoja wa wakaazi wa eneo hili ni anaeleza kwamba:

> "kuwepo kwa udongo wenye rangi nyekundu katika eneo hilo, ndiyo sababu iliyopelekea eneo hilo pakaitwa Kidongo chekundu".

#### 4.2.24.2 Kigezo cha Uanzilishwaji wa Jina la Kidongochekundu

Kigezo kilichotumika kuanzishwa jina la Kidongochekundu ni kigezo cha maumbile asilia ya eneo hili, ambalo rangi ya udongo wake ni nyekundu. Matokeo haya yanakubaliana na maelezo ya Arthur (ameshatajwa) ambaye ameeleza kuwa jina la pahala linaweza kutokana na jina la mtu maarufu au umbile asilia.

#### 4.2.24.3 Umuhimu wa Jina la Kidongochekundu Katika Lugha ya Kiswahili

Jina hili linatokana na maneno mawili tofauti yenye maana tofauti. Neno la mwanzo ni Kidongo ambalo **"Ki**" huonesha udogoshi na dongo inatokana na neno "***udongo"*** ambayo maana yake ni ardhi ya juu kwenye uso wa nchi ambapo aghlabu mimea huweza kuota (TUKI, 2014). Na neno la pili ni **"chekundu"** ambalo linatokana na neno "ekundu" ambayo maana yake ni rangi inayofanana na damu (TUKI, 2014). Umuhimu wa mwanzo wa jina hili unatokana na maneno hayo mawili tunapata neno jingine Kidongochekundu ambalo maana yake ni mahala ambapo kuna udongo mwekundu.Umuhimu mwingine jina hili linatokana na njia moja wapo ya uundaji wa misamiati ya Kiswahili ya uambatishaji maneno. Wakaazi wa mtaa huu wanapenda jina hili libakie hivi hivi lisibadilishwe kwa sababu wamelizoea, maarufu na la asili.

### 4.2.25 Mtaa wa Mwembeladu

Mtaa wa Mwembeladu upo katika wilaya ya Mjini Unguja katika mkoa wa Mjini Magharibi. Mitaa iliyopakana na mtaa huu ni Mwembemimba, Mfereji wa wima,

Bizredi na Mitiulaya. Wakaazi wa eneo hili wanajishughulisha na shughuli za ufundi wa magari, shughuli za biashara na pia kuna kituo kikuu cha gari za kwendea mashamba. Mitaa midogo midogo iliyomo katika mtaa wa Mwembeladu ni Mwembeladu stendi, Mwembeladu gereji (Rejea ramani nambari 2 kwenye viambatanisho).

#### 4.2.25.1 Asili na Mchakato wa Kuanzishwa Jina la Mwembeladu

Kutokana na data za mahojiano ambazo zinaonesha kuwa jina la Mwembeladu lilianzishwa kabla ya mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964. Jina hili lilianzishwa na wenyeji wa eneo hilo kutokana na kuwepo kwa mwembe uliokuwa unauzwa ladu. Mmoja wa wahusika wa utafiti huu anaeleza kuwa:

> Katika eneo hili palikuwa na mwembe ambao ulikuwa unauzwa ladu, watu wa maeneo mbalimbali walikuwa wanakuja kuuza na kununua ladu".

Ladu ni andazi gumu la mviringo litengenezwalo kwa kutumia unga wa mtama, mchele au dengu, unaochanganywa na vitu mbalimbali kama vile sukari, asali, ufuta, tangawizi au pilipili manga (TUKI, 2014) (angalia picha nambari 9 kwenye viambatanisho). Ushahidi wa uchunguzi makini umeonesha kuwa mwembe huo kwa sasa haupo tena limebakia jina tu.



**Picha Na 4.8: Ladu Za Ufuta**

Channzo: http://4.bp.blogspot.com/ (Imepatikana 24.9.2016)

#### 4.2.25.2 Kigezo cha Uanzilishwaji wa Jina la Mwembeladu

Kigezo kilichotumika kuanzishwa kwa jina la mtaa huu ni kigezo cha shughuli za kiuchumi, ambapo watu kutoka sehemu mbalimbali walikuwa wanauza ladu kwenye mwembe huo ili kupata kipato cha kuwasaidia kuendeleza maisha yao.

#### 4.2.25.3 Umuhimu wa Jina la Mwembeladu Katika Lugha ya Kiswahili

Mwembeladu inatokana na muunganiko wa maneno mawili tofauti yenye maana tofauti. Neno la mwanzo ni ***"mwembe"*** lenye maana ya mti mkubwa wenye majani marefu na membamba kiasi, magome magumu, unazaa embe lenye ganda laini, kokwa moja, nyama laini na tamu linapoiva (TUKI, 2014). Neno la pili ni "***ladu"*** ambalo tumeshalielezea maana yake.

Umuhimu wa mwanzo wa jina hili unatokana na maneno haya mawili tofauti tunapata neno jingine Mwembeladu lenye maana ya pahala penye mwembe ambao ulikuwa unauzwa ladu. Vile vile, umuhimu mwingine jina hili linatokana na njia moja wapo ya uundaji wa misamiati ya Kiswahili ya uambatishaji maneno. Pia kuendelea kwa matumizi ya jina hili kunafanya lisisahaulike. Wakaazi wa eneo hili wanalipenda, wanalifurahia jina hili na wanataka liendelee kutumika lisibadilishwe kwa sababu ni jina maarufu, wamelizoea na jina la asili.

### 4.2.26 Mtaa wa Michenzani

Mtaa wa Michenzani ni mtaa uliopo katika wilaya ya Mjini Unguja katika mkoa wa Mjini Magharibi Unguja. Mtaa huu umepakana na mitaa ya Kisiwandui, Mwembetanga, Mwembeshauri, Mwembekisonge, Rahaleo, Mwembemadema,

Barastekipande na Kisimamajongoo .Shughuli zinazofanywa katika eneo hili ni biashara, ufundi na utalii kutokana na kuwepo mnara wa kumbukumbu (Rejea ramani nambari 2 kwenye viambatanisho).

### 4.2.26.1 Asili na Mchakato wa Kuanzishwa Jina la Michenzani

Kutokana na data za mahojiano na mapitio ya nyaraka zinaonesha kwamba jina la Michenzani lilianzishwa kabla ya mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964. Jina hili lilianzishwa na wenyeji yaani wakaazi wa eneo hili kutokana na kuwepo shamba la michenza katika eneo hilo. Mmoja wa wakaazi wa eneo hili anaeleza hivi:

> ”kulikuwa na shamba kubwa katika eneo hili ambalo lilikuwa na miti aina ya michenza, baadae michenza hiyo ilikatwa na yakajengwa makaazi ya watu katika eneo hilo na jina likabakia lile lile la Michenzani”.

Watafitiwa wa utafiti huu pia wanaeleza kuwa: baadae serikali ikajenga nyumba kubwa za fleti na ikawapa wananchi wakae katika nyumba hizo, jambo ambalo lilipelekea kuitwa eneo hili nyumba za Michenzani. Ushahidi wa uchunguzi makini haukuonesha kuwepo kwa miti hiyo ya michenza katika eneo hilo.

### 4.2.26.2 Kigezo cha Uanzilishwaji wa Jina la Michenzani

Kigezo kilichotumika kuanzishwa jina la Michenzani ni kigezo cha maumbile, kutokana na kuwa palikuwa na shamba la miti aina ya michenza katika eneo hilo.Matokeo haya yanalingana na maelezo ya Arthur (ameshatajwa) anafafanua kuwa jina la pahala liaeleza kazi ya pahala kama soko, ngome, shamba au umbile asilia.

#### 4.2.26.3 Umuhimu wa Jina la Michenzani Katika Lugha ya Kiswahili

Jina la Michenzani linatokana na neno ‘***michenza”*** ambayo ni miti jamii ya michungwa yenye majani membamba na matunda madogo madogo yenye maganda laini yanayomenyeka kwa urahisi (TUKI, 2014), na mofimu **–“ni”** ya pahala. Umuhimu mmoja wapo wa jina hili ni unatokana na matumizi ya njia moja wapo ya uundaji wa misamiati ya Kiswahili ya unyambuaji. Hivyo, jina hili linakuza misamiati ya lugha ya Kiswahili. Pia kutokana na matumizi ya jina hili kunafanya liendelee lisisahaulike. Vile vile kutokana na kuwepo nyumba za fleti zimenasibishwa na sehemu ambazo kuna nyumba kama hizi kama vile Gamba, Makunduchi na sehemu nyingine, mtu akitaka kumfahamisha au kumuelekeza maeneo yenye nyumba kama hizi anamwambia kwa mfano “Gamba kwenye nyumba kama za Michenzani” au “ Makunduchi kwenye nyumba kama za Michenzani”. Jina la Michenzani linatambulika na watu wengi hadi sasa na wakaazi wake wanalipenda libakie hivi hivi lisibadilishwe kwa sababu wamelizoea, maarufu na la asili.

### 4.2.27 Mtaa wa Kibandamaiti

Mtaa wa Kibandamaiti unapatikana katika wilaya ya Mjini Unguja katika mkoa wa Mjini Magharibi. Mtaa huu unapakana na mitaa ya Mikunguni, Sogea, Sebleni, Muungano na Amani.Wakaazi wa eneo hili wanajishughulisha na biashara mbalimbali na ufundi.

#### 4.2.27.1 Asili na Mchakato wa Kuanzishwa Jina la Kibandamaiti

Data za mahojiano na dodoso zinaonesha kuwa jina la Kibandamaiti lilianzishwa kabla ya mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964. Jina hili la Kibandamaiti

lilianzishwa na wenyeji wa mtaa huu kutokana na eneo hilo kuwa na makaburi na kibanda ambacho watu walikuwa wakija na maiti kwa ajili ya kuzika wanawaweka kwenye kibanda hicho kwa ajili ya kusubiri mazishi. Mmoja wa watafitiwa wa uchunguzi huu alieleza ifuatavyo;

> ……., "palikuwa na kibanda katika eneo hili, pia pana makaburi ambayo yalikuwa yamepangwa kwa safu yaani kwa mstari, watu walikuwa wanakuja na maiti halafu wanawaweka kwenye kibanda hicho kusubiri kuzikwa ndio sababu eneo hili likaitwa Kibandamaiti."

Ushahidi wa uchunguzi makini haukuonesha kuwepo kibanda hicho na watu hawazikwi tena katika eneo hilo. Maelezo ya mtafitiwa mwingine yanaeleza kuwa: kabla ya eneo hili kuitwa Kibandamaiti palikuwa panaitwa Makaburi msafa. Na sasa kuna majina mawili katika eneo hili Kibandamaiti na Uwanja wa demokrasia. Kupitia maelezo hayo Anna (ameshatajwa) anasema kuwa mara nyingi mvutano hutokea wakati majina ya pahala yaliyotumika na watu wa asili na majina mapya yaliyowekwa na serikali, kinachojitokeza ni kutumika yote mawili kwa wahusika tofauti, jamii hutumia yao na serikali hutumia yao kwa pahala pale pale.

#### 4.2.27.2 Kigezo cha Uanzilishwaji wa Jina la Kibandamaiti

Kigezo kilichotumika kuanzishwa kwa jina la Kibandamaiti ni kigezo cha kijamii, kwa sababu shughuli za mazishi hufanywa na watu pale mmoja wao anapofariki dunia.

#### 4.2.27.3 Umuhimu wa Jina la Kibandamaiti Katika Lugha ya Kiswahili

Jina hili linatokana na mwambatano wa maneno mawili tofauti yenye maana tofauti. Neno la kwanza ni ***"kibanda"*** ambalo maana yake ni kijumba kidogo kitumiwacho

kwa shughuli maalumu (TUKI, 2014). Neno la pili ni "***maiti"*** ambalo maana yake ni mfu (TUKI, 2014). Umuhimu wa jina hili mwanzo unatokana na maneno haya mawili tunapata neno jingine Kibandamaiti ambalo maana yake ni pahala palipokuwa wanawekwa maiti wakisubiri kuzikwa. Umuhimu mwingine jina hili linatokana na moja ya njia za uundaji wa misamiati ya lugha ya Kiswahili ya uambatishaji maneno. Vile vile kuendelea kwa matumizi ya jina hili kunafanya lisisahaulike. Jina la Kibandamaiti wakaazi wake wanalipenda na wanataka libakie hivi hivi kwani wamelizoea na jina maarufu.

### 4.2.28 Mtaa wa Mitiulaya

Mtaa wa Mitiulaya upo katika wilaya ya Mjini Unguja katika mkoa wa Mjini Magharibi. Mtaa huu unapakana na mitaa ya Mwembemimba, Gulioni, Makadara, Mwembeladu**.** Shughuli muhimu ya wakaazi wa mtaa huu ni kufanya biashara mbalimbali.

#### 4.2.28.1 Asili na Mchakato wa Kuanzishwa Jina la Mitiulaya

Data za mahojiano na dodoso zinaonesha kwamba jina la Mitiulaya lilianzishwa kabla ya mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964. Jina hili la Mitiulaya lilianzishwa na wenyeji wa mtaa huu kutokana na kuwepo miti ambayo inasadikiwa asili yake inatoka Ulaya kupandwa katika eneo hili. Mkaazi mmoja wa eneo hilo anafafanua kwamba:

> "kuwepo kwa miti ambayo inasadikiwa kuwa si ya Zanzibar inatoka nje ya nchi yaani Ulaya, hivyo miti hiyo ililetwa Zanzibar na ikapandwa katika eneo hilo na mpaka sasa hivi miti hii ipo katika eneo hili. Kutokana na kuwepo kwa miti hiyo katika eneo hilo ndio likaitwa Mitiulaya."

#### 4.2.28.2 Kigezo cha Uanzilishwaji wa Jina la Mitiulaya

Kigezo kilichotumika kuanzishwa kwa jina la Mitiulaya ni kigezo cha maumbile, kwa sababu miti hii ipo ni miti mikubwa na yenye kivuli kizuri.



**Picha Na 4.9: Mtaa wa Mitiulaya**

Chanzo: Mtafiti 2016

#### 4.2.28.3 Umuhimu wa Jina la Mitiulaya Katika Lugha ya Kiswahili

Jina la Mitiulaya linatokana na muunganiko wa maneno mawili tofauti yenye maana tofauti. Neno la mwanzo ni ***"miti"*** ambalo maana yake ni mimea inayoota ardhini (TUKI, 2014). Na neno la pili ni ***"Ulaya"*** ambalo maana yake ni bara lililopo kaskazini ya bara la Afrika linalojumuisha nchi kama vile Uingereza, Ufaransa, Italia, Ujerumani n.k. (TUKI, 2014).Umuhimu wa mwanzo wa jina hili unatokana na maneno hayo mawili tunapata neno jingine Mitiulaya ambapo maana yake ni pahala penye miti yenye asili ya Ulaya. Pia jina hili linatokana na njia ya uundaji wa misamiati ya Kiswahili ya uambatishaji maneno. Vile vile kuendelea kwa matumizi

ya jina hili kunafanya liendelee na lisisahaulike. Jina la Mitiulaya linatambulika na wengi hadi sasa, na wakaazi wa eneo hili wanapenda libakie hivi hivi lisibadilishwe kwa sababu wamelizoea, maarufu na la asili.

### 4.2.29 Mtaa wa Makadara

Mtaa wa Makadara upo katika wilaya ya Mjini Unguja katika mkoa wa Mjini Magharibi Unguja. Mtaa huu umepakana na mitaa ya Gulioni, Mwembemimba, Saateni na Mitiulaya. Mitaa midogo midogo iliyomo katika mtaa huu ni Kwa Mdoe, Msikiti zabibu, Mharitani.Wakaazi wa mtaa huu wanajishughulisha na biashara ndogondogo.

#### 4.2.29.1 Asili na Mchakato wa Kuanzishwa Jina la Makadara

Kwa mujibu wa data za mahojiano zinaonesha kuwa jina hili la Makadara lilianzishwa kabla ya mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964. Jina hili lilianzishwa na mtu mmoja na baadae likaenea kwa watu wingine. Mmoja wa wakaazi wa eneo hili anaeleza kuwa:

> ”hapo zamani kulikuwa na mwitu walikuwa watu hawaishi, baadae akatokea mtu akajenga kibanda katika eneo hilo akawa anaishi peke yake. Alipokuwa anakwenda kwenye shughuli zake au anapokutana na wenzake wakawa wanamuuliza anaishi wapi, akawa anajibu “naishi kule kwenye makadara yangu” akimaanisha alikokadiriwa na Mungu, ikaendelea hivyo, hata wale watu walipokuwa wanaulizana wenyewe anaishi wapi bwana yule, wakawa wanajibizana kuwa anaishi kwenye makadara yake ndio sababu eneo hili likapewa jina hilo.”

Ushahidi wa uchunguzi makini haukuonesha kuwepo kwa mwitu huo kwa sasa watu wanaishi na wanaendelea kupaita jina hilo la Makadara.

#### 4.2.29.2 Kigezo cha Uanzilishwaji wa Jina la Makadara

Kigezo kilichotumika kuitwa jina la Makadara ni kigezo cha kijamii, kwa sababu huyu mtu alikwenda kuishi katika eneo hilo pakiwa na msitu mkubwa na ikawa ndio makaazi yake peke yake akitegemea kadari ya Mungu amlinde na kumuhifadhi na mabaya yote.

#### 4.2.29.3 Umuhimu wa Jina la Makadara Katika Lugha ya Kiswahili

Umuhimu wa mwanzo wa jina la Makadara ni kuwa lina asili ya Kiarabu lenye maana ya nguvu au uwezo hususan wa Mwenyezi Mungu (TUKI, 2014), hivyo kutumika kwake katika jamii ya Kiswahili ni kutokana na njia moja wapo ya uundaji wa maneno ambayo ni kutohoa, njia hii ni ya kuazima maneno kutoka lugha moja kwenda nyingine. Kwa njia hii neno Makadara limeazimwa na kuingia katika lugha ya Kiswahili. Matumizi yake yamesaidia kukuza misamiati ya lugha ya Kiswahili kwani limeongeza maneno katika Kiswahili. Pia kutokana na matumizi ya jina hili kunafanya liendelee kutumika lisisahaulike kwa sababu vijana wa sasa hawalitumii sana neno hili makadara. Jina la Makadara wakaazi wake wanapenda libakie hivi hivi lisibadilishwe kwa sababu wamelizoea, maarufu na la asili. Pia linatambulika na wengi hadi sasa.

### 4.2.30 Mtaa wa Mwembeshauri

Mtaa wa Mwembeshauri unapatikana katika wilaya ya Mjini Unguja katika mkoa wa Mjini Magharibi. Mtaa huu umepakana na mitaa ya Michenzani, Miembeni, Rahaleo na Kariakoo.Wakaazi wa mtaa huu hujishughulisha na biashara ndogondogo na shughuli za ufundi mbalimbali.

#### 4.2.30.1 Asili na Mchakato wa Kuanzishwa Jina la Mwembeshauri

Data zilizotokana na mahojiano na dodoso zinaonesha kuwa jina la mtaa huu lilianzishwa kabla ya mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964. Wakaazi wa eneo hili ndio walioanzisha jina la mtaa huu kutokana na kuwepo mwembe ambao waliutumia wakaazi wa eneo hili kwa ajili ya kupeana ushauri wa matatizo mbalimbali yanayowakabili. Hoja hii ya chimbuko la jina la Mwembeshauri inathibitishwa na mkaazi mmoja wa eneo ambaye kwenye maelezo yake anasema ifuatavyo;

> “katika eneo hilo palikuwa na mwembe, na watu wengi waliokuwa wanakaa ni watu wazima wenye busara na hekima, jambo lililopelekea watu wenye matatizo na wanaohitaji ushauri kuwafuata watu wazima hao kwa lengo la kupata ushauri mbalimbali hasa katika mambo mbalimbali ya kijamii. Kama vile harusi, ugomvi wa kifamilia na mambo mengine. Kutokana na hali hiyo watu waliamua kupaita sehemu hiyo Mwembeshauri, wakimaanisha ni sehemu ambayo ushauri mzuri hupatikana.”

Ushahidi wa uchunguzi makini haukuonesha kuwepo kwa mwembe huo katika eneo hilo limebakia jina tu.

#### 4.2.30.2 Kigezo cha Uanzilishwaji wa Jina la Mwembeshauri

Kigezo kilichotumika kuanzishwa jina la Mwembeshauri ni kigezo cha kijamii, kutokana na kupatikana kwa ushauri mzuri na wa busara katika eneo hilo la mwembe.

#### 4.2.30.3 Umuhimu wa Jina la Mwembeshauri Katika Lugha ya Kiswahili

Jina la Mwembeshauri linatokana na mwambatano wa maneno mawili tofauti yenye maana tofauti. Neno la mwanzo ni “***mwembe”*** ambalo maana yake ni mti mkubwa wenye majani marefu na membamba kiasi, magome magumu na unazaa embe lenye

ganda laini, kokwa moja, nyama laini na tamu linapoiva (TUKI, 2014). Neno la pili ni "***shauri***" ambalo maana yake ni jambo linalohitaji kuzungumzwa au kujadiliwa na kutolewa maamuzi (TUKI, 2014). Umuhimu wa jina hili kwanza unatokana na maneno haya mawili, tunapata neno jingine Mwembeshauri ambapo ni pahala penye mwembe ambao watu walikuwa wanakwenda kwa ajili ya kupata ushauri. Vile vile linatokana na njia moja wapo wa njia za uundaji wa misamiati ya Kiswahili iitwayo uambatishaji maneno. Jina hili linatambulika na wengi hadi sasa, na wakaazi wake wanalipenda na wanataka libakie hivi hivi lisibadilishwe kwani la asili, maarufu na limezoeleka. Jedwali lifuatalo linaonesha muhtasari wa mjadala wetu kuhusiana na

**Jedwali 4.1 : Uchanganuzi wa Michakato ya Kiisimu ya Uundaji na Muundo wa Maneno**

| Na | Jina la mtaa | Kigezo cha chimbuko la jina la mtaa | Michakato ya kiisimu katika uundaji maneno na muundo wa maneno | |
|---|---|---|---|---|
| | | | **Njia za uundaji wa maneno** | **Muundo wa neno** |
| 1 | Shangani | kiuchumi | Njia ya Mnyambuliko<br>*Shanga + ni* (ya mahali) | N+kiambishi ‘ni’ |
| 2 | Forodhani | kiuchumi | Njia ya Mnyambuliko<br>*Forodha + ni* (ya mahali) | N+kiambishi ‘ni’ |
| 3 | Darajani | maumbile | Njia ya Mnyambuliko<br>*Daraja + ni* (ya mahali) | N+kiambishi ‘ni’ |
| 4 | Sokomuhogo | kiuchumi | Njia ya mwambatano<br>*soko + muhogo* | N + N |
| 5 | Hamamni | maumbile | Njia ya Mnyambuliko<br>*Hamam + ni(*ya mahali) | N+kiambishi ‘ni’ |
| 6 | Funguni | maumbile | Njia ya Mnyambuliko<br>*Fungu + ni* (ya mahali) | N+kiambishi ‘ni’ |
| 7 | Mnazi mmoja | maumbile | Njia ya mwambatano<br>*Mnazi + mmoja* | N + V |
| 8 | Mkunazini | maumbile | Njia ya Mnyambuliko<br>*Mkunazi + ni (ya mahali)* | N+kiambishi ‘ni’ |
| 9 | Gulioni | kiuchumi | Njia ya Mnyambuliko<br>*Gulio + ni (*ya mahali) | N+kiambishi ‘ni’ |
| 10 | Kisiwandui | kijamii | Njia ya mwambatano<br>*Kisiwa + ndui* | N + N |
| 11 | Mwembetanga | kiuchumi | Njia ya mwambatano<br>*Mwembe+tanga* | N + N |
| 12 | Kisimamajongoo | maumbile | Njia ya mwambatano<br>*Kisima + majongoo* | N + N |
| 13 | Mfereji wa wima | kijamii | Njia ya mwambatano<br>*Mfereji + wa + wima* | N + U + E |
| 14 | Mfenesi mazizi | maumbile | Njia ya mwambatano<br>*Mfenesi + mazizi* | N + N |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 15 | Mikunguni | maumbile | Njia ya mnyambuliko<br>*Mikungu + ni(*ya mahali*)* | N + kiambishi "ni" |
| 16 | Kaburikikombe | maumbile | Njia ya mwambatano<br>*Kaburi + kikombe* | N + N |
| 17 | Mwembebeni | kijamii | Njia ya mwambatano<br>*Mwembe + beni* | N + N |
| 18 | Mwembenjugu | kiuchumi | Njia ya mwambatano<br>*Mwembe + njugu* | N + N |
| 19 | Mwembemadema | kiuchumi | Njia ya mwambatano<br>*Mwembe + madema* | N + N |
| 20 | Mwembemimba | kijamii | Njia ya mwambatano<br>*Mwembe + mimba* | N + N |
| 21 | Shaurimoyo | maumbile | Njia ya mwambatano<br>*Shauri + moyo* | N + N |
| 22 | Mlandege | maumbile | Njia ya mwambatano<br>*Mla + ndege* | N + N |
| 23 | Kwa Hajitumbo | kiuchumi | Njia ya ambatano<br>Kwa + Haji + tumbo | U + N + N |
| 24 | Kidongochekundu | maumbile | Njia ya mwambatano<br>*Kidongo + chekundu* | N + V |
| 25 | Mwembeladu | kiuchumi | Njia ya mwambatano<br>*Mwembe + ladu* | N + N |
| 26 | Michenzani | maumbile | Njia ya mnyambuliko<br>*Michenza + ni* (ya mahali) | N + kiambishi "ni" |
| 27 | Kibandamaiti | kijamii | Njia ya mwambatano<br>*Kibanda + maiti* | N + N |
| 28 | Mitiulaya | maumbile | Njia ya mwambatano<br>*Miti + ulaya* | N + N |
| 29 | Makadara | kijamii | Njia ya kutohoa<br>*Makadara* | N |
| 30 | Mwembeshauri | kijamii | Njia ya mwambatano<br>*Mwembe + shauri* | N + N |

Mambo muhimu yafuatayo yamedhihirika kutokana na uchanganuzi uliofanywa kwenye sura hii:-

### 4.3 Vigezo vya Chimbuko la Majina

Majina ya mitaa katika wilaya ya Mjini Unguja yametokana na vigezo vikiwemo pamoja na kigezo cha kiuchumi, kigezo cha kijamii na kigezo cha maumbile.

#### 4.3.1 Kigezo cha Kiuchumi

Majina yatokanayo na kigezo cha kiuchumi ni yale ambayo chimbuko lake ni shughuli za kiuchumi (kama vile biashara na uvuvi) zilizokuwa zikifanywa kwenye eneo hilo, baadhi ya shughuli za kiuchumi za biashara ambazo zilianzisha majina ya mitaa ya wilaya ya Mjini Unguja ni pamoja na bidhaa mbalimbali kama vile *ladu* (Mwembeladu), *njugu* (Mwembenjugu), *shanga* (Shangani), *muhogo* (Sokomuhogo). Baadhi ya shughuli za kiuchumi za uvuvi ambazo zilianzisha majina ya mitaa katika wilaya ya Mjini Unguja ni *madema* (Mwembemadema), *tanga* (Mwembetanga) nk. Katika utafiti huu, jumla ya majina 9 ambayo ni sawa na asilimia 30 ya majina yaliyofanyiwa utafiti yalitokana na kigezo cha kiuchumi.


#### 4.3.2 Kigezo cha Kijamii

Majina yaliyotokana na kigezo cha kijamii ni yale ambayo chimbuko lake lilikuwa shughuli mbalimbali za kijamii zilizokuwa zikifanywa kwenye eneo husika. Baadhi ya shughuli za kijamii zilizoibua majina ya mitaa ya wilaya ya Mjini Unguja ni pamoja na *kutoa ushauri* (Mwembeshauri), *kupiga beni* (Mwembebeni), *utekaji wa maji* (Mferejiwa wima), *uwekwaji wa wagonjwa wenye maradhi ya ndui* (Kisiwandui), *makaazi ya watu* (Makadara), *mazish*i (Kibandamaiti). Katika utafiti

huu jumla ya majina yaliyoibuliwa kutokana na kigezo cha kijamii ni majina 7 ambayo ni sawa na asilimia 20.

#### 4.3.3 Kigezo cha Maumbile

Majina yaliyotokana na kigezo cha maumbile ni yale ambayo chimbuko lake ni vitu mbalimbali asilia au vilivyotengenezwa na binaadamu ambavyo vipo kwenye sehemu, mkoa, nchi au bara fulani. Baadhi ya hali za kimaumbile asilia zilizoibua majina ya mitaa ya wilaya ya Mjini Unguja ni pamoja na *mizizi kwenye mfenesi* (Mfenesimazizi), *mti ambao ndege walikuwa wanakula tunda zake* (Mlandege), *michenza* (Michenzani), *mikungu* (Mikunguni), *fungu* (Funguni) *mikunazi* (Mkunazini), *udongo wenye rangi nyekundu* (Kidongochekundu), *miti ambayo asili yake ni kutoka bara la Ulaya* (Mitiulaya), *msitu* (Shaurimoyo), *kubakia kwa mnazi mmoja* (Mnazimmoja).




**Kielelezo Na 4.1: Vigezo Vilivyotumika Kuibua Majina ya Mitaa ya Wilaya ya Mjini Unguja**

Baadhi ya hali za kimaumbile zilizotengenezwa na binaadamu ambazo zimeibua majina ya mitaa katika wilaya ya Mjini Unguja ni *hodhi la kuogelea* (Hamamni), *daraja* (Darajani) na *kaburi* (Kaburikikombe). Katika utafiti huu jumla ya maneno yaliyotokana na majina yaliyoibuliwa kutokana kigezo cha maumbile ni 14 ambayo ni sawa na asilimia 50.

Kielelezo hiki kinaonesha kuwa kigezo kilichotumika zaidi katika kuibua majina ya mitaa ya wilaya ya Mjini Unguja ni kigezo cha maumbile ambacho kilikuwa na asilimia 50 ya majina yote, kigezo kilichofuatia katika uibuaji wa majina ni kigezo cha shughuli za kiuchumi ambacho kilikuwa na asilimia 30 za majina yaliyotafitiwa.

### 4.3.4 Michakato ya Kiisimu ya Uundaji wa Maneno ya Majina ya Mitaa

Michakato ya kiisimu inaelezea njia mbalimbali za uundaji wa maneno ya majina ya mitaa na miundo mbalimbali iliyotumika katika kuunda maneno hayo. Maneno yaliyotumika kama majina ya mitaa katika wilaya ya Mjini Unguja yanatokana na njia mbalimbali za uundaji wa maneno, ambazo ni pamoja na njia ya mnyambuliko, njia ya mwambatano na njia ya kutohoa.

#### 4.3.1.1 Njia ya Mnyambuliko

Ni njia ya uundaji wa maneno ambapo viambishi mbalimbali huambikwa kwenye mzizi husika na kuunda neno jipya. Baadhi ya majina ya mitaakatika wilaya ya Mjini Unguja ambayo yanatokana na njia hii ni Mkunazini, Mikunguni, Forodhani nk.

Katika utafiti huu jumla ya majina yatokanayo na njia ya mnyambuliko ni 9 ambayo ni sawa na asilimia 30.


#### 4.3.1.2 Njia ya Mwambatano

Ni njia ya uundaji wa maneno inayohusishwa kuunganishwamaneno mawili kuunda neno moja jipya ambalo maana yake huwa tofauti na maneno ambayo yametumika kuunda neno hilo. Katika wilaya ya Mjini Unguja baadhi ya majina ya mitaa yenye maneno ambatano ni Kibandamaiti, Mwembenjugu, Mfenesimazizi,

Mwembeshauri nk. Katika utafiti huu jumla ya majina yatokanayo na njia ya mwambatano ni 20 ambayo ni sawa na asilimia 66.7.

#### 4.3.1.3 Njia ya Kutohoa

Utohoaji wa maneno ni njia ya kuchukua msamiati wa lugha fulani kisha kulitumia kama msamiati katika lugha nyingine. Katika wilaya ya Mjini Unguja jina la mtaa linalotokana na njia ya kutohoa ni Makadara, kwa hiyo katika utafiti huu ni jina moja tu ambalo limetokana na njia ya kutohoa ambayo ni sawa na asilimia 3.3.




**Kielelezo Na 4.2: Njia Zilizotumika Kuunda Maneno ya Majina ya Mitaa ya Wilaya ya Mjini Unguja**

Kwa mujibu wa kielelezo hiki, njia iliyoongoza kama njia ya uundaji wa maneno ya majina ya mitaa ni njia ya maneno mwambatano iliyokuwa na asilimia 66.7, ikifuatiwa na njia ya maneno mnyambuliko iliyokuwa na asilimia 26.7

### 4.3.5 Muunndo wa Maneno ya Mitaa

Maneno yaliyotumika kama majina ya mitaa katika wilaya ya Mjini Unguja ni ya miundo tofauti, kama vile muundo wa nomino moja pekee, muundo wa nomino nakiambishi "ni", muundo wa nomino na nomino, muundo wanomino na kivumishi, muundo wa kiunganishi, nomino na nomino, na muundo wa nomino, kiunganishi na kielezi.

#### 4.3.1.4 Muundo Wa Nomino Moja Pekee

Majina yaliyotokana na muundo wa nomino moja pekee ni yale ambayo yameundwa na nomino moja pekee bila ya kuingia kitu kingine. Mfano wa jina la mtaa katika wilaya ya Mjini Unguja ambalo limeundwa na nomino moja pekee ni Makadara. Kwa hiyo, katika utafiti huu jina moja tu limeundwa na nomino moja pekee ambayo ni sawa na asilimia 3.3

#### 4.3.1.5 Muundo wa Nomino na Kiambishi "Ni"

Majina yaliyotokana na muundo wa nomino na kiambishi "ni" ni yale ambayo yameundwa na nomino pamoja na mofimu "ni". Baadhi ya majina ambayo yameundwa kutokana na nomino na kiambishi "ni" katika wilaya ya Mjini Unguja ni pamoja na Mikunguni, Mkunazini, Michenzani, Forodhani, Shangani, Darajani, Hamamni na Gulioni.

Katika utafiti huu maneno yaliyotokana na majina yaliyoundwa kwa nomino na kiambishi “ni” ni majina 9 ambayo ni sawa na asilimia 30.

#### 4.3.1.6 Muundo wa Nomino na Nomino

Majina yaliyotokana na muundo wa nomino na nomino ni yale yaliyoundwa na nomino na nomino (maneno mwambatano). Majina ambayo yameundwa kutokana na nomino na nomino katika wilaya ya Mjini Unguja ni kama vile Mwembenjugu, Mwembemimba, Mwembemadema, Mwembeshauri, Sokomuhogo, Kisiwandui, Kisimamajongoo nk. Katika utafiti huu maneno yaliyotokana na majina yaliyoundwa kwa nomino na nomino ni majina 16 ambayo ni sawa na asilimia 53.3.

#### 4.3.1.7 Muundo wa Nomino na Kivumishi


Majina yaliyotokana na muundo wa nomino na kivumishi ni yale yaliyoundwa na nomino na kivumishi. Mfano wa majina ya mitaa katika wilaya ya Mjini Unguja ambayo yameundwa kwa nomino na kivumishi ni Mnazimmoja na Kidongochekundu. Katika utafiti huu majina yaliyoundwa kwa nomino na kivumishi ni majina 2 ambayo ni sawa na asilimia 6.7.

#### 4.3.1.8 Muundo wa Kiunganishi, Nomino na Nomino

Haya ni majina yaliyoundwa kutokana nakiunganishi, nomino na nomino. Jina ambalo limeundwa kutokana na muundo wa  kiunganishi, nomino na nomino katika majina ya mitaa katika wilaya ya Mjini Unguja ni Kwa Hajitumbo. Hivyo katika utafiti huu ni jina moja tu lililo katika muundo wa kiunganishi, nomino na nomino, ambayo ni sawa na asilimia 3.3.

#### 4.3.1.9 Muundo wa Nomino, Kiunganishi na Kielezi

Majina haya ni yale yaliyoundwa kutokana na nomino, kiunganishi na kielezi. Mfano wa jina la mtaa katika wilaya ya Mjini Unguja lililoundwa kutokana na muundo wa nomino, kiunganishi na kielezi ni Mfereji wa wima. Kwa hivyo katika utafiti huu ni jina moja tu katika wilaya ya Mjini Unguja lililo katika muundo wa nomino, kiunganishi na kielezi, ambayo ni sawa na asilimia 3.3.




**Kielelezo Na 4.3: Miundo ya maneno ya majina ya mitaa ya wilaya ya Mjini Unguja**

Kielelezo kinaonesha kuwa majina mengi zaidi ya mitaa ya Unguja mjini yana muundo wa muunganiko wa nomino na nomino kwa asilimia 53.3, yakifuatiwa na muundo wa nomino na kiambishi '*–ni*' yenye asilimia 30.

## 4.4 Hitimisho

Katika sura hii mtafiti amewasilisha data kulingana na malengo na maswali ya utafiti na amechanganua kwa kutumia mbinu ya maelezo na takwimu Ameeleza maeneo ilipo mitaa ya majina husika, asili na michakato ya kuitwa majina ya mitaa hiyo, vigezo vilivyotumika katika kuitwa majina ya mitaa hiyo, umuhimu wa majina ya mitaa hiyo katika kukuza lugha ya Kiswahili na kuhitimisha kwa kuonesha uchanganuzi wa vigezo vya chimbuko la majina, njia za uundaji wa maneno na miundo ya maneno.

Sura ifuatayo inaelezea muhtasari, hitimisho na mapendekezo.

# SURA YA TANO

## 5.0 MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 5.1 Utangulizi

Utangulizi na usuli wa mada umeelezwa kwenye sehemu ya kwanza ya utafiti huu. Mapitio ya maandishi yamefafanuliwa kwenye sehemu ya pili, mbinu za utafiti zimeelezwa kwenye sehemu ya tatu na uchanganuzi wa data umefafanuliwa zaidi kwenye sehemu ya nne. Sehemu hii ya tano itaeleza muhtasari wa utafiti, hitimisho pamoja na mapendekezo.

### 5.2 Muhtasari wa Utafiti

Utafiti huu ulichunguza michakato na mbinu zilizotumika katika uundaji wa maneno ya mitaa mbalimbali katika wilaya ya Mjini Unguja . Utafiti huu uliongozwa na malengo mahsusi matatu ambayo ni kueleza michakato iliyotumika kutoa majina ya mitaa ya wilaya ya Mjini Unguja, vigezo vilivyotumika katika kutoa majina ya mitaa ya wilaya ya Mjini Unguja na lengo la mwisho ni kubainisha umuhimu wa majina ya mitaa ya wilaya ya Mjini Unguja katika kukuza Kiswahili. Eneo lililotumika kufanyia utafiti huu ni wilaya ya Mjini Unguja. Muundo uliotumika ni wa maelezo. Mtafiti wa utafiti huu alitumia sampuli nasibu tabakishi na aliwateua watafitiwa 90 ili kupata data. Pia mtafiti alitumia mbinu mbalimbali za kukusanya data kama vile mahojiano (usaili), dodoso na mapitio ya nyaraka. Data zilizopatikana zilichambuliwa kwa njia ya maelezo. Na pia utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uumbaji iliyoasisiwa na mwanaisimu wa Kimarekani Sapir na kuendelezwa na mwanafunzi wake Whorf (2004).

## 5.3 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Matokeo ya utafiti huu yameonesha kuwa vigezo ambavyo vimetumika kutoa majina ya mitaa katika wilaya ya Mjini Unguja ni vigezo vya kijamii, kimaumbile na kiuchumi. Kigezo ambacho kimetumika zaidi katika utoaji wa majina katika wilaya ya Mjini Unguja ni kigezo cha maumbile. Pia utafiti huu umeonesha michakato mbalimbali iliyotumika katika kutoa majina ya mitaa ya wilaya ya Mjini Unguja kwamba majina mengi yalianza kabla ya mwaka 1964, wakaazi wa eneo husika hasa wazee wenye hekima ndio walioanza kutoa majina hayo, mengine yameanza na mtu mmoja na baadae kuenea eneo lote, pia majina hayo yameanza sehemu ndogo ambayo ina kitu fulani au mtu maarufu na baadae kuenea katika eneo kubwa. Kwa mfano, mtaa wa "Darajani" ulianzia sehemu ndogo tu yenye daraja lakini baadae likaenea katika eneo la karibu linalozunguka daraja lile, na mfano wa mchakato huo ndivyo ulivyotokezea katika mitaa mbalimbali ya wilaya ya Mjini Unguja kama Hamamni, Mnazimmoja nk.

Vilevile, utafiti huu umeonesha majina haya ya mitaa katika wilaya ya Mjini Unguja yana umuhimu mkubwa katika lugha ya Kiswahili kama vile kukuza misamiati ya lugha ya Kiswahili, hasa majina yenye maneno ambatano. Pia yamedumisha matumizi ya misamiati mbalimbali ya lugha ya Kiswahili kwa kuendelea dhana yake ileile asilia. Vilevile yamehusisha majina na shughuli ambazo zikifanywa na wakaazi wa eneo husika kama shughuli za kijamii, kiuchumi na kiutamaduni.

Pia majina haya ya mitaa yamechangia kuhifadhi maneno ambayo vizazi vya sasa hawayatumii kwa mfano maneno gulio na hamam. Hata hivyo, kubaki kutumika kwa

maneno ya majina haya kumeweza kutoa taswira ya jiografia ya maumbile yaliyokuwa yapo hapo zamani kama vile majina ya Mfenesimazizi, Gulioni, Funguni, Kisiwandui, Darajani nk. Kubaki kutumika majina hayo katika maeneo husika yamepelekea kuleta utambulisho wa wakaazi wa maeneo kati ya mmoja na mwengine na kuleta mashirikiano. Njia mbalimbali za uundaji wa misamiati zimetumika katika majina hayo kama vile kutohoa, unyambuaji na uambatishaji wa maneno. Njia ambayo imetumika zaidi katika kuunda maneno ya majina ya mitaa katika wilaya ya Mjini Unguja kwa mujibu wa utafiti huu ni njia ya uambatishaji wa maneno.

Vilevile utafiti huu umeonesha kuwa majina ya mitaa katika wilaya ya Mjini Unguja yanatokana na miundo mbalimbali ya maneno kama vile nomino moja pekee, nomino na kiambishi "ni", nomino na nomino, nomino na kivumishi, nomino, kiunganishi na kielezi, na hata kiunganishi,nomino na nomino. Muundo ambao umetumika zaidi ni muundo wa nomino na nomino.

## 5.4 Hitimisho

Majina mengi ya mitaa ya Mjini Unguja yameanza kabla ya mwaka 1964. Ni majina ambayo yamerithiwa kutoka kwa wazee na mababu waliotangulia mbele ya haki kwa miaka mingi iliyopita na mengi bado yanatumika mpaka leo.

Katika kuitwa majina ya mitaa ya wilaya ya Mjini Unguja, vigezo mbali mbali vilitumika kama vile vigezo vya kimaumbile, vigezo vya kijamii na vigezo vya kiuchumi.

Majina ya mitaa ya wilaya ya Mjini Unguja imepitia michakato mbali mbali mpaka ikafikia kutumika majina hayo katika sehemu husika, michakato hiyo ni pamoja na kuwepo na kudhihiri maumbile asilia au yaliyotengenezwa na binaadamu, watu wachache kuanza kuvutika na umbile hilo, baadhi ya maumbile hayo kuhusishwa na zinazofanyika kwenye umbile hilo kwa watu wengi zaidi na kusambaa jina la mtaa lenye umbile au shughuli inayofanyika kwenye sehemu hiyo kutoka sehemu ndogo ya shughuli au ya shughuli au umbile husika na kuenea kwa sehemu zilizo karibu na eneo husika.

Majina ya mitaa ya wilaya ya Mjini Unguja yamechangia sana katika kukuza lugha ya Kiswahili kwa kuongeza misamiati kwa mfano yameleta maneno ambatano na kudumisha matumizi ya lugha kwa kupitia majina yenyewe kutumiwa katika shughuli mbalimbali. Majina haya ya mitaa ya wilaya Mjini Unguja bado yanapendwa yaendeleee kutumika na wakaazi wengi wa maeneo husika ingawaje kuna dalili ya mengine kuanza kutoweka na kuzorota na pia kuanza kuzuka majina ya mitaa ambayo hayana asili ya lugha ya Kiswahili.

Sababu zinazochangia kupotea au kuzuka majina mengine ni kutoandikwa majina haya, kuanza kupotea asili yake na vijana kuiga majina mapya kutoka sehemu nyengine ndani na nje ya Tanzania. Bado wilaya ya Mjini Unguja ina urithi wa majina mengi yenye asili ya Kiswahili ambayo yana mchango mkubwa katika kukuza lugha ya Kiswahili. Majina ambayo yanapaswa yalindwe, yakuzwe na kuhifadhiwa kwa njia zote ili vizazi vijavyo vije kufaidika zaidi na kuzidi kukitumia

Kiswahili katika shughuli zao mbali mbali za kijamii, kiutamaduni, kiuchumi na kisiasa.

## 5.5 Mapendekezo ya Utekelezaji

Ili majina yenye asili ya Kiswahili yaendelee kutumika kwenye mitaa mbali mbali ya wilaya ya Mjini na wilaya nyingine Tanzania Visiwani na Tanzania Bara, mambo yafuatayo yafanyike:-

- Serikali iandike majina ya mitaa mbali mbali kwenye mitaa yote husika ili watu wazidi kujua na kuitumia.
- Taasisi ya Kiswahili na lugha za kigeni (TAKILUKI) na baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA) waboreshe vipindi vya kueleza majina ya mitaa mbali mbali kwa undani zaidi asili, maana na umuhimu wa mitaa yote ya wilaya ya Mjini Unguja pamoja na mitaa ya wilaya nyingine mbali mbali. Na vipindi hivyo viwe kwa televisheni na redio.
- Manispaa ya wilaya ya Mjin Unguja iweke sheria ndogo ndogo zitakazolinda urithi huu wa majina na kuzuia uanzishwaji wa majina mengine yasiyozingatia lugha yetu ya Kiswahili kwenye maeneo yote ya wilaya ya Mjini Unguja pamoja na wilaya nyingine.
- Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA) litowe machapisho mbali mbali kama vile vitabu, magazeti, vipeperushi vitavyolezea majina ya mitaa mbali mbali.
- Idara ya mipango miji iweke kitengo maalum katika kila manispaa na halmashauri ili kijishughulishe na kuweka mikakati na mbinu mbali mbali za kulinda na kuhifadhi majina ya mitaa katika kila wilaya.

- Baraza la manispaa na halmashauri yaKuendelea kutoa majina ya sehemu mpya kwenye wilaya ya Mjini au wilaya nyengine kwa kufuata vigezo walivyoviacha wazee na mababu zetu navyo ni vigezo vya kimaumbile, kijamii na kiuchumi.
- Baraza la sanaa Zanzibar (BASAZA) liwashauri watunzi wa vitabu vya riwaya na waigizaji wa maigizo, michezo na filamu mbali mbali kutumia majina ya Kiswahili ya mitaa ya wilaya ya Mjini Unguja na wilaya nyengine pale wanapofanya sanaa zao kwenye maeneo husika.
- Baraza la manispaa na Halmashauri ya wilaya ya mjini Unguja wafanye jitihada ya kuyabadilisha majina ya kigeni yalioitwa kwenye sehemu za wilaya ya Mjini na wilaya nyengine yawe majina ya Kiswahili.
- Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA) wahakikishe lugha ya Kiswahili inaendelea kukua kupitia majina ya mitaa mbali mbali Tanzania visiwani na Tanzania bara.
- Serikali inapotaka kuita jina la mtaa ishirikiane na wakaazi wa eneo husika katika kuita jina la mtaa huo, isiite jina jingine wakati wakaazi wenyewe wameshapaita jina sehemu hiyo bila ya kuwashirikisha wakaazi hao.

## 5.6 Tafiti za Baadae

Ili lugha yetu ya Kiswahili iendelee kuwa ni urithi kwa vizazi vya sasa na baadaye na iendelee kukua zaidi, mtafiti anapendekeza kwa siku za mbele zifanyike tafiti zifuatazo:-

- Utafiti wa majina ya mitaa midogo midogo iliyomo kwenye wilaya ya Mjini Unguja.

- Tafiti nyingine za majina ya mitaa katika wilaya mbali mbali za Unguja na Pemba.
- Mchango wa dini katika kukuza Kiswahili.
- Mchango wa siasa katika kukuza Kiswahili.

## MAREJELEO

Abeid, B. (2005). *"Makala ya Bakari Abeid"*: Baraza la Kiswahili Zanzibar, (Haijachapishwa).

Abshir, M. S. M. (2016). *Utambulisho wa Somo la Jiografia*. Tasnifu ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha kumbukumbu ya Abdul –rahman Al – Sumait Zanzibar (haijachapishwa).

Arthur, T. (1998). *Concise Oxford Companion to the English Language:* New York: Oxford University Press.

Cornevin, R. (1978). *The Standardization of the Spelling of Africa Names*: Toponymy and ethnonymys. Paris: UNESCO.

Crowley, E. K. (1962). *The History of South Perth*. Australia. Rigby Limited.

Drummond, P. (2014). *An analysis of Toponyms and Toponymic patterns in Eight Parishes of Upper Kelvin Basin.* London: University of Glasgow Press.

El Fas, M. (1978). *Toponymy and Ethnonymy as Scientific Aids to History*. *African Ethnonymys and Toponymys*. Paris: UNESCO.

Enon, J. C. (1998). *Educational Research Statistics and Measurement.* Kampala: Makerere University Press.

Guma, C. (2011). The culture meaning of name among Basotho of Southern African. A Historical and Linguistic Analysis, *Nordic Journal of Africa Studio* 10(3): 265-279. Imepatikana tarehe 21/5/2016 kutoka www.njas.helsinki.fi/pdf-files/vol10num3/guma.pdf.

Haji, M. M. (2014). Uchanganuzi wa kiisimu jamii na mifumo ya utoaji wa majina ya mitaa katika Mkoa wa Kusini Unguja. Tasnifu ya M.A Kiswahili, Chuo Kikuu cha Kiislamu Uganda, (haijachapishwa).

Hammersley, M., Traianou, A. (2012). *Ethics and Educational Research.* London: BERA.

Joho, H. A. (2011). *Matumizi ya majina katika utambulisho wa jamii ya Watanzania*. Tasnifu ya M.A Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (haijachapishwa).

Juma, M. A. (2011). Ulinganishi Wa Kimakunduchi, Kimtende, Kibwejuu Na Kimakunduchi. Tasnifu ya M.A Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (haijachapishwa).

Kadmon, N. (2000). *Toponymy, the role, laws and language of Geographical Names*. New York: Vontage Press.

Kadmon, N. (2004). Toponym and Geopolities: The Political Use and Misuse of Geographical Names: *The Cartographic Journal*, 41(2), 85-87. Imepatikana kutoka www.iwp.edu/docLib/20131022....pdf tarehe 13/1/2017.

Khamis, A. A. (2003). *Uchambuzi halisi wa matumizi ya Kiswahili Asili Sekondari na Vyuo*, Chuo Kikuu cha Elimu Zanzibar.

Khamis, A. A. (2011). *Uchambuzi wa Kiswahili Fasaha (Sarufi na Lughawiya).*

King, J. (2008). *Analytical Tools for Toponymy*: Their application to Scottish Hydronymy a Thesis submitted for the degree of Doctor of Philosophy, University of Edinburgh.

Kombo, A. A., na wenzake. (2015). *Asili na Historia ya Majina ya Mitaa ya Fukuchani*. Chuo Kikuu cha kumbukumbu ya Abdul –rahman Al – Sumait. Zanzibar (haijachapishwa).

Kothari, C. R. (2004). *Research Methodology*: *Methods and Techniques*, New Delhi: New Age International (P) Ltd.

Langford, G. (2013). *Examine the value of place name as evidence for the history, landscapeall especially, language(s) of your chosen area* .Volume 5:. The University of Nottergham, school of England. INNERVATE leading undergraduate work in English studies, volume 5(pp 24-38).

Lehrer, A. (1992).*NamesandNaming: WhyweNeedFieldsandFrame: USA: University* of Arizona.

Majapela, P. (2009). *''Namna ngeli zinavyosaidia kuunda majina ya watu*'' M.A Dissertation. University of Dar-es-salaam.Haijachapishwa.

Makame, K. O. (2001). *Uhusiano wa vitendawili na masomo mengine yanafundishwa katika shule za Zanzibar*. Tasnifu ya M.A. Kiswahili, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (haijachapishwa).

Masebo, J. A. & Nyangwine, N. (2004). *Nadharia ya Lugha ya Kiswahili 1*. Kidato Cha 5 Na 6. Dar es Salaam: Nyambari Nyangwine Publisher.

Masoud, A. M. (2014). *Mchango wa majina ya Vijiji vya Donge katika kuhifadhi Historia ya Unguja*. Tasnifu ya M.A. Kiswahili, Chuo Kikuu cha Waislamu Morogoro, (haijachapishwa).

Massamba, D. P. (2003). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: TUKI.

Mazhar, A. S. (2013). *Research Methodology in social science*. Unguja: UCEZ Press.

Mukuthuria, M. (2010). Maadili ya Utafiti. *African Journals Online*. 73(1): AJOL. Imepatikana kutoka https://www.ajol.info/index.php/ksh/article/view/ tarahe 11/2/2017.

Mzee, S. Y. (2014). Nafasi ya majina ya Mizimu na Pepo za Makunduchi katika kuhifadhi utamaduni wa Makunduchi. Tasnifu ya M.A Kiswahili, *Chuo Kikuu cha Kiislamu Morogoro*, (haijachapishwa).

Nieminen, A. (1998). The Cultural Politics of Place Naming in QUEBEC: toponymic negotiation and struggle in Aborigonal territories. Collection of Theses, University of Ottawa, Canada. Imepatikana tarege 25/3/2017 kutoka https://www.ruor.uottawa.ca/handle/10393/4180.

Njozi, H. M. (2010). *Muslim and the state in Tanzania.* Dar es Salaam: Dumt.

NSW Heritage Office. (2004). *Place Names of Heritage Value:* A Heritage Council Policy. Imepatikana tarehe 23/02/2017 kutoka www.heritage.nsw.gov.au.

Pandu, R. S. (2014). *Asili na maana ya majina ya shule za Unguja mijini katika kutunza Historia ya Zanzibar*. Tasnifu ya M.A Kiswahili, Chuo Kikuu cha Kiislamu Morogoro, (haijachapishwa).

Pons, V. (1992). *Introduction to social Research*. Tanzania: Dar es Salaam: University Press.

Rawnsley, A. C. (2015). Policy, procedures and Guidelines for Research Ethic, Teesside University. Imepatikana tarehe 30/3/2017 kutoka https://www.tees.ac.uk/docs/DocRepo/Research/ethics.pdf.

Saparov, A. (2003). The alteration of place names and construction of national identity in Soviet Armenia. *Cahiers du Monde russe,* 44(1), 179 - 198. Imepatikana kutoka http://monderusse.revues.org/docannexe4079.html tarehe 29/4/2017.

The United Republic of Tanzania. (2013). *2012 Population and Housing census*. Dar es Salaam: Government Printer.

TUKI, (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.* Dar es Salaam: Oxford University Press.

Van den Hoonard, W. (2011). *The Seduction of Ethics: Transforming the social sciences*. Toronto: Toronto University Press.

Wardhaugh, R. (1992). *Intoductory Sociologuistic*. New York: Blackwell Publishers Ltd.

White, J. & Fitzgerald, T. (2010). Researcher tales and research ethics: the spaces in which we find ourselves, *International Journal of Research & Method in Education* 33(3), 273–285. Imepatikana tarehe 23/6/2017 kutoka www.tandfonline.com/doi/full/10.1080/1743727X.2010.511711?src=recsys.

Yai, O. (1978). *African Ethnonymy and Toponymy*: *Reflection on decolonization.* Paris: UNESCO.

Zubeir, Z. S. (2015). *Etimolojia ya majina ya mahali ya Kaskazini Pemba kuwa utambulisho wa utamaduni wa wapemba*. Tasnifu ya M.A. Kiswahili, Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania, (haijachapiswa).

# VIAMBATISHO

## KIAMBATANISHO NA. I :

## HOJAJI KWA WAZEE NA VIJANA WA WILAYA YA MJINI UNGUJA KWA AJILI YA KUCHUNGUZA ASILI YA MAJINA YA MITAA KATIKA WILAYA YA MJINI UNGUJA KATIKA KUKUZA KISWAHILI

**UTANGULIZI: Mtafiti** wa utafiti huu ni mwanafunzi wa Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania. Ambaye anasomea fani ya Kiswahili katika kiwango shahada ya uzamili. Anafanya utafiti unaohusu mada ya asili ya majina ya mitaa katika kukuza Kiswahili . Majibu utakayotoa mtafitiwa yatakuwa ni siri na yatatumika kwa madhumuni ya utafiti huu tu na si vinginevyo. Kwa hivyo naomba mashirikiano yako ya dhati katika kukamilisha kazi hii.

**SEHEMU YA KWANZA: MAELEZO YA MSINGI**

1. Mtaa anaoishi mtafitiwa ………………………………
2. Muda wa kuishi katika mtaa: ………………………………………………….
3. Jinsia: mwanamme [ ] mwanamke [ ]
4. Umri wa mtafitiwa: …………………………..
5. Kiwango cha elimu:[ sijasoma] [msingi] [ kidato cha nne] [kidatu cha sita] [cheti] [ diploma] [chuo kikuu].
6. Hali ya kifamilia: [ sijaoa/sijaolewa] [nimeoa/nimeolewa] [ nimeachika] [kizuka]
7. Kazi: ……………………………………………………………

**SEHEMU YA PILI: MASWALI YANAYOBAINISHA VIGEZO AMBAVYO HUTUMIKA KATIKA KUTOA MAJINA YA MITAA**

8. Jina la mtaa huu lilianza lini? …………………………………………
9. Nini maana ya jina la mtaa huu?....................................................................
10. Ni nani aliyeanzisha jina la mtaa huu ? ……………………………….
11. Kwa nini limeaaaanzishwa jina la mtaa huu? ……………………………
12. Ni vigezo vipi au mambo yepi yametumika katika kuanzisha jina la mtaa huu?
    (a) Vigezo vya kisiasa (b) vigezo vya kiuchumi (c) vigezo vya kijamii (d) vigezo vya kiutamaduni (e) vigezo vya kimaumbile (f) vigezo vyenginevyo (vitaje)…………

**SEHEMU YA TATU: MASWALI YANAYOELEZEA MICHAKATO INAYOTUMIKA KATIKA KUTOA MAJINA YA MITAA**

13. Ni hatua zipi zimetumika katika kuanzisha jina la mtaa huu? ……………………………………………………………………………...
14. Kabla ya kuanzishwa jina hili palikuwa panaitwaje?
    ……………………………………………………………………………....
15. Na hilo jina lake la mwanzo linatokana na kitu gani?
    ……………………………………………………………………………....
16. Je kuna majina mengine mbadala yanayotumika katika mtaa huu? (a)Yapo (b)Hapana
17. Sababu gani iliyopelekea kuzuka majina mbadala?
    ……………………………………………………………………………...
18. Jina la sasa linatambulika na wengi mpaka sasa? (a)Ndio (b)Hapana
19. Je kuna jina dogo linalokwenda sambamba na jina kubwa?) (a)Ndio (b)Hapana

20. Kama ndio ni sababu zipi zilizopelekea kuzuka kwa majina hayo?

…………………………………………………………………………....

**SEHEMU YA NNE :MASWALI YANAYOBAINISHA UMUHIMU WA MAJINA YA MITAA KATIKA KUKUZA LUGHA YA KISWAHILI**

21. Hili jina la mtaa linatokana na lugha ya Kiswahili? (a)Ndio (b)Hapana

22. Jina hili lina umuhimu gani katika lugha ya Kiswahili?

(a)Linakuza misamiati (b) Linaunganisha kati ya lugha na jamii husika

(c)Linaelezea dhana ya jina lililotumika kwa kutoa maana halisi ya jina lenyewe (d)Linawasaidia wakaazi katika kutumia vitamkwa, silabi,na muundo wa lugha ya Kiswahili (e) Linakuza na kudumisha matumizi ya lugha ya Kiswahili kupitia jina husika

(f)Umuhimu mwengine(utaje)…………………………………… …

23. Jina la mtaa linachangia kukuza lugha au linadumaza?

24. Kama linakuza ni kwa kiasi gani? (a)Kidogo (b)Kikubwa

(c) wastani

25. Na kama linadumaza ni kwa kiasi gani? (a)Kidogo (b)Kikubwa

(c) wastani

26. Je unapenda jina la mtaa huu libakie hivihivi au libadilishwe?

(a)Libakie (b)Libadilishwe

27. Kama libakie kwa nini?......................................................

28. Kama libadilishwe kwa nini?...............................................

29. Je ni hatua zipi zichukuliwe ili jina la mtaa huu lisisahaulike

………………………………………………………………………………

30. Je kutokana na jina hili la mtaa kuna athari yoyote iliyosababishwa na jina hili?

(a) Linatisha (b) Linashitua (c)Linafurahisha (d) linaudhi

(e)Athari nyingine (zitaje)…………………………

**AHSANTE KWA MASHIRIKIANO YAKO MAZURI**

# KIAMBATANISHO NA. II:

# MAHOJIANO KWA WASOMI NA WATAFITI WA WILAYA YA MJINI UNGUJA KWA AJILI YA KUCHUNGUZA ASILI YA MAJINA YA MITAA KATIKA WILAYA YA MJINI UNGUJA

## SEHEMU YA KWANZA: MAELEZO YA MSINGI

1. Mtaaa anaoishi mtafitiwa ………………………………
2. Muda wa kuishi katika mtaa: ………………………………………………….
3. Jinsia: mwanamme [ ] mwanamke [ ]
4. Umri wa mtafitiwa: …………………………..
5. Kiwango cha elimu:[ sijasoma] [msingi] [ kidato cha nne] [kidatu cha sita] [cheti] [ diploma] [chuo kikuu].
6. Hali ya kifamilia: [ sijaoa/sijaolewa] [nimeoa/nimeolewa] [ nimeachika] [kizuka]
7. Kazi: ……………………………………………………………

**KIAMBATANISHO NA: III**

**MASUALI YA MAHOJIANO**

1. Jina la mtaa huu lilianza lini?
2. Nini maana ya jina la mtaa huu?
3. Ni nani aliyeanzisha jina la mtaa huu?
4. Kwa nini limeanzishwa jina la mtaa huu?
5. Ni vigezo vipi au mambo yepi yametumika katika kuanzisha jina la mtaa huu?
6. Ni hatua zipi zimetumika katika kuanzisha jina la mtaa huu ?
7. Kabla ya kuanzishwa jina hili palikuwa panaitwaje
8. Na hilo jina lake la mwanzo linatokana na kitu gani?
9. Je kuna majina mengine mbadala yanayotumika katika mtaa huu?
10. Sababu gani iliyopelekea kuzuka majina mbadala?
11. Jina la sasa linatambulika na wengi mpaka sasa hapa mtaani ?
12. Je kuna majina madogo linalokwenda sambamba na jina kubwa (jina mama)?
13. Sababu zipi zilizopelekea kuzuka kwa majina hayo?
14. Hili jina la mtaa linatokana na lugha ya Kiswahili?
15. Jina hili lina umuhimu gani katika lugha ya Kiswahili ?
16. Je linachangia kukuza lugha au linadumaza? Kwa nini?
17. Kwa kiasi gani linakuza lugha ya Kiswahili?
18. Kwa kiasi gani linadumaza lugha ya Kiswahili?
19. Lugha ya Kiswahili inafaidika vipi kutokana na jina hili?
20. Je unapenda jina la mtaa huu libakie hivihivi au libadilishwe ? Na kwa nini?
21. Je ni hatua zipi zichukuliwe ili jina la mtaa huu lisisahaulike?

22. Hatua zinazopaswa kuchukuliwa na wanajamii (wakaazi wa mtaa)
23. Hatua zinazopaswa kuchukuliwa na serikali
24. Hatua zinazopaswa kuchukuliwa na wasomi (wataalamu wa lugha)
25. Je kutokana na jina hili la mtaa kuna athari yoyote iliyosababishwa na jina hili

**AHSANTE KWA MASHIRIKIANO YAKO MAZURI**